Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Tano - Tarehe 19 Juni, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 38

**Matatizo Yanayoikabili *PSRC***

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, *PSRC* inaendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali katika utekelezaji wa mipango ya Ubinafsishaji ikiwa ni pamoja na matatizo ya ugumu wa kuwapata wawekezaji wazuri wenye sifa na uwezo unaotakiwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na matatizo hayo?

(b) Je, kuna vigezo vyovyote vinavyowavunja moyo wawekezaji?

(c) Je, miundombinu yetu ya uwekezaji sio kikwazo kimojawapo cha kuwakimbiza wawekezaji?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji ulioanza kiasi cha miaka 14 (kumi na nne) iliyopita umekwenda vizuri na umeonyesha mafanikio ya kuridhisha kulingana na madhumuni yaliyowekwa. Jumla ya Mashirika 335 na mali zisizokuwa Mashirika 648 zimebinafsishwa.

Hadi sasa Kampuni/Mashirika 35 yapo katika hatua mbalimbali za kubinafsishwa. Katika kundi hili kuna Mashirika makubwa ya kudumu na miundombinu ambayo ubinafsishaji wake unafanywa kwa umakini na uangalifu mkubwa kwa utaratibu wa ukodishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji ulikumbwa na matatizo kadhaa, baadhi ya matatizo hayo ni:-

1. Mashirika mengi yalikuwa na madeni makubwa na hivyo yalishindwa kuvutia wawekezaji.

2. Viwanda vingi vilikuwa na mitambo iliyochakaa yenye teknolojia iliyopitwa na wakati na hivyo kushindwa kupata wawekezaji kirahisi.

3. Baadhi ya Mashirika yalishindwa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao katika Mifuko ya Pensheni na hivyo kuwasababishia wafanyakazi usumbufu mkubwa wanapokwenda kudai mafao yao ya pensheni wakati wa kustaafu au kupunguzwa kazi.

4. Watanzania wengi kukosa mitaji ya kuwekeza katika Mashirika waliyokabidhiwa kwa njia ya ubinafsishaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali wakati wote imekuwa ikikabiliana kikamilifu na matatizo hayo kwa kutumia mikakati mbalimbali ambayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kuwafanyia upekuzi na tathmini *(due diligence*) wawekezaji wote ili kubaini uwezo wao kiutendaji, kibiashara na kifedha na hivyo kuwachuja wawekezaji wasiofaa.

(ii) Wawekezaji Watanzania kupewa muda mrefu zaidi hadi (miezi 24) kukamilisha bei ya ununuzi wa Mashirika na kuwauzia kwa thamani ya vitabuni *(book values*). Hata hivyo, wawekezaji wa nje hununua Mashirika kwa bei za soko na wanatakiwa kukamilisha malipo wakati wa kusaini mkataba wa mauzo.

(a) Kutoa elimu ya ubinafsishaji kwa wawekezaji na wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari, vipeperushi, semina na mikutano ya hadhara kuhusu maana na umuhimu/faida ya sera ya ubinafsishaji na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengi yaliyowapata wawekezaji katika Mashirika yaliyobinafsishwa ni sawa na matatizo ambayo yamewakumba wawekezaji katika sekta nyingine za kiuchumi. Mifano wa matatizo hayo ni kama umeme, maji, usafirishaji, malalamiko ya kodi kubwa, migogoro ya kikazi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na matatizo hayo zikiwemo za kisheria, ili wawekezaji na wananchi wote kwa ujumla waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi, usalama na kwa gharama nafuu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha bainisha kwenye majibu yangu ya sehemu (b), Serikali inaendelea kutilia mkazo uboreshaji na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo inayohusika na uwekezaji ili iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya Taifa kiuchumi na kijamii.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri amesema kuwa matatizo yapo na mafanikio yapo. Lakini ukiangalia *PSRC* inamaliza muda wake ifikapo Desemba, 2007. Je, hiyo mikakati iliyowekwa itaweza kutatua tatizo ambalo lipo hivi sasa.

Pili, Mheshimiwa Waziri amesema kuwa matatizo yaliyopo yanalingana na mafanikio. Je, tathmini inaonyeshaje kuwa tumefanikiwa zaidi au tumepata hasara kulingana na uwekezaji uliopo Tanzania?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi matatizo haya si pekee kwa ajili ya Mashirika au Taasisi zilizobinafsishwa ni matatizo yanayohusu uchumi wote kwa ujumla. Ukichukua kwa mfano umeme na kadhalika. Kwa hiyo, haya ni matatizo ya wote sio ya wao peke yao. Lakini hatua tunazochukua ni hizi kama nilivyosema za kuboresha miundombinu yote ya maji, umeme, barabara ili kufanya uwekezaji uwe wa gharama nafuu.

Tathmini iliyofanywa kama nilivyosema kwenye jibu la msingi inaonyesha Sera ya Ubinafsishaji ina mafanikio makubwa zaidi kuliko matatizo. Kwa sababu kwanza unapimaje mafanikio ya ubinafsishaji. Unapima mafanikio ya ubinafsishaji kutokana na malengo yako uliyojiwekea. Lengo letu kubwa la kubinafsisha ni kwamba Mashirika haya mengi ya umma yalikuwa mzigo mkubwa kwa Serikali, hilo la kwanza. Lakini la pili, sera yetu pia tulishafika mahali tukasema Serikali si vizuri kufanya biashara.

Kwa hiyo, ukipima hayo kwanza Serikali imejivua kufanya biashara, pili, ule mzigo ambao tulikuwa tunaulipia kwa ajili ya kuendesha Mashirika tumeondokana nao. Kwa hiyo, hayo ni mafanikio makubwa. Fanikio lingine ni kwamba wananchi sasa wanamiliki uchumi, wanaendesha wenyewe sekta binafsi badala ya sisi Serikali kuendesha uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Na. 39

**Uhaba wa Mahakimu**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA (K.n.y. MHE. KHALIFA S. KHALIFA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi kuisaidia Mikoa ya Tanzania Zanzibar kwa kutoa shs. 100,000,000 kwa kila Mkoa na shs. 200,000,000/= kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ili zisaidie kuondoa umaskini:-

(a) Je, fedha hizo zimeshatumwa kwenye Mikoa husika sawasawa na ahadi ya Mheshimiwa Rais?

(b) Kama jibu ni 'ndiyo'. Je, zimetumika kwa mchanganuo gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA(MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya Bajeti ya mwaka 2007/2008 ilivyosema kwamba katika mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali ilianzisha awamu ya kwanza ya mpango maalum wa kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu kupitia Benki za *CRDB* na *NMB* kwa kudhaminiwa na Serikali. Mpango huu ulianza, mwezi Aprili, 2007 baada ya kukamilika kwa taratibu husika, awamu hiyo bado inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hivi sasa iko katika zoezi la kukamilisha taratibu kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya mpango huo itajumuisha Zanzibar. Maandalizi ya kuingiza Zanzibar katika mpango huo ni pamoja na kukubaliana kuhusu Benki itakayotoa mikopo hiyo, utaratibu wa usimamizi na uratibu wa mpango huo kama ilivyo kwa Tanzania Bara.

Na. 40

**Uhaba wa Mahakimu**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Hakimu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo huhudumia Mahakama zaidi ya tatu:-

Je, ni lini Serikali itaweza kuongeza Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo Wilayani Biharamulo?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashameza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Biharamulo ina jumla ya Mahakama za Mwanzo kumi na moja (11) ambazo ni:-

(a) Biharamulo Mjini;
(b) Ichwankima;
(c) Chatu;
(d) Mugaanza;
(e) Nyamirembe;
(f) Buselayombo;
(g) Bwanga;
(h) Buserasera;
(i) Runazi;
(j) Nyakahaura; na
(k) Isimbiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Biharamulo ina Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo saba (7). Kwa mantiki hiyo basi kuna Mahakama nne tu ambazo hazina Mahakimu na hizi hupewa huduma na Mahakimu 7 waliopo katika Mahakama zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kupeleka Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Wilayani Biharamulo kwani tunaamini kuwa Wilaya ya Biharamulo ina nafuu kidogo katika upungufu wa Mahakimu ukilinganisha na Wilaya zingine zilizo jirani na Wilaya ya Biharamulo.

Kwa mfano, Wilaya ya Ngara ina Mahakima 13 lakini ina Mahakimu 4 tu. Wilaya ya Bukoba ina Mahakama 25 lakini ina Mahakimu 7 tu. Hata hivyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mahakimu watapelekwa Biharamulo kadri hali inavyoruhusu. Kwa hivi sasa ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mahakimu 115 wa Mahakama za Mwanzo wameajiriwa na watagawanywa kwa kadri mahitaji yatakavyokuwa. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali. Ninayo maswali mawili.

Swali la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba sasa hivi Wilaya ya Biharamulo iliyo na Mahakimu hao aliowataja imegawanyika sasa hivi ni Wilaya mbili na Wilaya ya Biharamulo ina Mahakimu wawili tu?

Pili, anafahamu kwamba katika Mahakama zote hizo hakuna jengo la Mahakama na wala hakuna nyumba ya Hakimu hata Hakimu wa Wilaya anapanga. Anafikiri ni Hakimu gani atakayekubali kuja kulala chini ya miti? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Biharamulo imegawanyika Kimajimbo ya Uchaguzi. Lakini kugawanyika huku hakuna maana kwamba sasa Serikali haitaishughulikia Wilaya ya Biharamulo kuwapatia Mahakimu wanaowahitaji.

La pili, la matatizo ya nyumba hili lipo nchi nzima kwa kweli na katika mradi wetu mkubwa wa *Legal Sector Reform Programme* tunajenga Mahakama na nyumba za Mahakimu. Tutajitahidi basi kwa Wilaya yako ya Biharamulo kukufikia na mradi huu ili tukupatie angalau nyumba Mahakimu waweze kukaa hapo.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mahakama ya Mwanzo ya Kariakoo ni Mahakama ambayo toka mwanzo ilikuwa haitoshelezi kwa kazi za Kimahakama. Hivi sasa Mahakama ya Kariakoo katika Wilaya ya Ilala imeongezewa mzigo mkubwa wa Mahakama zingine kusogezwa katika Mahakama hiyo na kusababisha mahabusu kubaki ndani ya magari. Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia Mahakama zingine ili msongamano ule uondolewe katika Mahakama ya Kariakoo na Mahakimu wapate kufanya kazi zao kwa utaratibu unaohitajika?

**NAIBU SPIKA:** Lakini kwa kweli Mheshimiwa Chaurembo hili swali ni la Biharamulo sasa Kariakoo imeingiaje? (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na jitihada za Serikali za kuanzisha vyuo kwa ajili ya kufundishia Mahakimu ili waweze kukidhi haja katika Mahakama zetu za Mwanzo nchini. Lakini inaonekana kwamba hivi vyuo tulivyoanzisha kwa ajili ya Mahakimu wale wanaohitimu wanatumia kama daraja ili waweze kwenda kusoma zaidi na sio lengo la Serikali kwamba wakitoka pale waende Mahakamani kwa kufanya kazi.

Je, Serikali ina mkakati gani kuzuia haya ili tuendelee kupata Mahakimu ili waende kuziba mapengo katika Mahakama za Mwanzo nchini? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba vijana wengi wanapokwenda kusoma hasa katika Chuo chetu cha Lushoto wakishamaliza pale wanaitumia kama ngazi ya kwenda Chuo Kikuu wakapate digrii au mafunzo zaidi. Kwa maana hiyo ni kweli kwamba kuna upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo.

Tunachokusudia kufanya ni kuhakikisha kwamba kwa vile tunazalisha Wanasheria wengi sana wenye digrii basi tunakusudia hapo baadaye tuwashushe waje

kufanya kazi katika Mahakama hizi za Mwanzo na hii itasaidia zaidi kwa sababu sasa hivi Vyuo karibu vyote vinavyofundisha Sheria vinazalisha Wanasheria wengi sana. Mwaka jana tulipata karibu 826 na mwaka huu zaidi ya 1,000. Tunadhani hapo baadaye basi hawa watashuka hadi Mahakama za Mwanzo.

Na. 41

**Utekelezaji wa Sheria Nchini**

**MHE. OMAR S. KWAANGW' (K.n.y. MHE. DAMAS P. NAKEI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nchi yetu inaongozwa kwa Sheria mbali mbali na utawala wa nchi pia unazingatia haki na Sheria:-

(a) Je, ni kwa kiwango gani Sheria zinazotungwa na Bunge zinatekelezwa?

(b) Je, ni kwa nini wananchi wengi hawaogopi kuvunja sheria kama vile vitendo vya uendeshaji mbaya wa magari ya daladala, matusi, vitishio vya hadharani, uwekaji wa "*tinted glass*" kwenye magari, uendeshaji kasi wa magari unaosababisha ajali na kadhalika?

(c) Je, ni lini Watanzania wataanza kuogopa kuvunja Sheria pasipo kuwepo kwa Polisi karibu?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kila sheria hutungwa ili kukidhi mahitaji yaliyokusudiwa katika jamii. Ili sheria ifanye kazi iliyokusudiwa ni lazima iwekewe usimamizi na mamlaka itakayokuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa sheria hiyo inatumika kwa makusudi yaliyokusudiwa na si vinginevyo. Kwa maana hii Sheria zilizotungwa na Bunge zinatekelezwa kwa kiwango cha juu.

(b) Katika nchi yoyote inayoendeshwa kwa kuzingatia utawala wa sheria, wananchi hupaswa kuziheshimu sheria hizo. Inapotokea wananchi wengi wanavunja sheria, basi maana yake ni aidha kuna mapungufu katika usimamizi wa Sheria inayohusika au mapungufu katika sheria yenyewe au inawezekana yakawa ni matatizo ya wananchi wenyewe kutokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu sheria zinazohusika. Aidha, wakati mwingine inawezekana mtu akawa anafahamu vizuri sheria lakini kwa makusudi akaamua kuivunja akijua adhabu yake ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la kupambana na vitendo vya uhalifu, linalotakiwa kuzingatiwa ni kuwafanya wananchi waelewe umuhimu wa

kuzitumia, kuziheshimu na kuzilinda sheria za nchi. Katika kutekeleza azma hii Serikali imekuwa ikiwaelimisha wananchi kupitia vyombo vya habari na katika warsha mbalimbali kuhusu sheria za nchi na umuhimu wake kwa jamii.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi wataanza kuogopa kuvunja sheria pale tu watakapokuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu sheria hizo na pale usimamizi utakapokuwa umeimarishwa. Serikali inajitahidi kuimarisha vyombo vyake vya usimamizi wa Sheria hasa Jeshi la Polisi ili liweze kusimamia vizuri utekelezaji wa Sheria hizo. Wananchi nao pia ni walinzi wa sheria za nchi hivyo wanapaswa kushiriki katika usimamizi wa sheria kwa kukemea vitendo vya uvunjaji wa sheria.

**MHE. OMAR S. KWAANGW'**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kuelimisha wananchi kuhusu sheria mbalimbali na kwa kuwa vitovu vya maendeleo ya wananchi ni kijijini. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha nakala za sheria zinazotungwa hapa Bungeni zinafika hadi vijijini mahali ambapo wananchi wengi wangepaswa kuelewa sheria hizi?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sheria nyingi sasa hivi hazifiki vijijini. Lakini tatizo hili ni tatizo kubwa kwa sababu ni la uzalishaji wa hizo sheria zenyewe. Sheria zinapotungwa zinabidi zichapishwe na uchapishaji wake una gharama. Swali hili tuliwahi kulizungumza wakati tunazungumzia suala la Katiba. Swali ambalo liliulizwa kwa nini nakala za Katiba hazipatikani. Tatizo ni gharama tu lakini kadri tutakavyoweza kupata uwezo basi tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba sheria hizi zinafika vijijini ili wananchi wazitumie.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Omar Kwaangw' ameuliza *exactly* mimi nilichotaka kuuliza.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru tunaendelea

Na. 42

**Ajali za Barabarani**

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN NGWILIZI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ajali zinazosababishwa na vyombo vya usafiri wa barabarani, majini na hata kwa njia ya anga zimekuwa zikisababisha vifo na majeruhi wengi kwa Watanzania; na kwa kuwa, Sheria za Nchi zimeagiza kuwa, kila chombo kinachojihusisha na biashara ya kusafirisha abiria kwa njia yoyote ile hakina budi kiwe na Bima ili wasafiri waweze kulipwa fidia pindi ajali zinapotokea:-

(a) Je, ni ajali ngapi za barabarani, majini na anga zimetokea katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na ni abiria wangapi wamepoteza maisha na au kujeruhiwa, na kati ya hao ni abiria wangapi wamelipwa fidia kutokana na vyombo hivyo vya usafiri vilivyopata ajali hizo?

(b) Kwa kuwa, wananchi wengi wameathirika kutokana na ajali zinazosababishwa na vyombo hivyo vya usafiri, na wengi wao bado wanadai fidia wanazostahili huku wakiwa hawajui taratibu za kufuata ili kupata haki zote. Je, Serikali inatoa maelezo gani ili kuwasaidia wananchi hao kupata haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Jen. (Mstaafu) Hassan Athumani Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, naomba kutoa maelezo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika,Wizara ya Miundombinu ndiyo Wizara yenye dhamana ya kusimamia sekta ya usafiri na usafirishaji nchini kuhakikisha kuwa usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo unakuwa wa uhakika, salama na wa gharama nafuu kwa pande zote zinazohusika.

Katika kupambana na tatizo la ajali za barabarani, majini na angani Wizara inashirikiana na Jeshi la Polisi na imeanzisha vyombo vifuatavyo:-

· Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)*

· Kitengo cha Usalama Barabarani *(RSU)*

· Wakala wa Usalama

Majukumu ya msingi ya vyombo hivi ni kuweka sera na mikakati ili kuhakikisha kuwa tatizo la usalama katika sekta ya usafiri na usafirishaji linadhibitiwa. Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Brig. Jen. (Mstaafu) Hassan Athumani Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)(i) **Ajali za barabarani**

· Kwa kipindi cha mwaka 2005 zilitokea ajali 16,300 zilizosababisha vifo 2,430 na watu 16,286 walijeruhiwa

· Katika kipindi cha mwaka 2006 ajali zilikuwa 17,677 zilizosababisha vifo 2,884 na watu 15,766 walijeruhiwa

(ii) **Ajali za Majini -** Kwa kipindi cha 2005 ajali zilikuwa 11, tano zikiwa za baharini na 6 za ziwani. Vifo baharini ilikuwa ni mtu mmoja na majeruhi 2; vifo ziwani vilikuwa 41, na hakuna majeruhi. Wakati kwa mwaka 2006 jumla ya ajali zilikuwa 8 baharini na 7 za ziwani. Vifo vilikuwa vitano baharini na 117 ziwani. Majeruhi walikuwa 20 baharini na 61 ziwani.

(iii) **Ajali za Angani -** Ajali zilizotokea angani zilikuwa mbili mwaka 2005. Moja ilitokea Ziwa Victoria karibu na Mwanza iliyohusisha ndege ya *Air Trans Inc* na nyingine ndege ya Nomad Safari katika Milima ya Lubulungu, *Mahale National Park* Mkoa wa Kigoma. Mwaka 2006 zilitokea ajali 4 katika Mikoa ya Manyara, Kigoma, Mpanda na Mbeya zilizosababishwa na ndege zifuatazo; *Mission Aviation Fellowship*, Monuc *United Nation Mission* in *DRC, Two Wings* na *Tanzanair.*

Vifo vilivyosababishwa na ajali hizo vilikuwa 13 kwa mwaka 2005 na vinne kwa mwaka 2006. Hapakuwepo na majeruhi mwaka 2005 na mwaka 2006 kulikuwa na majeruhi watatu.

Takwimu zinaonyesha kuwa kwa upande wa Bima za Magari waliodai fidia mnamo mwaka 2005 walikuwa 697 na jumla ya fidia 366 zililipwa. Jumla ya gharama za fidia ilikuwa ni shilingi milioni 711.44. Madai 331 hayakulipwa mwaka huu kwa kutokamilika kwa uchambuzi wa uhalali wa kulipwa waliohusika.

Katika mwaka 2006 jumla ya madai ya fidia za Bima ya Magari zilizopokelewa yalikuwa 864 na kati ya hizo fidia 355 zililipwa. Jumla ya shilingi milioni 634.94 zilitolewa kwa madai halisi. Madai ambayo hayakulipwa fidia katika mwaka huo yalikuwa 509.

Kwa upande wa Bima za Majini hakuna madai yaliyolipwa, kadhalika hakuna madai yaliyolipwa katika ajali ya Bima ya vyombo vya angani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa baadhi ya wananchi wetu hawajui taratibu za kudai fidia na walio wengi hawana taarifa kuwa mtu anapopata ajali anastahili kulipwa fidia inayotokana na Bima ya chombo alichosafiria.

Wizara yangu kupitia taasisi zake za *Road Safety Unit* na *SUMATRA* imeanzisha kipindi cha *Radio* na kuchapisha kwenye magari kwa lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za abiria baada ya ajali. Aidha, Wizara yangu inashirikiana na Wizara ya Fedha ambayo inahusika na Bima katika kuelimisha umma, kuhusu taratibu za kutoa fidia kwa waliopatwa na ajali zilizosababisha vifo na majeruhi.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenye ufasaha ambayo yameonyesha ukubwa wa tatizo. Nina maswali madogo mawili ya kuuliza. La kwanza. Kwa kuwa tukichukua tu takwimu za mwaka 2005 kwamba ni ajali 16,300 watu 2,400 wamekufa 16,000 wamejeruhiwa lakini waliolipwa fidia miongoni

mwa hao wote 366. Je, hii haionyeshi jinsi gani ambavyo tunashindwa kusimamia haki za Watanzania ambao wanaumia?

La pili, kwa vile vyombo hivi vya usafiri vinavyosababisha ajali na umaskini kwa Watanzania inaelekea ajali hizo zinandelea kuongezeka, kwanini Serikali isiweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba chombo kinachosababisha ajali hakilipwi fidia yoyote mpaka wahanga wote wamelipwa kwanza? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU - MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wanaodai fidia ni wachache ukiangalia takwimu ambazo tumezitoa hapa. Lakini kama nilivyoeleza nadhani suala muhimu ni elimu. Sasa kama nilivyosema Wizara yangu na Wizara ya Fedha inaendelea kutoa elimu hiyo kwa programu mbalimbali.

Lakini ningewaomba vilevile wananchi na Waheshimiwa Wabunge wasaidie wapiga kura wao katika kutoa elimu hii kwamba unapopata ajali kwenye chombo cha usafiri ni vyema ukajua taratibu na ukafuatilia malipo yako ya bima. Tukisaidiana kwa pamoja katika kutoa elimu hiyo nadhani tutafika mahali ambapo wananchi wetu watajua haki zao.

Kuhusu swali la chombo kilichosababisha ajali kwanza kilipe fidia kama nilivyosema hili ni suala la Sheria na fidia huwezi kuanza kuilipa kabla yule aliyeumia au aliyepata madhara kuleta madai yake. Kwa hiyo, taratibu zitafuatwa kisheria lakini nieleza tu hapa kwamba Wizara yetu vilevile kwa sasa inaandaa sera na baadaye Sheria ya usalama barabarani. Hii itasaidia sana ikishirikiana na Sheria tuliyoipitisha ya barabara kuweza kudhibiti haya matatizo ya ajali na kuangalia kwa umakini namna gani tunaweza tukaepuka ajali za barabarani na kwenye vyombo vingine vya usafiri.

Na. 43

**Hitaji la Umeme Kijiji cha Kharumwa**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA (K.n.y. MHE. JAMES P. MUSALIKA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inatambua uhitaji wa umeme wa *Grid* kaitika Kijiji cha Kharumwa Wilayani Geita, na tayari njia za umeme huo kutoka Ibadakuli (Shinyanga) hadi Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu na kutoka Bulyanhulu – Mradi wa Maji wa Shinyanga na Kahama zinapita kijijini hapo na kwa kuwa, Waziri wa Nishati na Madini alipojibu swali langu Na. 56 katika Mkutano wa Tano wa Bunge aliiagiza *TANESCO* kupeleka wataalamu katika vijiji vya Kharumwa, Ikangala, Kitongo, Nyarubele, Kakora na Nyamtukuza ili kupata makisio ya gharama za mradi:-

(a) Je, *TANESCO* ilitekeleza agizo hilo?

(b) Kama agizo hilo limeshatekelezwa. Je, ni gharama kiasi gani zinahitajika katika mradi huo?

(c) Je, ni lini Mradi huo utatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'wale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* ilitekeleza agizo hilo kwa kupeleka wataalam kufanya tathmini mwezi Aprili, 2007. Wataalam hao walibaini kuwa kutokana na unyeti wa mitambo ya kusukuma maji ya Ihelele ambayo matumizi yake yanakadiriwa kuwa kiasi cha megawati 12, njia ya umeme inayojengwa sasa haiwezi kuunganishwa na wateja wengine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za utekelezaji wa mradi huo ni shilingi milioni 600. Kiasi hiki cha pesa kitawezesha kuvipatia umeme vijiji vya Kharumwa, Ikangala, Kitongo, Nyarubele, Kakora na Nyamtukuza baada ya kufanya mambo yafuatayo:-

(1) Kujenga njia ya aumeme wa kilovoti 33 na yenye urefu wa jumla ya kilomita 50 kutoka kituo cha kupozea umeme cha Bulyanhulu;

(2) Kufunga vipoza umeme katika vijiji vya Kharumwa, Ikangala, Kitongo, Nyarubele, Kakola na Nyamtukuza; na

(3) Kujenga njia za umeme wa msongo wa volti 400/230 zenye jumla ya urefu wa kilomita 10 na kuunganisha wateja wapatao 200.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhaba wa fedha na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, imekuwa vigumu Serikali kuutekeleza mradi huo kwa sasa. Aidha Serikali inaendelea na mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji w miradi ya umeme vijijini chini ya *Access Expansion Program (AEP)* ambayo itajumuisha na mradi huo.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuniruhusu niulize maswali mawili ya nyongeza. Inavyoonekana Serikali imekuwa ikipitisha nguzo za umeme au *TANESCO* imekuwa ikipitisha nguzo za umeme kwenye maeneo mbalimbali wananchi wanabaki wanaziangalia nguzo hizo kama kwenye vijiji vilivyotajwa ni muda mrefu na huwawekea simanzi. Haioni kwamba hilo ni tatizo?

La pili, mradi Serikali inapeleka umeme Bukombe kutoka Kakola na matatizo yaliyo katika Jimbo la Busanda yanafanana na matatizo yaliyo katika Jimbo la Nyang'wale umeme huo utapitia katika maeneo ya Bukoli, Nyarugusu, Rwamgasa na Katoto na wenyewe wataendelea kushangaa nguzo hizo. Je, Serikali ina mpango gani

kuwapa umeme wananchi hawa walio kwenye njia ambapo kuna madini chini na wanafanya kazi ya uchimbaji na wanahitaji umeme na maombi hayo nimeshayapeleka, Serikali inafikiria nini kuwawekea umeme wakati inapeleka umeme Bukombe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Kabuzi kwa sababu Wizara yangu imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana Mheshimiwa Kabuzi kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia upatikanaji wa umeme kwenye maeneo ya Jimbo lake kwa hiyo nampongeza sana. Lakini la kwanza kuhusu kwamba *TANESCO* imekuwa ikipitisha umeme nguzo zinasimikwa ama zinajengwa lakini wananchi katika maeneo husika wanakuwa hawapati huduma ya umeme, ninaomba kulieleza Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba huduma ya umeme inayotolewa na Shirika letu la *TANESCO* inaambatana na mambo mbalimbali mojawapo ni jambo la kitaalam.

Kuna nguzo ambazo zimekuwa zikipitishwa lakini zenye msongo mkubwa kiasi kwamba haziwezi kushushwa katika maeneo yote ambayo umeme huwa unapita. Kuna masuala ya kitaalam ya kufanya kwanza tathimini ijulikane, lakini pia kuna gharama zake za kushusha maeneo husika pia kuna masuala ya kibiashara kujiridhisha kama maeneo yanayopitiwa yanajitosheleza kukidhi utashi wa kibiashara kwa huduma inayotolewa ya umeme. Lakini nia ya Serikali ni kwamba ni kuwafikishia umeme wananchi wengi kadri itakavyowezekana.

Kuhusu swali la pili, ni kwamba kuna mradi wa umeme kutoka maeneo ya Bulyanhulu kutoka Kakora, kupitia vijiji vya Bukoli, Nyarugusu Rwamgasa, namwomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake linafanana na swali ama mahitaji ya maeneo mengi sana nchini. Kwa kweli naomba kuwaarifu wananchi kupitia Bunge lako kwamba Serikali inakamilisha maandalizi ya utekelezaji wa mradi ambao siku nyingi ambao tumekuwa tukiusemea mradi wa usambazaji wa umeme vijiji. Vijiji vilivyotajwa maombi yake yapo ofisini kwetu tunayafanyia kazi tunamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa kweli jambo hili la kuvuta subira tumelisema sana lakini naomba niseme kwa mara nyingine tena kwamba si muda mrefu utekelezaji wake huu utatekelezwa.

Na. 44

**Mkakati wa Kupiga Mila Potofu dhidi ya Wanawake Nchini.**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara husika inapiga vita mila na desturi potofu za makabila mbalimbali zinazokandamiza mwanamke hapa nchini; na kwa kuwa, utekelezaji wa zoezi hili unaweza kuchukua muda mrefu sana:-

Je, ni mbinu gani Serikali itazitumia ili kufupisha muda huo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika (Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto inaendelea na hatua za kupiga vita mila na destuli potofu za makabila mbalimbali ambazo zinamkandamiza na zinamletea madhara mwanamke hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, utekelezaji wa zoezi hilo, utachukua muda mrefu, hii ni kwa sababu mila na desturi hizo zimekuwa zikitumika tangu enzi na enzi na bado zinaendelea kutekelezwa na baadhi ya jamii zetu hapa nchini. Kwa hiyo, ili jamii zetu ziweze kuachana na mila hizo potofu inabidi kutumia mbinu mbalimbali shirikishi zitakazowezesha jamii kubadilisha mila desturi hizo. Mchakato huu wa kupinga mila potofu zinazokandamiza wanawake ni kazi inayohitaji juhudi za pamoja. Mila na desturi potofu zinaendelea kuleta madhara makubwa si kwa wanawake tu bali kwa jamii yote. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali inaendelea kutekeleza mbinu mbalimbali shirikishi ili kufupisha muda wa kuelimisha jamii katika kubadilisha fikra zao na hatimaye waweze kukataa na kuzitokomeza kabisa mila na desturi zote zenye kuleta, madhara kwa jamii, hususani wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbinu hizo shirikishi zinazotumiwa na Serikali ni pamoja na:-

· Mikutano ya hadhara na Semina ili kuelimisha jamii kuhusu madhara ya mila desturi potofu ambazo ndizo zinazomkandamiza mwanamke, kama vile ndoa za utotoni unyanyasaji, ukeketaji uuwaji wa vikongwe na nyingine nyingi. Katika ngazi ya Halmashauri kazi hii inafanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ugani waliopo kuanzia katika ngazi ya Kata.

· Kutumia maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani na Siku ya Mtoto wa Afrika kuelemisha na kuhamasisha jamii kuhusu mila potofu na zinazoleta madhara na kukandamiza wanawake.

· Kutumia vyombo vya habari kuelimisha jamii, kwa mfano *radio, TV,* magazeti, ngoma za asili na kadhalika.

· Kushirikiana na wazee na kujadili suala la mila zenye kuleta madhara ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu, kwa kuwa wao wakikataza mila hizo hazitaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali ili kuondoa mila zote potofu ikiwemo ya ukeketaji. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kuchukua nafasi hii kuyashukuru na kuyapongeza Mashirika yote yasiyo ya Kiserikali kwa ushirikiano wao na juhudi wanazoendelea nazo za kuondoa mila zote potofu ambazo zinazomkandamiza mwanamke.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mkakati maalum wa kupiga vita mila potofu. Je, ni maeneo gani ya Tanzania yanayoongoza kwa ukeketaji na uuwaji wa vikongwe kwa imani za uchawi na ni adhabu gani zilizowahi kutolewa kwa wanawake wanaogundulika kwa kukeketa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Maeneo ambayo yanaendeleza sana shughuli za ukeketaji ni hapa Mkoani Dodoma, Mkoa wa Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Mikoa mingi mingine ambayo kutokana na kuhama kwa makabila mbalimbali huingia katika mikoa mingine ukeketaji upo hata Morogoro, Mara, Dar es Salaam. Kwa sababu hatuwezi sasa kusema upo sehemu moja tu. Sijasikia kwa maeneo mengine kama Zanzibar, bado haujafika. *(Makofi)*

Mkoa ambao unaongoza kwa uuwaji wa vikongwe mpaka sasa tunajua kwamba ni Mkoa wa Shinyanga na maeneo mengine ya Mkoa wa Mwanza. Kuhusu adhabu zinazotolewa ni zile zile ambazo zinaonekana katika Sheria ya kujamihiana na Sheria nyingine za Jinai ambazo zinakataza vitendo vyote vya ukatili. *(Makofi)*

Na. 45

**Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA (K.n.y. MHE DEVOTHA M. LIKOKOLA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hutoa vibali kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa kufanya shughuli mbalimbali za kisekta ili kuleta maendeleo nchini:-

(a) Je, yapo mashirika ya aina hiyo mangapi yanayofanya kazi hapa nchini, orodha kwa kila mkoa?

(b) Je, ni kwa nini mashirika hayo yanachagua yenyewe eneo la kufanyia kazi badala ya Serikali kushauri maeneo yenye mahitaji na sekta zenye maslahi zaidi kwa Watanzania?

(c) Je, kwa nini Mkoa wa Ruvuma hauna mashirika mengi ya kimataifa?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* ya kimataifa kabla ya kuanzisha shughuli zao hapa nchini hutakiwa kusajiliwa kwanza. Usajili huo huwapatia fursa ya kuendesha shughuli zao kwenye Mikoa yote nchini. Aidha, dhana nzima ya utendaji kazi wao katika sekta hii imejikita zaidi katika kujitolea na kuhudumia jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devota Likokola (Viti Maalum) lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kulingana na takwimu tulizonazo *NGOs* za Kimataifa zilizoko nchini ni 107 na bado mashirika mengine yanaendelea kujisajili. Kati ya hizi *NGOs* zenye miradi Mkoa wa Ruvuma ni *Technoserve,* Dai Pesa na *Enterprise Work* pamoja na *Population Service International*

*NGOs* zote za kimataifa zinapoingia nchini husajiliwa kitaifa hivyo wanaruhusiwa kuendesha shughuli zao kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa hadi Wilaya. Idadi hii inahusisha *NGOs* zilizosajiliwa chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24 ya mwaka 2002. Sheria ya Vyama, Sura 337, Sheria ya Udhamini, Sura 375 na Sheria ya Makampuni, Sura 212 kama ilivyorekebishwa. Orodha ya *NGO's* kwa kila Mkoa nitampatia Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa orodha hiyo ni ndefu itakuwa ni vigumu kuisoma hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Takwimu ya *NGOs* zilizosajiliwa chini ya Sheria ya *NGOs* Na. 24/2002 ambayo inasimamiwa na Wizara yangu kuanzia Januari 2005 hadi Desemba 2006 zipo *NGOs* za kimataifa 72. Kati ya hizi 38 zina vyeti vya usajili *(Certificate of Registration)* na 34 Vyeti vya Ukubalifu *(Certificate of Compliance).* Mashirika yote haya yanaendesha shughuli zao nchini kote na yametandaa katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kulingana na uwezo wao wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahimiza na kuzielekeza *NGOs* za kimataifa kutandaa na kuendesha shughuli zao nchi nzima. Jitihada hizi za Serikali zitaendelea ili kuhakikisha kwamba maeneo mengine ambayo hayana miradi inayoendeshwa na *NGOs* za kimataifa ikiwemo Mkoa wa Ruvuma yanafikika. Kimsingi *NGOs* huendeshwa kwa dhana ya kujitolea. Kisheria si rahisi kuwalazimisha kutandaa nchi nzima au kuwapangia kwa nguvu maeneo ya kufanyia kazi kwa kuwa huduma zao pia hutegemea rasilimali watu na fedha.

Aidha, Mashirika haya hutegemea fedha au misaada ya wafadhili kutoka nchini mwao au makao makuu ya mashirika hayo. Uzoefu umeonyesha kuwa pia wafadhili wa *NGOs* nao hawachangii sekta zote bali hujikita kwenye maeneo machache hivyo *NGOs* nyingi hulazimika kuendesha shughuli zao kwenye baadhi ya Mikoa na Wilaya chache tu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea na utaratibu wake wa kuzishawishi na kuzielekeza *NGOs* kutandaa

nchi nzima kulingana na vipaumbele vya Serikali, ili Mkoa wa Ruvuma uweze kufaidika zaidi na miradi ya *NGOs* za kimataifa.

Na. 46

**Askari waliopigana Vita ya Kagera**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa majeshi yetu yalitujengea heshima kubwa katika vita ya Kagera, ikiwa ni pamoja na askari mgambo ambao nao walipelekwa mstari wa mbele kwa mapambano:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia askari wa mgambo ambao walisukumwa zaidi na uzalendo kwa kuwapa motisha angalau kila baada ya miaka mitatu?

(b) Kwa kuwa, kwa sasa askari hao wana umri mkubwa na wengi wao hawakuwa na ajira zenye mafao ya uzeeni. Je, Serikali haiwezi kutoa matibabu bure kwa mgambo hao na familia zao kwa kuwa hawana kipato?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 1978, nchi yetu ilivamiwa na majeshi ya Uganda. Kutokana na uvamizi huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alilazimika kutangaza vita dhidi ya majeshi ya Iddi Amin Dada, vita hivyo vililenga katika kuilinda nchi yetu na siyo vinginevyo. Baada ya Amiri Jeshi Mkuu kutangaza vita, vijana wa mgambo walikuwa ni miongoni mwa waliojitokeza kushiriki vita hivyo. Kupitia kwako, naendelea kuwashukuru wale wote walioshiriki katika vita hivyo. Baada ya vita hiyo kumalizika, askari wa mgambo walioshiriki, walipewa fursa ya kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Baadhi na kwa ridhaa yao, walikubali kujiunga na Jeshi la Wananchi na wengine waliamua kuendelea kufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, msaada mkubwa uliotolewa na Serikali, kwa askari wa mgambo ni kuwapatia fursa ya ajira katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania mara baada ya kumalizika kwa vita na kuwalipa haki zao wale walioamua kuendelea na shughuli zao badala ya kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwa sasa hakuna mpango wowote ulioandaliwa zaidi ya ule uliokwishatolewa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya askari wa mgamboi kulipwa haki zao, walirejea katika maeneo yao na kuendelea na maisha kama wananchi wengine. Utaratibu wa matibabu uliopangwa na Selrikali kwa ajili ya wananchi, ndio huo huo unaotumika hata kwa wanamgambo waliostaafu. Aidha, Serikali bado inaendelea kuwasaidia matibabu wazee wasiokuwa na uwezo ikiwa ni pamoja na wanamgambo waliostaafu ambao kwa sasa ni wengi wao ni wazee.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi, na Jeshi la Kujenga Taifa kwa majibu yake mazuri. Lakini bado naisihi Serikali itakapokuwa imejiweka sawasawa iwaangalie wanamgambo hawa na wanajeshi waliopiganya vita vya Kagera kama jinsi Serikali ya Uingereza inavyowaangalia Askari waliopigana Vita Kuu ya Pili ya Dunia lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Serikali ina mamlaka ya kuunda na kuweka Jeshi la aina yoyote katika nchi yetu kwa kifungu 147 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kifungu kidogo cha kwanza, na pia Majeshi rasmi katika nchi yetu yametajwa katika kifungu hicho hicho cha 147 kifungu kidogo cha nne. Sasa je, ni lini Serikali itafikiria Jeshi la Mgambo kulitangaza kama jeshi rasmi.

La pili, katika maeneo mengi katika nchi yetu Askari wa Jeshi la Mgambo wanatumika kufanya shughuli mbalimbali zikiwemo kuwakama waharifu na *operation* mbalimbali katika Halmshauri zetu. Je, kwa kufanya hivyo wamekuwa wamefanya makosa na wanaweza wakashitakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza majukumu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na majukumu la Jeshi la Mgambo ni tofauti.

Kwanza tukitaka kubadilisha wanamgambo kuwatangaza kama ni wanajeshi tutalazimika kubadilisha Sheria na Majukumu yao. Muda bado upo na ninadhani si busara kwa wakati huu kulingana na majukumu ya mgambo tukawapa majukumu mengine ya kitaifa.

Swali la pili, Mheshimiwa Arfi ameuliza kuhusu kukamata kwa wanamgambo watakaokuwa wanakamata watu wanaofanya makosa. Wanamgambo hawana Sheria ya kukamata. Sheria ya wanamgambo ni kuwakamata wahalifu na kuwafikisha Polisi ili wao waweze kuwachukulia Sheria kwa mujibu wa Sheria.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili niweze kuongezea kidogo kwenye swali lile la nyongeza la kwanza la Mheshimiwa Arfi, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ni kwamba Sera yetu ya Ulinzi ni Ulinzi wa Umma. Tunakuwa na Jeshi dogo lakini tunakuwa na *Reserve Forces* ikiwemo mgambo.

Kwa hiyo, ni vyema tukaelewa Sera hii kwa sababu hatuwezi kutangaza kwamba iko siku mgambo nao watakuwa Jeshi rasmi. Kwa sababu sera yetu inajikita katika kuhakikisha ulinzi unakuwa ni wa umma ambao na mgambo wanakuwa ndani yake likiwa kama ni Jeshi la Akiba.

Na. 47

**Kambi za Jeshi la Wananchi – Bububu**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jimbo la Bububu lina Kambi mbili kubwa za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambazo ni Kambi ya Mwanyanya na ile ya Bububu:-

(a) Je, ni lini eneo la Kambi ya Mwanyanya litazungushiwa uzio ili kuweka usalama zaidi kwenye Kambi hizo?

(b) Kwa kuwa, Kambi ya Mwanyanya ina gari dogo moja tu na chakavu na pia hakuna nyumba za kukaa Askari na eneo la Kambi halina hatimiliki. Je, Serikali inasema nini juu ya hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Jimbo la Bububu, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuyapima maeneo yote ya Kambi za Jeshi la Wananchi na hatimaye kuyapatia hatimiliki. Kazi hiyo imeanza na baadhi ya Kambi za Jeshi tayari zimeshapimwa na kupatiwa hatimiliki. Aidha, Serikali imeanza kuchukua hatua za kuzifanyia ukarabati pamoja na kujenga nyumba mpya za askari na maafisa katika kambi mbalimbali Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa ambalo linapunguza kasi ya juhudi hizo ni upatikanaji mdogo wa fedha. Hata hivyo, bado Wizara yangu inalipa kipaumbele suala la kukarabati zana na majengo na tuna matumaini makubwa baada ya muda, matatizo haya yatapungua kutegemeana na hali ya kukua kwa mapato ya Serikali kama yanavyoendelea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Cosmas swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mipango ya Wizara ya Ulinzi ni kuzizungushia uzio Kambi zote za Jeshi la Wananchi ikiwa ni pamoja na Kambi ya Mwanyanya hali ya fedha itakapoimarika. Kwa wakati huu, Makao Makuu ya Jeshi imeagiza eneo lote la mzunguko wa kambi ya Mwanyanya iliyoko Wilaya ya Magharibi Zanzibar, lipandwe miti. Hali hii itasaidia sana kulitambua kwa haraka eneo la kambi pamoja na kulinusuru kuvamiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa upatikanaji wa gari, Wizara imeshaanda utaratibu wa kuagiza sehemu ya magari kwa ajili ya matumizi ya Jeshi, mara baada ya kuwasili magari yaliyoagizwa suala la usafiri kwa kambi ya Mwanyanya na Kambi nyingine yataangaliwa kulingana na uzito wake.

Kwa upande wa nyumba za kuishi askari, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kutafuta mikopo nafuu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa nyumba za kuishi askari kwa nchi nzima.

Lengo letu ni kuwarejesha Wanajeshi wote makambini, ili lengo hili liweze kufikiwa ni dhahiri tutahitaji kwanza kujenga nyumba za kutosha.

Aidha, kambi ya Mwanyanya imepimwa na ina hatimiliki namba 831 na imetolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 17/3/2003.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kutokana na maelezo yake ya msingi ni kwamba Serikali ina mpango wa kujenga nyumba katika Kambi zote za Tanzania Bara na Visiwani. Ninauliza kwamba ni nyumba ngapi zitajengwa kwa upande wa Tanzania Zanzibar ikiwemo Kambi ya Mwanyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni Chombo cha Muungano. Tunapofanya tathmini huwa tunafanya kwa pande zote mbili za Muungano, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Tathmini ya mahitaji ya nyumba inaonyesha kwamba Tanzania Visiwani wanahitaji zaidi ya nyumba 1000.

Kwa hiyo, hali ya fedha itakaporuhusu, tutajenga nyumba hizo kwa Tanzania Visiwani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa Maswali umekwisha na maswali yamekwisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nifanye ufafanuzi kuhusu uamuzi wangu wa kukataa swali la Mheshimiwa Chaurembo. Swali la Msingi liliulizia Mahakama za Biharamulo. Swali la nyongeza likaulizwa habari za Kariakoo.

Ni maswali mawili tofauti kabisa! Kumbe swali alilouliza Mheshimiwa Rished, aliuliza juu ya suala la kwamba utaratibu mzima wa kuelimisha Mahakimu. Sasa,

linaelekea kama ni *Principal* ya Mahakimu, lakini si *specific* swali linalouliza eneo fulani, ndio maana nikasema hilo halikuwa swali. Lakini, unaweza kuliuliza tena na ukapata majibu. Naomba tuelewane hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, halafu tuna Mheshimiwa John Cheyo, ameuliza swali moja hapa anasema "naomba unisaidie kiutaratibu na kiitikadi ya Bunge, kwa mfano Bungeni tunao utaratibu wa kuvaa, kusimama Spika anapoingia na kadhalika.

Utaratibu wetu wa kushangilia na kupiga meza. Mtindo wa sasa wa kupiga makofi kama watoto wa shule ya msingi unanikera na unakera wengi. Hadhi ya Bunge lako inaathirika. Naomba mwongozo" *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kumwambia kwamba kwa kuwa tunaendelea na kuandaa marekebisho ya Kanuni, hili litapelekwa kwenye Kamati ya Kanuni. Tunaendelea na Utaratibu wa kukarabati Kanuni zetu, tutaenda kulijadili. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2006, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Jana tulipoahirisha shughuli za Bunge, ambaye alikuwa anaendelea kuzungumza na muda wake ulikuwa haujakwisha kwa dakika 5, ni Mheshimiwa Mrope, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Zuber Ali Maulid ajiandae na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ajiandae. Kabla ya hapo nina wageni.

Leo katika *Speaker's Gallery* tuna wageni ambao mimi nitakuwa nao mchana huu wanatoka *UNDP*, wanashughulikia Mpango unaoitwa *Deepening Democracy*. Mpango huu wa *Deepening Democracy* tumeuingiza katika *Corporate Plan* yetu ya Bunge pamoja na Mpango Maarufu wa Wanawake, *TWPG*. Kwa hiyo, tutakuwa nao mchana. Nao ni Ndugu Theo Caspus, *If you can stand up so that we can see you!* Caspus ni *First Secretary, Governance Democracy Processes* na *Civil Society* ya *European Union*. Tunaye Dimitrio Stolling, yeye yuko kwenye *Netherland Embassy*, halafu tuna Sagito Muko, linakuwa kama jina la Kiswahili, *she is from Havard University* na wengine watakuja tutakuwa na mazungumzo nao mchana. *You are welcome and we shall see you in the afternoon, thank you!*

Waheshimiwa Wabunge, halafu nina wageni wengine, hawa wanatoka Shirika la Simu Tanzania, *TTCL* na wako hapa kwa ajili ya kuwaonyesha Waheshimiwa Wabunge bidhaa zao mbali mbali.

Nadhani wameweka kule ambazo ni kama *handsets*, *Broad band* na *Internet Connectors*. Nao ni Bwana Mohamed Hussein, Meneja wa Biashara Mkoa wa Dodoma, Bi. Eva Mwabulambo, Afisa Biashara kutoka Makao Makuu Dar es salaam, tuna Bi. Agripina Polycarp, yeye ni Afisa Biashara kutoka Makao Makuu Dar es salaam, tuna Bwana Davd Kidenya, Afisa Biashara kutoka Makao Makuu Dar es salaam na tuna Bi. Zenna Mmbaga, Afisa Biashara kutoka Makao Makuu Dar es salaam. Pamoja na wageni wengine wote mnakaribishwa, Ukumbi wa Bunge ni huru kwa wananchi wote. Karibuni sana!

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizitumie vizuri dakika zangu tano zilizobaki. Jana nilisema Bajeti hii ilikuwa ngumu kidogo, lakini kama utekelezaji utakuwa makini, basi hatutakuwa na matatizo, mambo mengi tutaya-*accomplish*. Jana nilianza kuzungumzia juu ya mradi wa Mbwinji mpaka Masasi. Mradi huu kwa bahati nzuri umekuwa katika awamu mbili. Awamu ya Tatu iliahidi, walitafuta fedha, baadae zikapelekwa katika Wizara nyingine. Kwa hiyo, ikaahidiwa kwamba utatekelezwa. Awamu ya Nne, wameahidi pia kwamba mradi huu ni lazima utekelezwe. Sasa, mimi nasema kwamba jamani safari hii kama mradi huu hautatekelezwa au hautaanza, basi mjue wananchi wa Masasi tutatoa shilingi katika Wizara husika. Kwa hiyo, naomba ieleweke wazi kwamba suala hili sasa lisiwe la mchezo. Wananchi wanasubiri kwa muda mrefu kupata maji, wana shida sana sana. Hili naomba litekelezwe kwa upesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nilitaka katika upande wa Wizara ya Nishati, kuna kipande kidogo kati ya Nyangao mpaka Ndanda, umbali wa kilomita 36. Kipande hiki bado hakijaunganishwa kwa nyaya za umeme pamoja na nguzo. Sasa, mimi naomba safari hii, hebu tujitahidi sana kipande hiki kiunganishwe ili umeme wa *Mnazi Bay* uwepo Ndanda, Mwena, Chikundi, Chigugu, Chikukwe mpaka Masasi. Kutoka Masasi uende Newala – Tandahimba – Nachingwea na Rwangwa ili huku Masasi kote kuwe kuchele (kumekucha) kabisa na umeme. Safari hii hakikisheni haya yanakamilika. Hapo tutakuwa tumeondoa matatizo ya wananchi na Bajeti hii wala hawatakuwa na matatizo nayo. Ninaamini Wizara hizi mbili zimenielewa na nataka kusema na kuwahakikishia kwamba naunga mkono hoja sana sana ili mradi haya niliyoyazungumza yanatekelezwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** “Kuchele” Siyo Kiswahili wala Kiingereza! *(Kicheko)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nikushukuru, kunipa nafasi asubuhi hii na mimi nichangie katika hotuba hizi mbili, hotuba ya Mipango pamoja na hotuba ya Bajeti. Lakini, niseme tu kwamba naziunga mkono hotuba zote mbili kwa sababu yale ambayo tulikusudia kwa Serikali yetu yametekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze kwanza kwa kushukuru kwamba sheria tuliyopitisha hapa Bungeni ya *Gaming Board* imesaidia sana Serikali kuongeza mapato. Kilikisiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.1, lakini baada ya kurekebisha sheria, Serikali imepata mapato ya shilingi bilioni 2.2. Kwa hiyo, nashauri kwamba iwapo zipo

sheria zingine ambazo zina manufaa kwa taifa letu, ni vizuri zikarekebishwa. Lakini, naomba niiombe Serikali hasa Wizara ya Fedha. Kufuatana na ile Sheria ya *Income Tax, ACT No. 11* ya mwaka 2004 ambayo imesababisha kwa Ndege za Mizigo kusitishwa safari zake katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, naomba na kushauri sheria hiyo ibadilishwe kwa sababu imeleta madhara makubwa kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ndege katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza zilikuwa zikija na kubeba minofu ya samaki. Taarifa ambazo tunazo, kuanzia mwaka 2001, kwa mwaka mzima kulikuwa na ndege 517 mwaka 2001, mwaka 2002, ndege zilikuja 375, mwaka 2003, ndege zilikuja 363, mwaka 2004 ndege zilizokuja ni 480, ndege zilizokuja mwaka 2005 ni 362. Zimeenda zikipungua kwa sababu ya sheria hii. Mwaka 2006, ndege zilizokuja Mwanza kwa ajili ya kubeba minofu ya samaki ni 162. Mbaya zaidi, kwa sababu ya sheria hii, tangu Januari mpaka leo, ndege zilizokuja kubeba minofu ya samaki ni 2 tu katika Uwanja wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kufanya hivyo kwa sababu sheria hii ni yetu na sisi ndio warekebishaji wa sheria hii, tunaiomba Serikali ibadilishe kwa sababu inakosesha mapato ya Serikali. Hivi sasa minofu ya samaki inabebwa kwa magari, lakini *TRA* haipati mapato, Uwanja wa Ndege haupati mapato, Hali ya Hewa pale Mwanza haipati mapato. Kwa hiyo, naiomba Serikali ijaribu kubadilisha utaratibu huu kwa sababu sheria ni zetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie uzalishaji wa Pamba hasa ubora wa zao la Pamba lenyewe. Ukiangalia mazao mengine yana *grade*, lakini bahati mbaya kabisa zao la Pamba halina *grade* hata siku moja. Tuliambiwa kwenye Kikao cha Nyanza wakati Waziri wa Kilimo na Chakula alipokuja kufungua kikao cha Nyanza, kwamba Marobota zaidi ya milioni moja yamekataliwa kwa sababu ni machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia kuleta fedha za kigeni, lakini kwa sababu ule ubora wa Pamba haupo, hata tukizalisha marobota kiasi gani, hatuwezi kupata pesa zingine kwa sababu Pamba tunayoipeleka nje ni fifi ambayo inafaa kwa kutengenezea Mablanketi. Tunaomba kwa kuanzia mwaka huu tuwe na utaratibu mzuri, Pamba tuipange kwa *grade*. Kwa mfano *grade one* iwe ni Pamba safi kabisa ambayo tunaweza kuipeleka nje. Lakini mbali na hiyo, kama ni *grade* ili tuwahamasishe hawa wakulima wetu, kama ni *grade one*, basi na bei iwe tofauti kama wanavyofanya kwenye korosho, kwenye kahawa na kwenye pareto n.k. Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, *grade* ya Pamba yetu tutakuwa tumeifikisha mahali pazuri zaidi, hilo naomba nishauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie usimamizi wa mapato ya *TRA*: Tilipotembelea Mkoa wa Tanga, tulikuta vitu vya ajabu, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama sikosei mwaka jana aliagiza kwamba katika Bandari ya Mkoa wa Tanga, lazima kuwekwe *flow meter.*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakuna *flow meter* pale. Samahani nitatumia neno ambalo siyo zuri, lakini nasema ni ubabaishaji

uliopo. Hakuna *flow meter* pale hata ukienda leo. Niliwauliza baada ya kutembelea kile kituo kimoja, nikauliza hivi mafuta yanapokuja pale kwenye meli, ukishafungua ile *tape*, yanapokuja mpaka hapa inakuwaje? Wanasema kuna *option* mbili: kama unataka kuiba, unaweza usiweke ile kadi kwa sababu ili mafuta yaende tofauti na ile ya Dar es salaam, lazima uingize kadi. Ukiingiza kadi ndio inaanza kujihesabu. Lakini, nikauliza Je, usipoweka? Wakasema usipoweka ile kadi, haihesabu. Nikauliza Je, Usipoweka ile kadi, mafuta yanapita? Wakasema usipoweka ile kadi mafuta yanapita. Sasa, nikasema sasa huu si ndio wizi? Wakasema huu ni wizi mtakatifu wala hakuna tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lakini, mbaya zaidi wasimamizi wa ile *flow meter* ni wenyewe wale wenye kumiliki kituo cha mafuta. Sasa tunasema mtu amiliki kituo cha mafuta wakati huo huo yeye ndiye awe msimamizi, wakati huo huo yeye ndiye awe mpitisha mafuta, inatokea wapi? Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaweza kufunga , ni asilimia *zero* yaani halikutekelezwa. Kwa hiyo, huo ni wizi wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie *T-Scan*, hivi *T-Scan* wamejipangaje kwa sasa? Naomba zile *document* za sasa badala ya kutumia siku nane, ziwe zinatoka ndani ya saa 24. Lakini, *TBS* wana utaratibu wao mbovu, wanasubiri wateja wawafuate ofisini kwao tofauti na Idara zingine. Waende kule wasikae ofisini, wao siyo Mameneja. Waende kule ili kudhibiti yanayoingizwa, kwa sababu bidhaa mbovu zinaingizwa, halafu baadaye ndio wanapelekewa ofisini ndio wanataka kupima. Waende wahakikishie kule kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TICKS* huduma yao ni ya pole pole sana , ndiyo inayoleta misongamano mikubwa Bandarini, magari na vitu vingine. Tunaomba sasa ushirikiano uwepo kati ya *TRA, T-Scan, TBS* ili shughuli za uondoshaji mizigo ziwe za haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu vipaumbele: Wale watu wa Kilwa Kipatimo wana msemo wao, wanasema *"dumbensai, dumbenkate"* Maana yake ni kwamba "nianze na mkate au nianze na chai" Wanaangalia kitu cha muhimu ni nini. Hiyo ilitokea wakati mtu mmoja alikuwa hotelini wakati yuko safarini. Sasa, basi linakuja, chai iko hapa na mkate uko hapa. Sasa akasema nianze chai, nianze mkate, lakini mwenzake akamwambia anza chai kwa sababu ukianza mkate. Chai huwezi ukabeba, lakini mkate unaweza kubeba. Sasa, sisi vipaumbele vyetu ni nini hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili twende vizuri, ningeshauri kwa nchi zile ambazo zimeendelea vizuri zaidi, yapo mambo ambayo zimeanza nayo. Naishukuru Serikali imeanza na Elimu. Bila Elimu hatuwezi kuendelea hata siku moja. Lakini, tukishatoka kwenye elimu, tunaenda kwenye mambo ya Miundombinu. Miundombinu iko mingi; barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile bandari yetu, mimi naomba Waziri wa Mipango Mheshimiwa Ngasongwa na timu yake, kama amewasikiliza vizuri Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakizungumza kuhusu bandari, reli, viwanja vya ndege,

wanasema ukishafungua reli kutoka Dar es salaam ikaenda mpaka Kigoma, ikaenda Mwanza, utakuwa umefungua uchumi. Bandari yetu ile pale ikiimarishwa vizuri, tutashindana na watu wa Dubai. Ukiangalia leo Dubai kuna ndege pale *Emirates* itakuja kila siku inabeba watu wanaokuja kutoka Dubai.

Lakini, watu hao wangeweza kuishia Dar es salaam badala ya kwenda Dubai. Dubai ndogo ingekuwa Dar es salam. Bwana Mipango tafadhali. Waheshimiwa Wabunge wanaposema hapa, uyachukue mawazo yao, siyo uende uyachukue uyaweke kwenye kabati, halafu unaondoka. Hapana, myafanyie kazi. Mipango lazima ipange mipango mizuri ya kuendeleza nchi hii. Vinginevyo, kama imeshindikana hiyo mipango, Wizara ya Mipango, basi iundwe Tume ya Mipango ambayo itasimamia moja kwa moja mipango mizuri ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mawasiliano: Tuwe na *IT*, maji, umeme. Tukifanya hayo, nina uhakika nchi yetu itasonga mbele na bahati nzuri nchi yetu ina utawala mzuri kabisa kabisa. Na bahati nzuri pia nchi yetu kama alivyosema Mwalimu Nyerere kwamba ili nchi iendelee inahitaji mambo manne:- Uongozi Bora ambao tunao - safi kabisa, Siasa safi ya Chama cha Mapinduzi - safi kabisa, Rasilimali watu, tunayo, Ardhi tumepewa kubwa kubwa, ina kila kitu ardhi yetu. Tungeomba sasa kupitia *TIC* ianze kufikiria ku-*invest* kwenye ardhi. Ardhi hatujaitumia hata kidogo, tuko juu juu tu hapa. Bado nasema ardhi bado hatujaitumia. Tukitumia ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, mito, maziwa bahari, nina uhakika tutatoka hapa tulipo, tutaenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niwashukuru sana ndugu zetu wafadhili. Wametufadhili kwa hali ya juu sana. Tumeambiwa mpaka Machi walikuwa wametufadhili kiasi cha asilimia 93. Tunawapongeza sana kwa sababu yale ambayo tulikuwa tumeyakusudia yatafikia lengo mpaka kufikia Juni. Lakini, ombi kwa Mkoa wangu wa Mwanza, tumepangiwa shilingi bilioni 2.4 ambazo ni pesa za ndani. Pesa za nje ni bilioni 20. Hizi ni za nje, naomba pesa hizo kwa sababu ni za nje, zije. Vinginevyo kama pesa hizo hazitakuja, basi, Mkoa wa Mwanza utadumaa, hakutapatikana maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika hii hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango. Kwanza kabisa, napenda sana nitoe pole kwa wale wote ambao wamefikwa na maafa ya ajali. Lakini, pia napenda kuwapongeza vijana wetu tuliokuwa nao hapa jana, tumetoa pongezi. Lakini na mimi napenda kusisitiza tu kuwapa pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, pamoja na kuwapa pole, kwenye suala la ajali, napenda sana kuitaka Serikali ivitumie vyombo hivi ambavyo vinaratibu masuala ya usalama wa vyombo vinavyosafiri barabarani. Wavishauri vyombo hivi vizingatie usalama wa wananchi wengi wanaosafiri katika haya mabasi kwa kuhakikisha kwamba

basi haliwi na mlango mmoja tu ili linapotokezea tatizo, iweze kupatikana njia ya kuokoa maisha ya wale watu ambao watakuwa wamenaswa na ajali hizi zinazotokea kama hii iliyotokea hivi karibuni hapa Singida. Kwa hiyo, wahimize sana vyombo hivi vinavyosimamia usalama vihimize uwekwaji wa milango ya dharura ili kuweza kuokoa maisha ya watu zinapotokea ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, naanza kwa kusema kwamba bajeti hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini, pamoja na hayo nitapenda nitoe michango yangu michache ili iweze kusaidia Serikali katika kuhakikisha kwamba tunaboresha na hatimaye tunafikia kwenye lile suala la maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza, nitaanza na suala la mafuta ya taa. Suala hili la mafuta ya taa limesikitikiwa na wengi waliochangia. Mimi nadhani nia ya Serikali haikuwa mbaya, lakini pamoja na nia njema kwamba hailogwi, naitaka Serikali iliangalie kwa undani zaidi hili suala. Kwa sababu pamoja na mkakati mzuri ambao tulikuwa tumeanza nao wa kupiga vita uharibifu wa mazingira. Suala hili la mafuta ya taa kwa kweli inabidi Serikali kwa huruma kabisa iliangalie tena, kwa sababu ikiwa tutakuwa tuko pamoja na wale wote ambao wanapiga vita uharibifu wa mazingira, lakini, wakati huo huo lile suala la mbadala ambalo lingewawezesha wananchi wengi sana kuepuka matumizi mabaya ya kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa pamoja na matumizi ya kuni, lile ambalo wangelitumia kama mbadala suala la mafuta ya taa, leo Serikali imeweza kulifikisha kodi kwa hapo ilipoweka. Mimi naishauri sana Serikali iliangalie tena kwa huruma kwa karibu sana ili ikiwezekana ishushe kodi kwenye mafuta ya taa ili kuyanusuru mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tu tulikumbwa na ukame nchi nzima na mchango mkubwa wa hili ilikuwa ni uharibifu wa mazingira. Lakini, yamezungumzwa mengi sana pamoja na kuhimizana kupanda miti. Mti unachukua muda mwingi sana kukua mpaka uwe mkubwa. Lakini, kukata miti ni jambo ambalo linaweza likachukua kipindi kifupi tu, kwa hiyo mazingira katika sehemu fulani yakaharibika. Kwa hiyo, kwenye suala la mafuta ya taa, mimi kilio changu ni kwamba Serikali iliangalie iteremshe hii kodi. Kodi iliyoteremshwa kidogo katika hili, kwa uwingi wake wa matumizi ya mafuta, kwa kweli tutaweza kufikia lengo pale kodi inayokusudiwa kukusanywa kutokana na suala la mafuta ya taa. Isitoshe, kwa hiki kiasi kilichowekwa kupandisha kodi kwenye mafuta ya taa, kwa kweli kuna watu wachache sana ambao watanufaika na hili na watu hawa ni wale ambao wanapitisha mafuta ya ndege *(Jet A1)* kwenda katika nchi za jirani ambazo hazina Bahari. Mafuta yale yanayopita *Transit*, mafuta ya Ndege aina ya *Jet A1* ni mafuta yale yale ya taa. Kwa hiyo, wachache hao wajanja watayapitisha kama yako *Transit*, lakini yataishia humu ndani nchini katika Mikoa ya katikati huku. Watayauza kwa bei ya mafuta ya taa ambayo ina kodi. Kwa hiyo, tutajikuta tumewapa na kuwatajirisha watu wachache kwa kunufaika na ile tofauti iliypo ta kodi baina ya mafuta ya taa na *Jet A1* ambayo haina kodi kabisa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naitaka Serikali wawe waangalifu sana sana kwa sababu wanaofaidika hapa ni wachache sana. Kwa kushusha kodi ya mafuta ya taa,

tutawanufaisha wananchi walio wengi ambao ndio watumiaji wa haya mafuta ya taa. Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dizeli na mafuta ya petroli, wala mimi sina maneno makubwa sana pmoja na kwamba mafuta kwa ujumla wake, ukisumbua kidogo bei ya mafuta ya taa, umesumbua uchumi mzima wa nchi. Hili halina pingamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nitapenda nilichangie ni suala la fedha za maendeleo ambazo zinatolewa na wahisani. Kwanza kabisa, mimi nitapenda niwapongeze sana wahisani ambao wanatusaidia katika maendeleo katika hii nchi. Lakini, napenda sana kuipa tahadhari Serikali, tusikimbilie kupata ahadi ambazo baadaye zinakuwa hazitimizwi, kwa sababu tunakwenda tunakutana na wahisani, wanaahidi kuchangia wanachoahidi kwenye bajeti. Kwa kweli takwimu zinazoonekana ni nzuri sana tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na mara nyingi sana huwa tunaangalia zile *vote* baada ya matumizi kufanyika. Lakini, ukweli ni kwamba kuna baadhi ya wahisani wanatoa ahadi ili tuweze kuziweka zile *figure* katika bajeti yetu. Hatimaye Waziri anaposoma hapo, aweze kutoa sifa kwa mataifa yale, lakini wao ule uungwana wa kutimiza ahadi yao, unakuwa haupo. Ukweli tunakuja kuuona wakati tunaangalia vitabu vya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vitabu vile vinaonyesha kwamba kuna baadhi ya wahisani, wanatoa ahadi, lakini baadaye wanarudi wanasema kwamba labda tofauti ya kipindi chetu cha Bajeti, wao pengine kinaanzia Machi au wengine kinaenda sawa sawa na mwaka wa kalenda. Sasa, masuala haya tuyaangalie kwa karibu na tuwe na uhakika tuwafanye wahisani watuhakikishie kwamba hizi fedha tutazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ndizo tuziingize kwenye bajeti na ziweze kusomwa hapa na hatimaye kwenda kusimamia upatikanaji wake na hatimaye kuweza kusaidia maendeleo katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nitapenda nichangie ni suala la miundombinu, suala la uboreshaji wa miundombinu yetu ya ndani hili lina umuhimu wa pekee, kwa kweli linarahisisha vitu vingi sana. Hata hizi bei za mafuta zinazopanda kwenye miundombinu ambayo dhaifu bado mtu yule yule wa mwisho, mwananchi wa chini ndiye ataendelea kuumia. Lakini ikiwa tutaboresha miundombinu yetu hasa barabara kuhakikisha kwamba nchi tunaiunganisha na barabara zilizo bora na safi kwa pande zote hili suala litasaidia sana kurahisisha pamoja na kutoa msukumo mzuri sana kwa uchumi wa nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *TRA,*. Bajeti iliyopita tulizungumza kwa ukali kidogo kuhusu suala la magari ambayo yana usajili wa Zanzibar tukazungumza kwa ukali na tulizungumza wengi sana. Utumikaji wake hapa Tanzania Bara ni Jamhuri ya Muungano, tumepata jibu zuri sana lenye matumaini kutoka kwa Waziri na wengine wote ambao wamekuwa wakijibu masuala mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ambazo tumekuwa tukizipata tuna wasiwasi hazitekelezwi wala sijui tatizo liko wapi. Tuliahidiwa kwamba tutaokolewa na *ascuda plus plus, ascuda plus plus* ni programu tu. Mimi tatizo nadhani siyo hii *soft* ya *ascuda,* tatizo liko kwa wale watendaji kwa sababu *software* inafanyakazi sasa hivi kule Zanzibar lakini tatizo liko pale pale kama ambavyo tulivyozungumza kipindi kilichopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, suala hili aliangalie kwa karibu sana kwa sababu bado usumbufu uko pale pale. Kwa nini baadhi ya watu katika nchi ile ile wapate matatizo kwa sababu magari ambayo yana usajili huku ukilichukua ukaenda nalo Zanzibar tatizo halipo, wanajua ni gari ambalo lina usajili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mahali pake pa halali na yanatumika. Kwa hiyo, hili liangalie kwa ukaribu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine ambalo ni suala la gawio la 4.5% la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili pia tumekuwa tunapata ahadi tu, mara tumo mbioni, tumo kwenye mchakato, tuko kwenye hili, haya masuala yataisha lini jamani? Uchumi wa Zanzibar ni muhimu sana ukasaidiwa , kwa hiyo, kwa hili tunaomba pia tuambiwe basi tupewe *deadline,* hili suala litakuwa limekamilika ifikapo wakati fulani ili tuweze kujua sasa tunaondokana na hii 4.5% na tunakwenda mbele zaidi ili kuweza kuboresha uchumi wa sehemu ya pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni Zanzibar. (*Makofi*)

Vilevile napenda kuzungumzia suala la *CDF*. Hapa napenda kutoa tahadhari, najua hili suala la *CDF* Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuja kulizungumzia kwa urefu zaidi katika hotuba yake. Lakini napenda kutoa tahadhari kwa sababu kwa upande wa Zanzibar sisi Wabunge ni tofauti kidogo na huku upande wa Jamhuri ya Muungano ambapo Wabunge pia ni Madiwani, sisi si Madiwani. Kwa hiyo, Manispaa za Zanzibar hazisimamii shughuli ambazo haziratibu masuala yetu sisi Wabunge.

Tunayo Ofisi ya Bunge kule, kwa hiyo, tungemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na mipango mizuri ambayo anayo, suala hili aliangalie kwa ukaribu sana ili kuhakikisha kwamba ile *CDF* tunaweza kuisimamia wenyewe Wabunge na kuona kwamba inafanya kazi vizuri katika upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kwamtipura, napenda kurudia kwamba naunga mkono bajeti hii asilimia 100. Lakini nasisitiza sana Mheshimiwa Waziri, niangalie kwa karibu sana suala hili la *TRA* na usajili wa magari, suala la gawio la 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, liangaliwe kwa karibu na tuambiwe basi ni lini ambako hiyo kazi ambayo imeshafanyika tupewe jawabu angalau tuzungumziwe tuambiwe kwamba hatua iliyofikiwa ni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, napenda kuishia hapo na naunga mkono bajeti asilimia 100. (*Makofi*)

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nizungumzie kidogo hoja mbili zilizoko mbele yetu. Nakushukuru, naomba nianze na kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Busanda, kwanza, kwa kunichagua na pili kwa kunivumilia. Wamevumilia upweke kwa muda miezi mitatu ambao sikufika jimboni kwa kuwa nilikuwa naumwa. Tulikuwa tunawasiliana kwa njia ya simu , napenda niwajulishe kwamba sasa niko sawasawa nimesharudi kazini na niko tayari kuwatumikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Ofisi ya Bunge, wamekuwa wakinisaidia na walinijali, waliweza kuja hospitalini, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Napenda nishukuru familia ya Mheshimiwa Rais, walikuja kuniona wakati nimelazwa Muhimbili, walinipa moyo na nikajisikia naanza kupona kadri walivyokuwa wanakuja kuniona, nawashukuru sana. Nawashukuru Wabunge wenzangu, waliniombea na wengi walikuja kuniona waliopata nafasi, nawashukuru sana walinipa moyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijielekeze kwa Serikali kwanza katika bajeti yake kwa kweli napenda kuishukuru, imefanya kazi kubwa sana. Katika bajeti napenda nianze na hili la *CDF* ambalo mwenzangu amelizungumza . Napenda nianze kwa kupongeza kuwepo kwa mfuko huo na kwamba utawapa Wabunge nguvu ya kufanya kazi. Tulianza kwa maneno, tukagombana na waandishi wa habari, sasa limekuwa letu sote tutalipeleka tuwafikishie wananchi nadhani watalipokea vizuri sana. Ni jambo zuri, ni jambo la busara nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nasoma bajeti vile vile nikasoma mawazo ya wenzetu wa upinzani, walitoa mawazo mazuri, nikasoma nikaona kwa kweli kulikuwa na vitu vingine niliviona vya msingi nikasoma. Lakini baadaye nilipokuwa naona utekelezaji ikanikumbusha nilipokuwa nasoma shule; nilipokuwa nasoma shule nilikuwa napanga bajeti. Napanga, nikianza kazi nitanunua makochi kwanza, halafu mwezi unaofuata lazima ninunue pikipiki, mwezi mwingine nitajitahidi nikusanye ninunue gari nzuri halafu mwaka unaofuata najenga nyumba. Na nilikuwa sipangi kukopa, nilikuwa nawaza hivyo. Sasa nilivyoanza kazi vitu haviendi, mwaka wa pili, wa tatu, haviendi. Nikienda likizo natamani kuuza rasilimali za nyumbani ili niweze kurudi ndiyo nikawaza jana hata walivyosema tuuze ndege nikasema ndiyo yale yale ya kwangu ya kuuza rasilimali za nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaambia wananchi kwamba ukiwa pembeni unaangalia mpira unaweza ma ukasema wenzako hawajui kucheza, unakuwa unarusha mguu unasema mimi ningefunga goli kumbe huwezi. Kwa hiyo, ndugu zangu wananchi kule ni kweli mtu akiwa anazungumza pembeni anafikiri hivi vitu ni rahisi kuvitekeleza, ni kazi ngumu sana ukiingia ndani. Kwanza, jiangalie hata kwenye familia yako au jiangalie ndani unawezaje kuyafanya haya. Mimi napenda niipongeze Serikali inafanya kazi nzuri sana, inajitahidi. Tunaangalia mabaya tu lakini shule zimejengwa sasa hivi. Mimi kwangu kila kata ina shule ila sasa tatizo tu huwezi kupata kila kitu mara moja kwa kweli kazi, na tunakwenda, hata Bunge hili linakwenda mimi nilitarajia nilivyoona bajeti ilivyokwenda wanavyosukuma nafikiri hata Bunge tutasimama lakini tunakwenda na

*CDF* tumepewa kwa kweli mambo yanakwenda. Nadhani wanajitahidi matatizo lazima yatakuwepo. (*Makofi*)

Bajeti kwa kweli imesomwa siyo kazi rahisi kwa sababu inakwenda, hakuna nchi ambayo inayoendeshwa bila bajeti. Kuna kukusanya lazima jasho litoke, kuna matatizo lazima yatokee. Yapo mambo mengi ambayo yanaumiza wananchi na mafuta nafikiri Serikali imeliona kuna watu viongozi watatumia hekima zao juu ya hilo.

Mimi shida yangu kubwa naomba viongozi wetu watusikilize hiki kinachokusanywa , hii fedha ya wafadhili, hii fedha ya wananchi, nilimsikiliza Waziri Mkuu anasema ni kasungura, tukapata haka kasungura kanapotolewa tukianza kugawana kanakwenda wapi na kanamfikia nani na hilo ndilo swali nitakaloulizwa na wananchi wangu nitakaporudi nyumbani. Kwa sababu wananchi wangu wamenituma hapa, sasa hivi wanajua tumekwenda kuwinda kila mmoja atarudi na mnofu.

Sasa mimi nitarudi na nini kwa sababu wananchi wangu watapenda kuona umeme unatoka Bukoli unakwenda Nyalugusu, unakwenda Lwamgasa, unakwenda Katolo unakwenda Bukombe wanaona mradi wa Nyakagomba wa maji unakwenda na wana Nyakagomba wanapata maji. Watapenda kuona shule zao na zenyewe zinapata kompyuta watapenda kuona wanapozama majini wanaokolewa. Je, kwenye bajeti tumeweka *rescue boat* ngapi? Juzi Mheshimiwa Diallo na wenzake wengi walizama tena na viongozi wa nguvu sana. Lakini Mikoa yote inayozunguka Mara, Mwanza, Kagera, na Wilaya zake hakuna *Rescue boat* hata moja. Gharama ya *rescue boat* ni shilingi ngapi, kama tutaweza kununua shangingi nafikiri haizidi shilingi milioni 80 je, VX inanunua shilingi ngapi? Tuangalie vipaumbele vyetu sasa. (*Makofi*)

Nashukuru Serikali imeangalia suala la elimu na miundombinu. Tuangalie je, hizi zinakwenda kwenye miundombinu na zinakwenda sehemu gani. Mimi napenda nizungumze kwa masikitiko kidogo, hapa nikandamize kidogo kuna tatizo. Mwakajana nililalamika kuhusu barabara ya Usagala kwenda Geita ilikuwa patupu, tukalalamika, nikaangalia kwamba siendi na chochote katika kale kasungura nikaona wengine wanachukua figo, maini na moyo, mimi hata ile kwato hakuna manyoya, nikaona hapa siyo sawa. Lakini viongozi walituita pembeni kwa heshima na busara wakatumbia tunawawekea bilioni tatu tukaambizana na wenzangu akina Mheshimiwa Mabina akina Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Chitalilo na wengine wa Kagera tukasema angalau sasa tunabeba.

Lakini hakuna kitu mpaka leo. Sasa napenda kuelezwa hiyo bilioni yangu tatu mbona haikufanya kazi na nikaenda kudanganya wananchi. Sasa hivi wananiuliza itakuwa namna gani? Mwaka huu nimeangalia tena halafu nikasoma vibaya wakasema bilioni 20 nikasema sasa sisemi Bungeni mimi nakaa kimya. Sasa nimefuatilia nikakuta bilioni 20 kuanzia Chamiolo kuja mpaka Usagala. Nikafuatilia tena bilioni 20 imegawanyika kutoka Chamunyolwa kwenda Bizalayombo ni billioni 8, kutoka Bizalayombo kuja Geita ni bilioni 8, bilioni 16 zimebaki bilioni 4 maana yake bilioni 4 ndiyo tena imepanga pale ina maana imezidi bilioni moja. Ile kazi ya mwaka haijafanyika maana yake iliyotakiwa mwaka jana ndiyo ingefanyika sasa hivi.

Sasa hivi hesabu hata kama sijui hesabu kweli jamani ndiyo mnanidanganya hivyo kweli jamani namna hii jamani! Jamani, jamani! Mambo namna hii kweli jamani! Hivi tutaeleza nini jamani kama hamtaki mimi wapendeni basi watu wangu, kama hamuwataki watu wangu muhurumieni Kikwete aliyekuweko huko juzi aliyesema inatengenezwa. Kama hamumuoni Kikwete muhurumieni Rais Mkapa aliyesema inatengenezwa, kama hamumuoni Kikwete muhurumieni Rais Mkapa aliyesimama katikati ya watu akasema inatengenezwa. Kama Mkapa siyo tatizo basi yahurumieni yale mazao yanayotakiwa kutoka Geita, dhahabu, pamba, ng'ombe, maharage, mchele unaolimwa Geita kwenda sehemu zingine jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 222 naona kuna jengo linajengwa, naomba zile bilioni 4 zihamishiwe pale. Mimi sina matatizo kabisa naomba zihamishiwe pale tuelewane hapo kitu kieleweke. Mimi sina matatizo, naomba zieleweke kwa sababu nashindwa mtaniuguza nimetoka hospitali mnataka nirudi tena hospitali kwa sababu nitakwenda kuwaeleza nini wale watu? Nisaidieni Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sana kwa hekima kabisa nisaidieni nisirudi tena kulazwa. Mnafanyakazi nzuri lakini katika hili ninaomba tusaidiane. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda niwaambie watu wa *TRA* jitahidini kufanya kazi na watu wa Bandarini, fanyeni kazi. Lakini hili suala la *fast track,* hivi kuna nini mpaka mnaweza *fast track,* kwa nini msiifanye bila kupendelea mtu ikawa *fast track* mkafanya usiku na mchana kwa nini kuongeza watumishi vitu vikatoka kagua vikatoka? Tatizo la pale wanalala saa 11.00 bandarini, eti tumemaliza kazi, *TRA* huku wanasema wamemaliza kazi, mimi nimekwenda mara nyingi sana pale kuchukua gari ni tabu, unazungusha watu, halafu watu utitiri wale mawakala wanaokwenda kuchukua ni wengi kweli. Ukienda tu kwenye jengo la *TRA* pale kuna dalili za rushwa tu pale. Bandarini pale ukienda usitaje kwamba wewe ni Mbunge, ukitaja ni Mbunge wanakuondoa haraka ili usiwaharibie mambo kuchungulia chungulia. Lakini kuna tabu pale. Nakumbuka tuliwahi kwenda Mheshimiwa Kijazi pale wanachozungumza wanazungumza mambo mazuri lakini kuna tatizo pale. Wafanye haraka vitu viondoke. Ile bandari inaweza kutuingiza fedha kuliko bandari zote kwa sababu sasa watu wanakwenda bandari ya Mombasa, kuna tafouti gani na yetu? *Fast track* mimi sikubaliani nayo hii itatoa mwanya kwa wachache kupeleka vitu na kupitisha vitu vyao na watu wengine kufanya mambo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niipongeze Serikali hakuna bahati itakayokuja tena, katika hili la michezo mmefanya vizuri sana tunafanya vizuri nawapongeza sana kwa upande wa michezo. Nimekuwa nikisema rudisheni michezo kwa ajili ya shule tungeshashinda tangu zamani. Sasa watu wanaondoa michezo mashuleni. Mimi nampongeza mama Sitta ameamua kurudisha michezo na amepeleka Serikalini. Safi vijana wetu wacheze hata juzi mlikuwa mnaona maandamano pale baada ya kwisha michezo watoto wote wakaondoka tukabaki sisi watu wazima. Michezo ndiyo inafanya mtoto asome, ndiyo inafanya watu waajiriwe. Kwa hiyo, michezo ni kitu kizuri na Rais wetu nafikiri tumpongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nasema suala la barabara ya Usagala tafadhali ili kieleweke naomba wakati kumalizia hii hotuba ya bajeti au wakati ku-*wind-up* tuelezewe hatima yake ni ipi kwanza kuna bilioni 3 ambazo tulitarajia kwamba sasa hivi hivi bilioni 4 angalau kuwe na mwendelezo. Lakini hakuna kilichofanyika. Njia ile ni hatari kwa sababu ukienda njia ya usagala ile feri yenyewe inakwenda inakotaka. Nahodha afanyeje inaweza ikaamua kwenda Misungwi.

Siku hiyo ikilala vizuri inaweza kwenda kwa Musalika. Ikilala vizuri inaweza ikaenda Ukerewe au ikawahurumia ikawavusha. *Rescue boat* ni muhimu katika Ziwa Victoria. Feri ya Lugezi hivyo hivyo. Sasa hivi ziwa Victoria nafikiri imesimamishwa. Kwa sababu ukienda kule chini inatoboka sasa fikiria hakuna usafiri na ndugu zangu wa Kagera ile barabara ya Usagala sijui watu wenu watapita wapi kwa sababu ni barabara hiyo moja tu inayounganisha Rwanda, Burundi, mpaka Kongo.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Rwilomba, tunakushukuru sana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi nashukuru sana naomba waendelee.

**MHE. KIDAWA H. SALEHE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nami kutoa mchango wangu mdogo katika hoja hii iliyoko mbele yetu ya Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kutoa pongezi kwa Wizara kwa bajeti ambayo iko mbele yetu na tunaijadili hivi sasa. Bajeti ambayo imetafsiri zile ahadi zilizokuwepo ndani ya Ilani ya Uchaguzi, kupitia bajeti yake ya Serikali, kwa sababu ni moja kati ya jukumu lake Serikali ya Chama Tawala kutafsiri yale ambayo yamo kwenye Ilani ya Uchaguzi wa Chama Tawala ambacho ni CCM kupitia bajeti ya Serikali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Watanzania waelewe kwamba utayarishaji wa bajeti katika hii hali ngumu tuliyonayo ni kitu kizito kabisa. Kwa sababu tumeelezwa kwenye bajeti hapa kuwa mahitaji yote yaliyopelekwa Wizara ya Fedha ni trilioni 12, mahitaji ambayo yametoka kwenye taasisi mbali mbali za Serikali, Wizara, Mikoa, Halmashauri ni trilioni 12.

Kwa hiyo, tuelewe ugumu waliokuwa nao Wizara katika kutengeneza bajeti hii. Kwani walipoangalia vianzio vyake vyote vya mapato vya ndani na nje wamefikia au wamegota kwenye trilioni 6 tu. Kijasho kimewatoka Wizara ya Fedha.

Nasema hayo kutokana na uzoefu ambao ninao mwenyewe, mimi nimewahi kufanyakazi Wizara ya Fedha, katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Idara ya Mapato ugumu huu tulikuwa tunapambana nao. Yanakuja mahitaji makubwa lakini uwezo wa kimapato ku-*finance* mahitaji yale unakuwa ni mdogo mno. Kwa hiyo kuweza Wizara kutengeneza bajeti waliyoileta hapa wamefanyakazi kubwa na nzuri inabidi tuwapongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mahitaji ni makubwa ndiyo Wizara ikatafuta kila mbinu, kila rai angalau inyanyue mapato ya kuweza ku-*finance* ili angalau asilimia 50 ya mahitaji na ndiyo ikaenda katika vianzio mbalimbal, vikiwemo vile vianzio vya mafuta na vinginevyo ambavyo vimeainishwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, *principles* za kodi zinatuongoza katika maeneo yepi tunaweza tukapata mapato mengi. Lakini vilevile lazima tahadhari ichukuliwe. Kwa mfano, *principle* ya kwanza inasema tunaweza tukaweka kodi nzito au *taxi heavy communalities* ambazo ziko *complimentary to leisure* ambazo zile *commodities* zinazoendana na mambo ya anasa, tunaweza tukaweka kodi kubwa pale, mapato yanaweza yakapatikana kwa sababu yule ambaye amezoea mambo yale ya anasa anaweza tu kupendelea kuyaendeleza, kuyatimiza yale ambayo yanamfurahisha yeye mwenyewe. Kwa mfano, kuna kodi zimeongezwa hapa katika vileo, bia, sigara wamelalamika kuwa bia itapanda bei ndiyo itapanda bei lakini kwa mnywaji hasa ataendelea kunywa bia na kodi itapatikana.

Lakini vilevile tunatakiwa tuwe na tahadhari, tuangalie viwango visipande kwa kiasi kikubwa sana kiasi ambacho kitaathiri matumizi ya familia (*expenditure pay turn)* , kwenye *family* isibadilike sana kwa sababu kuna wengine wanaweza kama kipato hakikubadilika kimebakia pale pale na huku kodi zimeongezwa bei itakuwa imeongezeka. Kwa hiyo, anaweza akabadilisha matumizi yake akapunguza matumizi ya mboga na chakula katika familia kwa kuweza kutimiza mahitaji yake ya kunywa kile kileo. Lakini mapato yanapatikana, ndiyo maana tunatakiwa Serikali tujaribu kuangalia yote haya.

Lakini *principle* ya pili vilevile inasema tunaweza tukaongeza kodi katika bidhaa ambazo hazina *substitute,* ukitakia usitake ni lazima utumie bidhaa ile. Kwa mfano, bidhaa ya mafut, Serikali imeongeza kodi katika bidhaa ya mafuta. Lakini mapato yatapatikana. Lakini sasa tuangalie namna gani haya maumivu yanayopatikana kwa kulipa kodi yanaweza yakapungua, yanaweza yakapungua tu kwa kutumia kodi ile kuwekeza kwenye sekta ambazo zinaweza zikamletea manufaa yule mwananchi ambaye aliumia katika kulipa kodi yaka-*balance*. Ndiyo maana hapa bajeti ya Serikali imetuelekeza kuwa fedha zitakazopatikana kwenye mafuta zitapelekwa kwenye ujenzi wa barabara. Sekta ambayo kwa kweli fedha hizi zikisimamiwa vizuri, zikipelekwa kwenye barabara wananchi watapata manufaa makubwa kwanza, mikoa itafunguka kwa wale wakulima ambao walikuwa wanalima kwa kulisha matumbo yao tu, sasa watalima mazao ya ziada ya kuwawezesha kupata soko kwa sababu mikoa imefunguliwa na baadae watapata kipato, watafidia yale maumivu ya ongezeko la kodi.

Lakini hapa tuangalie kuwa kweli usimamizi wa kodi hii unawekwa vizuri. Fedha zinapelekwa katika eneo lile. Matumizi ya holela yanapunguzwa. Serikali inadhibiti matumizi yake kwa asilimia kubwa na matumizi ya lazima ni lazima tuyapunguze ili kweli manufaa ya wananchi wetu yaonekane na wao wenyewe wasahau yale maumivu ya kuongeza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kodi ya mafuta ya taa, naungana na baadhi ya wenzangu kwamba kodi ya mafuta ya taa itawaumiza zaidi watu wanyonge, wananchi wa vijijini wanaotumia koroboi kupata hata mwanga katika nyumba zao. Kwa hiyo, nashauri kuwa hizi shilingi 4 iliyoongezwa hapa katika mafuta itafutiwe sehemu nyingine kama zile za anasa kwa mfano *lottery clubs* zipelekwe pale. Au vilevile tukubali sisi wafanyakazi tunaopata kiwango cha juu cha mshahara basi hizi shilingi 4 zigawiwe katika zile *taxi band* zile za juu, kile cha chini tubakishe pale pale ile *pay as you earn,* tuache ile kodi ile ile ndogo iliyopunguza angalau itasaidia na hawa wa kima cha chini kupata *disposable income* iliyonyanyuka ya kuweza kuongeza matumizi yao na wao wakawa *better off*. Lakini *bands* za juu tunaweza tukazigawanya sehemu tukazipeleka kwenye *lottery club activities* lakini tukagawanya na kwenye *income tax* ili tukaweza kuondoa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda unanikimbia , sasa nije kwenye masuala yanayogusa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Naipongeza Serikali kwa kuweka ushuru wa bidhaa zile za *excise duty* ambazo zinazalishwa bara na kutumika Zanzibar. Tunapongeza kwa hili lakini tunaomba liwekwe kwenye *finance bill* ionekane kisheria. Vilevile tunaomba kwenye sheria kwa sababu kodi hizi kwa kule Zanzibar zinasimamiwa na Bodi ya Mapato, itambulike katika sheria kama ni *agent* ya ukusanyaji wa hii kodi.

Lakini si hilo tu kuna kodi ya *cooperation tax* kwa zile taasisi ambazo zina sura za kitaifa lakini matawi yake yako kule Zanzibar kama *air Tanzania*, au Posta na nyinginezo. Mapato yanayotokana na taasisi hizi kwa kule Zanzibar nayo yawekwe kwenye utaratibu huu huu kwa sababu yanakuwa yanazalishwa kutoka kule Zanzibar nayo Serikali ya Mapinduzi irudishiwe hizi na watumie kule. Lakini lingine ni *pay as you earn,* kwa taasisi hizi hizi za muungano wanatumia *service* za kule, wafanyakazi wako kule lakini *pay as you earn* inaletwa kwenye kasha la Muungano, naomba nazo zirudishwe kule waweze kutumia kwa vile huduma wanazipata kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili linalohusiana na mikopo kutoka *World Bank.* Unajua misaada siyo jambo la muungano kwa hiyo, SMZ ilikuwa na uwezo wa kwenda yenyewe kama SMZ kuomba misaada. Lakini sasa hivi mambo yamebadilika *World Bank* baada ya misaada sasa wanaleta mikopo na kwa vile mikopo ni jambo la Muungano SMZ haiwezi kwenda moja kwa moja mpaka ipitie Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, tunaomba sasa utaratibu uandaliwe vizuri ili SMZ iweze kupata hii mikopo ya *World Bank* ambayo sasa hivi wameamua kuileta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala linalohusiana ahadi ya Mheshimiwa Rais. Alipokuwa akilihutubia Bunge hili wakati analifungua mwezi wa Desemba alisema, nanukuu: “nitaangalia upya mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bila ya kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo si ya Muungano”. Sasa hapo namwomba tu Mheshimiwa Waziri yeyote yule kati ya hawa wawili wa Wizara mama waje watuelezee ahadi hii ya Mheshimiwa inatekelezwa vipi kivitendo na Wizara hizi mbili? (*Makofi*)

Mwisho ambalo mwenzangu hapa ameligusia ni lile linalohusiana na Tume ya pamoja ya Fedha. Tusiwaache wananchi wakajiuliza na wakaweza kujipatia majibu wao wenyewe. Tukifanya hivyo wanaweza wakajipatia majibu ambayo si sahihi. Kimya kimekuwa kirefu, tumeambiwa hapa ripoti ya Tume imekwishatayarishwa, imekwishapeleka huko Serikalini lakini sasa ni muda mrefu umepita bila kupata jibu, watu wanajiuliza na wanatafuta majibu wao wenyewe. Tusiruhusu hilo, tutoe majibu tuone haya yaliyopendekezwa maamuzi yake yakoje, tutoe majibu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. Sana. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti. Lakini kabla sijaanza kuchangia bajeti ya mwaka ujao nigusie kidogo bajeti ambayo inakwisha mwisho wa mwezi huu. Jana wakati Naibu Waziri wa Maji anajibu swali Na. 32 lililoulizwa na Mheshimiwa Nkumba alisema kwamba fedha za *Quick Wings* zimeingia na ziko Hazina, 19,000,000,100. Sasa hizi fedha mwaka unakaribia kwisha. Katika fedha hizi Wilaya ya Iramba inayo milioni 123,000,100 kwa ajili ya maji na Iramba Mashariki vijiji vya Dominiki, Matongo na Mkalama vinahusika na hizi fedha. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha tunakuomba hizi fedha ziende haraka Halmashauri, zisibaki pale Hazina mkasema mwaka umekwisha, mwaka bado haujaisha, waagize watu wako wapeleke hizi fedha haraka ili zikafanye kazi zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nimepitia Hotuba ya Bajeti mbadala, kuna mambo mawili ambayo nataka niyazungumzie. Kwanza, wenzetu hawana ruhusa ya kutengeneza bajeti mbadala. Inayotengeneza bajeti ni Serikali iliyoko madarakani. Wamezungumzia juu ya barabara ya Lalago kupitia Iramba Mashariki kwenda Makuyuni. Serikali ilishapima hiyo barabara na ikatuambia humu ndani kwamba sasa hivi uwezo wa kujenga hiyo barabara haina. Inachoweza kufanya hivi sasa ni kutengeneza daraja la Mto Sibiti na kilomita 40 ili ile barabara iweze kupitika na upande wa Kisesa na Bariadi ni kujenga daraja la Mto Simiu linalounganisha Longolaniga na Gambasigu. Kwa hiyo, Serikali iko makini juu ya haya mambo, tusiingilie tuipe muda itekeleze mambo yake. *(Makofi)*

Lingine ambalo ningependa nizungumzie, ni bajeti juu ya vipato vya maliasili, uvuvi, wanyamapori na utalii. Serikali ilishaandaa mambo yake kuhusu mambo ya wanyamapori, bei za wanyamapori, bei za vitalu, utalii, uvuvi. Kwa hiyo, tusiipeleke kasi. Linalongoja Serkali ni kutangaza tu hapa. Kwa hiyo, wenzangu wa Upinzani subirini mambo yatakuja, yatakuwa mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye bajeti ya mwaka huu. Kwanza, wastani wa pato la Mtanzania mpaka sasa ni shilingi laki tatu na sitini elfu. Mikoa ninayoitaja hapa maana yake bado ni maskini. Wa kwanza, Mkoa wa Singida, pato lake ni 208,240. Lindi, 210,360. Dodoma, 219,882, Shinyanga, mia mbili arobaini na tatu laki tatu na elfu hamsini. Tabora, 296,992. Hii ndiyo mikoa ambayo haijafikia wastani wa pato la Taifa. Sasa naiuliza Serikali kwenye bajeti ya mwaka unaokuja imefanya nini kuisaidia hii mikoa. *(Makofi)*

Je, itaongeza ruzuku kuliko hiyo mikoa iliyoendelea au tutaendelea kubakia maskini tunaotoka kwenye mikoa hii? Hii mikoa siyo maskini kama Serikali ingekuwa makini jinsi ya kuisaidia. Mikoa ya Dodoma, Singida inalima alizeti. Lakini Serikali haisaidii kupandisha bei ya alizeti. Na bado inatoa msamaha kwa mafuta yanayotoka nje. Hiyo ni njia mojawapo ya kuikandamiza hii mikoa. Hata ukienda Shinyanga wanalima pamba, ukienda Tabora wanalima tumbaku, ni mazao ambayo hayapati ruzuku Serikalini. Sasa tunataka Serikali ituambie itaisaidia vipi ili mikoa hii nayo iweze kuendelea.

Mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara Mkoa wa Singida, alisema kwamba kuna kampuni imepatikana ambayo itanunua alizeti kilo moja kwa shilingi elfu moja. Wastani wa mapato ya alizeti kwa mwananchi wa Iramba Mashariki ni gunia 10. Sasa kwa bei iliyoko sasa moja kwa moja tutakuwa tumeondokana na umaskini na Wilaya zote za Mkoa wa Singida zitakuwa zimeondokana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuambie sasa hivi watu hawajauza alizeti wameweka ndani. Kwa hiyo, tunaiomba hiyo kampuni iwahi ili ije itukomboe. Lingine linalotupa umaskini Mkoa wa Singida, Mkoa wa Singida toka tupate uhuru mwaka 1960, bado haujagawanywa hata mwaka mmoja. Bado tunaendelea na shida zetu, mikoa mingine imegawanywa zaidi ya hata mara tano. Kwa mfano, Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Kilimanjaro, na hata huu mkoa ambao tulikuwa pamoja Dodoma umeshagawanywa. Ni lini Singida itapata Wilaya mpya?

Nikichukua mfano, Wilaya ya Iramba, Jimbo la Iramba Mashariki, watu wake hawawezi kufika Wilayani wanatibiwa Wilaya jirani, tena hospitali ya kulipia ya Haidom. Kwa hiyo, hawafurahii matunda ya *Basket Fund.* Sasa kama hatuwezi kufika Makao Makuu ya Wilaya kweli tutaendelea? Watumishi walioko katika Jimbo la Iramba Mashariki hawafuati pensheni Wilayani kwa sababu pensheni wanayofuata ni ndogo kuliko gharama wanayotumia. Ukitaka kwenda Kyomboi, mwananchi wa Iramba Mashariki ni lazima aende Singida alale, kesho yake ndiyo aende Kyomboi. Akimaliza shida arudi alale Singida ndiyo arudi Jimboni kwake.

Watumishi wa Serikali, Walimu, kila siku, kila mwezi, wanapoteza wastani wa siku tano kwa kufuata mshahara. Kwa sababu ni lazima afuate hizi *process.* Sasa kweli tutaendelea kwa vigezo hivi? Mimi naiomba Serikali ituambie imetenga pesa kiasi gani kwa ajili ya kugawanya Wilaya tukianzia Mkoa wa Singida. Mkoa wa Singida mwaka huu katika uchaguzi wa kuchagua Rais, ulikuwa Mkoa wa pili. Upande wa Chama huu ndiyo mkoa wa chama ambao upinzani wameshindwa kuugusa. Sasa hebu tuwahurumie watu wa Singida. Tutasema mpaka lini. Tulikuwa tumeahidiwa kupata Wilaya mwaka 1979, wakati Babati inagawanywa ilikuwa ianzishwe Wilaya ya Basuto ambayo ingejumuisha Iramba Mashariki, Tarafa ya Dongobeshi na ya Basuto.

Lakini Baba wa Taifa na aliyekuwa Waziri Mkuu, Marehemu Sokoine wakasema tusubiri kwanza. Subira imevuka mpaka. Tunaomba Serikali sasa ichukue hatua. Nirudie kusema hii mikoa niliyoitaja hapa ndiyo maskini, tuongezewe ruzuku na

zitafutwe njia ili na sisi tuweze kuendelea. Mazao tunayozalisha alizeti na mengine yalindwe kwa kuongeza ushuru kwa mafuta ya kutoka nje. *(Makofi)*

Kwanza, hatuna uhakika na mafuta yanayotoka nje juu ya usalama wake. Lakini mafuta ya alizeti hayana tatizo na ndiyo yanategemewa na watu wengi. Hata Shirika la Biashara duniani linasema pale ambapo nchi inaona nchi changa ambayo inaona ina kitu ambacho inaweza kubania na ikakiendeleza inaruhusiwa kufanya hivyo. Lakini sisi wa Kanda ya Kati sisi wa Singida tunaendelea kuumia mwaka hadi mwaka. Naomba Serikali iliangalie hili. Na tulishasema tujengeeni daraja la Mto Sibiti na Mto Simiu, barabara tutasubiri. *(Makofi)*

Sasa hivi kiangazi twendeni mkaone magari yanayotumika kule, hata matela yanapita pale. Ahadi ya kujengewa daraja iko toka mwaka 95. Hebu mwaka huu tufikiriwe, na tulipokuwa tunapitia bajeti ilionyesha kwamba Serikali itapeleka nguvu zake kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo machache niliyotaka kuchangia. Ahsante sana na naunga hoja mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii kwa asubuhi ya leo kuchangia hotuba za bajeti mbili hizi ya Mipango na Fedha. Kwanza, kabla sijaendelea mbele niwashukuru Mawaziri wote wawili, Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao nzuri walizowasilisha juzi Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza na hotuba yangu, kwanza nishukuru sana kwa maelezo ambayo katoa Waziri wa Mipango katika hotuba yake hii ambayo amewasilisha. Lakini kuna suala zima la mipango ambayo nataka kuongezea na katika hotuba yake sikuliona ni suala zima la mipango ya uvuvi. Katika sekta nyingi ameeleza mipango ilivyo. Lakini sikuona jinsi gani uvuvi unavyochangia pato la taifa nchini Tanzania, ikiwa kwenye bahari au kwenye maziwa. Kuna takwimu nyingi alizozionyesha huku madini, ujenzi, miundombinu, jinsi inavyochangia lakini sikuona suala zima la uvuvi jinsi gani linavyochangia katika pato la Taifa ikiwa ni sekta moja muhimu ambayo inaongeza kipato nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilitaka Mheshimiwa Waziri kuja kulifafanua baadaye kuhusu jinsi gani Sekta ya Uvuvi inavyotoa mchango katika pato la Taifa. Suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la ukulima wa mwani katika mwambao wa Bahari ya Tanzania au mwambao wa Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, huwezi kupita kati ya Spika na Msemaji!

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulizungumzia suala la ukulima wa mwani. Katika ukulima wa mwani sikuona jinsi gani mipango ambayo Serikali inaweza ikawasaidia wakulima wa mwani katika mwambao wa pwani ya Tanzania, na sikuona jinsi gani ambavyo anaweza akakomboka mkulima wa

mwani na kuweza kupata soko la uhakika kuhakikisha kuwa anaweza akajikwamua katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho atueleze jinsi gani wananchi wetu wanaweza wakakwamuka katika ukulima wa mwani katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu programu ambazo tayari zipo hivi sasa za kuondoa umaskini nchini Tanzania. Zipo programu nyingi tu lakini utekelezaji wake zingine zinasuasua, utekelezaji wake mwingine wananchi hawaelewi ipasavyo. Ipo haja kwa wananchi kuelimishwa jinsi ya hizi programu zilizopo nchini. Mfano programu iliyopo hivi sasa ya ukulima wa chumvi Zanzibar. Ukulima wa chumvi Zanzibar kwenye mashamba ya chumvi unazungumzwa siku zote na upo na umetengewa fedha katika programu hii na hivi sasa upo katika kijiji cha Wawi Pemba na Zanzibar upo. Lakini wananchi walio wengi hawaelewi nini kinachoendelea katika programu hizi. Ipo haja wananchi waelimishwe na kama wananchi hawajaelimishwa hizi programu zitamsaidia nani na wakati ambapo zimewekwa fedha na zimetengwa na fedha hizi zimo ndani na fedha nyingine ziko nje ya nchi.

Kwa hiyo, ipo haja kuwa hizi programu zinapoingia nchini lazima wananchi waeleweshwe. Kama tutaweka programu nyingi lakini wananchi hawaelewi kinachoendelea katika nchi yao, kwa hivi, inaonyesha kuwa kama tunawadhulumu haki yao. Na inaonyesha kuwa kuna wajanja fulani ambao wanaweza wakahodhi hizi programu na wakatumia pesa bila ya utaratibu ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilitaka kuelezea kwamba hizi programu ambazo zipo zihakikishe kuwa zinafanya kazi vizuri na wananchi wapate taaluma nzuri na waelimishwe juu ya hizi programu ambazo zinakwenda hivi sasa katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu TASAF, kwa kweli TASAF hivi sasa imeingia vizuri sana na inawasaidia baadhi ya wananchi ambao walikuwa hawajui maana ya TASAF kuelewa maana yake kwa sababu inawasukuma katika maendeleo yao ambayo inahakikisha kwamba shule zinajengwa.

Watu wanapata maji, wanajenga barabara na kadhalika. Lakini tatizo kubwa lililopo hivi sasa ni kwamba kuna wananchi wengine wanaelewa nini kinachoendelea kwenye Serikali. Lakini wapo baadhi ya wananchi hawaelewi.

**NAIBU SPIKA:** *Chief Whip* nadhani umepita kati ya Spika na Msemaji!

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mbona nina bahati mbaya kila mtu anapita mbele! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kwamba TASAF tayari hivi sasa imeingia TASAF II, lakini baadhi ya wananchi hawaelewi kinachoendelea na wananchi wengine wanaelewa kinachoendelea, kwa hiyo, ipo haja kwamba tutoe elimu zaidi kwa wananchi kuhakikisha kuwa elimu ya TASAF inawafikia na vile vikwazo ambavyo viko vidogo vidogo kuhusu TASAF tuviondoe ili wananchi waifurahie hii miradi wahakikishe kuwa wanaleta maendeleo katika jamii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la Bajeti ya Serikali hii iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hili suala mimi tokea niingie Bungeni huu ni mwaka wa 12 sasa, lipo linazungumzwa, nalo ni kuhusu Tume ya Fedha ya Muungano ambalo kwa kweli limeshakuwa sugu. Katika taarifa iliyopo hapa ni uchambuzi wa taarifa ya Waziri wa Muungano na Waziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Taarifa hii inachambuliwa vipi wakati ambapo Serikali zinaweza zikaweka bajeti. Yaani kuichambua taarifa ya Tume iliyopelekewa ni kitu ambacho kinachukua muda.

Kikwazo kiko wapi hasa cha kuchukua taarifa muda mrefu mpaka kufikia wananchi wanaona kwamba hizi kero zinatatuliwa kwa njia ya siri, wao hawaelewi. Kwa hiyo, ipo haja hizi taarifa kama zipo, na Tume imeshapeleka hizi taarifa kwa Mawaziri, kwa hiyo, tuchambue hizi taarifa tuzipeleke kwa vyombo vinavyohusika ili tupate taarifa moja tuweze kuitumia ili kuhakikisha kuwa baadhi ya kero zinaondoka. Kwa sababu ilikuwepo kero zamani ya *TRA* lakini ilipoonekana kero hii ya kisheria zikaondoshwa baadhi ya sheria na kufanyiwa kazi na hivi sasa inafanya vizuri na baadhi ya mambo ambayo kwa kweli ni kero tuyafanyie marekebisho mara moja ili tuhakikishe wananchi wetu hawapati kero.

Lakini hii taarifa ambayo ipo hapa inaonyesha kuwa na mwakani itakuja taarifa hii hii kuwa Mawaziri wanakutana au hawajakutana kuchambua taarifa. Suala kama hili tunaomba tena lisije Bungeni katika sura hii, lije katika sura nyingine ambayo hatujajua kero zinatatuliwa vipi na hii fedha ambayo imezugumziwa inakuwa na utaratibu gani Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni ubinafsishaji *PSRC.* Mheshimiwa Waziri leo amenijibu vizuri sana na ametoa takwimu za mafanikio na matatizo. Lakini sasa *PSRC* inamaliza muda wake ifikapo Desemba mwaka huu.

Sasa kiwepo chombo ambacho kitasimamia utekelezaji wa yale mashirika ambayo yamesimamiwa na *PSRC* ambayo tayari yameshabinafsishwa, ambayo tutahakikisha kuwa ufanisi unapatikana ili kuhakikisha kuona ubinafsishaji umeleta mafanikio zaidi. Huu ulikuwa ni ushauri wangu kwa chombo ambacho tayari au kama sheria iundwe ya kukiongezea muda hii *PSRC* au kiundwe chombo kingine cha kusimamia utaratibu mzima wa utekelezaji wa hayo ambayo yamekubaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ninataka kuzungumzia ni kuhusu *BoT*. *BoT* kwa kweli nilikuwepo katika Kamati ya Fedha na Uchumi, tumezunguka

nafikiri katika matawi mengi ya Benki Kuu ikiwemo Mwanza, Mbeya, Zanzibar na Dar es Salaam. Tumeona mafanikio yaliyopatikana hata kama yapo matatizo madogo madogo ni ya kawaida yanaweza yakatatuliwa. *(Makofi)*

Lakini *BoT* inatoa ushauri mzuri wa kitaalamu na kiuchumi kwa Taasisi za Fedha. Suala zima ambalo nataka kuliulizia, tulipoenda Mwanza tukaona taarifa nzuri ambazo *BoT* wametoa kuhakikisha kuwa uchumi wa Tanzania unategemea vyanzo vifuatavyo:-

Wakasema kuwa madini, minofu ya samaki, miundombinu, n.k. yakaelezwa pale. Sasa suala zima nataka kuliulizia *BoT* Zanzibar inashaurije uchumi wa Zanzibar wakati ambapo tatizo lipo. Ukiona mfumko wa bei tulionao Tanzania nzima unakua unawiana kwa sababu taarifa ya Benki Kuu ni moja.

Lakini ukiona bei ya Zanzibar na Tanzania Bara ni tofauti, sasa tunashauri vipi wakati ambapo wananchi wanategemea kuwa ushauri mzuri unatokana na Benki Kuu juu ya uchumi uliopo Tanzania. Sasa jinsi gani Benki Kuu inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu uchumi hivi sasa. *(Makofi)*

Kwa sababu ukiangalia karafuu hivi sasa haina soko ulimwenguni, imeshuka kabisa. Je, kama *BoT* inashauri nini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu uchumi wake mbadala utakuwaje huko tunakoelekea. Sasa nilipenda kuwa hili suala lieleweke kuwa *BoT* kama ni chombo cha ushauri ijue kuwa mfumko wa bei ukoje Zanzibar, uchumi wa Zanzibar unaendaje, na zao ambalo litakuwa mbadala wa karafuu litakuwaje kuhakikisha kuwa uchumi wa Zanzibar unakua katika miaka hii tuliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo nataka kulizungumzia la *TRA,* ukweli *TRA* inafanya vizuri sana nchini Tanzania. Inapita lengo katika makusanyo yake yote na kwa kweli ni watu ambao ni lazima tuwasifie hivi sasa ni taasisi ambayo kwa kweli inafanya kazi ipasavyo. Lakini ipo haja na wao kuwapongeza, kwetu ilikuwa nashauri kuwa hivi sasa kuwaweka katika hali nzuri tuwape bajeti yao kama tunavyozipa taasisi zingine za kifedha na wao wanakuwa na bajeti yao wenyewe bila kutegemea Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Lingine ambalo nataka kulizungumzia Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba *TRA* inafanya kazi vizuri sana. Lakini kufanya kazi kwa *TRA* ni kuijenga miundombinu ya *TRA* iwafikie walipa kodi na waweze kukusanya kodi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima tulililoliona katika ziara tuliyotembelea Horohoro, kwa kweli *TRA* inafanya kazi katika mazingira magumu sana. Lazima tufikie mahali tuwaonee huruma kwa hili. Tumeenda katika kituo cha Horohoro ambako wanakusanya makusanyo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia hotuba hizi mbili. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kuwapongeza wananchi wa jimbo la Lushoto kwa kutekeleza Ilani ya CCM kwa ari, nguvu na kasi mpya. *(Makofi)*

Ndani ya miezi 15 jimbo la Lushoto wameweza kujenga sekondari mpya 16, vyumba 55 vya madarasa na kukidhi nafasi za wanafunzi 2,200 na sekondari nyingine 7 za Makole, Kilole, Tambwe, Kwekanga, Mshangai, Irende na Kwembago ziko katika hatua mbalimbali na itakapofika Oktoba 2007 jimbo hilo litakuwa na sekondari 27 na hivyo kuvuka malengo ya Ilani ya 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutumia Bunge hili naomba kuwaarifu ndugu zangu wa Tarafa ya Mlola, Jimbo la Lushoto, kwamba kero yao kubwa ya barabara ya Mlalo-Mlola na barabara ya Lushoto-Mlola, ninaendelea kuihimiza Serikali na *TANROADS* waitengeneze barabara hiyo ipitike kwa kipindi chote cha mwaka. Barabara hii ni kero kubwa na kikwazo kikubwa sana cha maendeleo ya Kata ya Kwai, Malibwi, Mlola na Makanya. Mwaka huu kwa kipindi kirefu barabara hiyo ilijifunga. Hivi karibuni nilipita na watu wa *TANROADS* kuikagua tukakuta maharage yameoza, matunda yameoza, mboga zimeoza na hivyo kuchangia kuongeza umaskini wa ndugu zangu wa Tarafa ya Mlola. Naiomba sana Serikali kwamba pamoja na umuhimu wa nguvu ya soko, nguvu ya soko peke yake bila kuwakwamua wananchi wetu kwa kuweka miundombinu ya kiuchumi inayowezesha kazi zifanyike kwa ufanisi haitoshi kwani umaskini utaendelea katika baadhi ya maeneo na hivyo maendeleo yataendelea katika baadhi ya sehemu zenye miundombinu mizuri na kule ambako miundombinu hakuna kabisa wananchi wetu wataendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa hii ya Milola ina shida ya barabara, haina umeme, haina simu, haina maji, kwa hiyo, ni matatizo makubwa. Naomba Mawaziri watakaohusika katika bajeti hii watusaidie sisi wa Tarafa ya Milola tuwe na barabara nzuri, tuwe na umeme ufike kule, minara ya simu iwekwe kule, na vitu vingine kama hivyo vya kuibua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hotuba ya Mipango na hotuba ya Waziri wa Fedha, kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali na Mawaziri kwa Bajeti nzuri na naunga mkono hoja zote mbili, isipokuwa nikumbushe kwamba miaka ya nyuma Serikali yetu labda ilisikiliza sana sehemu au uwajibikaji wa Serikali katika usimamizi wa uchumi, baadaye tukadhani nguvu ya soko ilihitaji kutiliwa maanani zaidi. Lakini niseme kwamba kinachohitajika hapa ni kufanya *balance* kati ya nguvu ya soko na *intervention* ya Serikali yetu. Sasa basi, ningetaka kutoa mchango wangu katika maeneo maangalizi machache, kuomba ufafanuzi na kutoa ushauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kazi ya kupanga, kufuatilia na kusimamia malengo yetu makuu ya uchumi, si kazi rahisi. Nilikwishafanya kazi katika Wizara ya Fedha miaka 20, najua kazi ilivyo ngumu ya kupanga bajeti. Sasa ushauri hapa ni kwamba pamoja na malengo haya mazuri, naziomba Wizara hizi mbili zijiwekee

utaratibu wa kukaa na wadau wote wa kisekta hata mdau mmoja mmoja ili uwepo utaratibu wa kufuatilia malengo hayo makuu na madogo ya kiuchumi na ikiwezekana kuwakwamua wazalishaji na wauzaji mathalani, wauzaji nchi za nje kila ponapojitokeza haja ya kufanya hivyo. Hapa nazungumzia suala la *performance exports* zetu.

Kwa hiyo, naishauri sana Serikali kwa ufupi iwe inachukua hatua ya kukokotoa malengo yote haya mpaka kwa sekta mojamoja mzalishaji mmojammoja, *exporter* mmoja mmoja, maana nikitoa mfano wa barabara wa kujifunga barabara ikijifunga basi muuzaji wa pamba, chai na kadhalika atakwama. Nimeangalia kipengele mathalani katika miundombinu ya barabara kule Wilaya ya Lushoto tunalima Chai lakini sioni pale barabara za chai, sasa hata ukilenga kuongeza uzalishaji wa chai kwa kiwango fulani, ukalenga ku – *export* chai kwa kiwango fulani kama barabara za chai zitajifunga basi malengo yale hayataweza kufikiwa. Hapa niseme kwamba masuala haya ya miundombinu mimi kwa maoni yangu yana uhusiano wa moja kwa moja na *performance* ya *export*, ujazo wa fedha na umaskini. Unapoweza kukwamua miundombinu hii ya kiuchumi basi utakwamua *export*, umaskini na utapunguza ujazo wa fedha au utasaidia kuimarisha thamani ya fedha ya nchi yetu. Suala lingine ambalo mimi hapa limenifurahisha ni hili la kupeleka madaraka zaidi Wilayani yaani *D by D*, lakini tahadhari imetolewa na wenzangu Wabunge na mimi naunga mkono kwamba ukipeleka madaraka haya ya matumizi au ya maamuzi zaidi ngazi ya Wilaya basi upeleke mafungu ya fedha na upeleke wataalamu katika ngazi ile ili ufanisi unaotarajiwa uweze kufikiwa na hapa nilikuwa nimshauri ndugu yangu mpendwa Waziri wa Elimu na Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri na kwamba kwa wingi huu sasa wa sekondari za wananchi je, isingekuwa vizuri usimamizi, umiliki na majukumu mengine ya sekondari hizi yakapelekwa Wilayani ili Wizara sasa ikabaki na majukumu yale makubwa ya kusimamia sera, taaluma na mambo mengine kama ambavyo inasimamia shule binafsi.

Kwa upande wa barabara hizi, sisi wa Wilaya ya Lushoto ni sehemu ya milima mara nyingi jiwe linadondoka barabarani, jiti linadondoka na mara zote mnaweza mkakaa siku tatu au nne tatizo hilo bado mnalo kwa maana *TANROADS* wako Mkoani Tanga. Sasa hapa ushauri wa ndugu yangu wa Miundombinu kwamba hivi je, isingewezekana *TANROADS* kuwa na ofisi Wilayani au isingewezekana Wahandisi wa Wilaya kuwa mawakala wa *TANROADS* kwa kazi hizi za *emergence*? Barabara inajifunga, Mhandisi wa Wilaya anaweza kuwa na *budget line* ya *TANROADS* kuweza kuingilia haraka? Kule kwangu tatizo lilipotokea ilibidi nimpigie simu Afisa wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga akusanye nguvu aje, naona utaratibu huu wa *D by D* basi ungehusisha maeneo kama hayo na mengine yanayofanana na hayo.

Mwisho, kwa vile sitaki kupigiwa kengele ya pili nilitaka niishauri Wizara kwamba suala la mafuta ya taa limezungumzwa sana hapa na suala la *balanced budget* mimi naliafiki moja kwa moja na niseme tu kwamba labda kama haitawezekana kufanya marekebisho wanayoomba Wabunge katika bajeti hii kulingana na muda basi Wizara ya Fedha inajua kwamba inaweza kufanya hivyo kwa kuleta *supplementary budget* kwa kipindi muafaka ili Wizara sasa ipate nafasi ya kutafakari uwezekano wa kupunguza viwango vya kodi katika maeneo kama vile ya mafuta ya taa ambayo yanawagusa

wananchi wengi vijijini na kuweza kuyapeleka sehemu nyingine ambazo hazitaleta usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache nasema naipongeza Serikali na ninaunga mkono hoja na ninawatakia kheri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. JOYCE NHAMANILO MACHIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu.Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natoa salamu za rambirambi na pole kwa waliopatwa na ajali nje kidogo ya Mji wa Singida, pamoja na salamu hizo naomba niweke angalizo au mjadala kwa Wizara husika inayohusika na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara husika ijadili suala lifuatalo ili kupunguza ajali kwa sababu tunapoteza uhai wa watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha kusikitisha au kinatisha basi linaondoka Mwanza saa 12 asubuhi na lifike Dar es Salaam saa 4 usiku siku moja hiyohiyo, je, kitu hicho kinawezekana? Kama kinawezekana hizo *speed governor* Serikali ilizipeleka wapi? Maana yake moja ya vitu vinavyochangia ajali ni *speed* za magari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepanda basi linalotoka Mwanza na limetoka saa 12 na nimefika hapa Dodoma saa 10 Jioni, kwa maana hiyo kwa vyovyote vile kama walivyodhamiria walifika Dar es Salaam. Sasa je, mwendo uliokuwa unatumika si wa kawaida, kwa hiyo, naomba Wizara husika ijadili hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo napenda niwapongeze Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa maandalizi ya bajeti yao kwani mipango yao ni mizuri na mafungu yao wameyaainisha vizuri. Lakini pamoja na pongezi hizo nami nitachangia lakini kabla ya kuchangia naomba nitoe pongezi za dhati kwa Serikali kwa suala la elimu katika Mkoa wa Shinyanga, nashukuru wameunga mkono nguvu za wananchi na kufufua vyama vya Ushirika vya SHIRECU na NYANZA ambavyo ni mkombozi wa Wakulima wa Pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitoe pongezi za dhati kwa kufufua kiwanda cha nyama cha Shinyanga na Mbeya hayo ni matarajio mazuri na ni matazamio ya Watanzania wengi wanaojihusisha na mambo ya mifugo yatawainua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba niingie moja kwa moja ili na mimi nitoe machache niliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga ni kati ya Mikoa inayolima mazao ya biashara na chakula, kitaifa mazao ya biashara na chakula yanayotakiwa yatiliwe mkazo ni pamoja na zao la Pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie moja kwa moja katika zao hili la Pamba katika Mkoa wa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga ni kati ya Mikoa inayozalisha kwa asilimia kubwa Pamba, 60% ya pamba ya pato la Taifa inatoka Mkoa wa Shinyanga na 30% inatoka Wilaya ya Bariadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika mikakati ambayo Serikali inapanga na katika kuleta mapinduzi ya kilimo zao hili basi litiliwe mkazo yaani uwepo mpango maalumu kwa sababu mkoa huu hakuna zao lingine linazowasaidia wananchi kuinua kipato chao tofauti na pamba. Kwa hiyo basi, kama ndiyo hivyo, ili tufanane na Watanzania wengine ambao wapo katika mikakati ya kuzalisha kwa hali ya juu basi na sisi pamba tunaomba iwekewe mpango maalumu ili tuweze kuendeleza zao hili na kuendeleza kupata pato la Taifa kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo madini ya dhahabu, almasi na ng’ombe pia lakini hayo yote yanaingiza pesa katika pato la taifa. Wananchi wa Shinyanga na Mwanza kuhusu Pamba ni wasikivu na watulivu lakini siyo kwamba wanabeza mipango mizuri ya Serikali ambayo imekwisha fanyika, kinachotakiwa hapa ni kuboresha. Kwa hiyo, tunaomba japo kwa bajeti hii haitawezekana, tunaomba basi kwa sababu bajeti yetu ni endelevu Serikali ifikirie kuweka mkakati maalumu wa zao hili kama nilivyoongea. Pia uboreshaji huo uende sambamba na ruzuku ya pembejeo. Sisi tumekuwa tukizalisha pamba kwa kutumia elimu dunia kwa sababu ukiangalia Mkoa wa Shinyanga kielimu tupo nyuma lakini wananchi wa Shinyanga si wazembe wanatumia nguvu zao za ziada kuzalisha na kujiwezesha kama Mheshimiwa Mgana I. Msindai alivyozungumza akaweka na asilimia, mimi bahati mbaya siyo mtaalamu wa kupembua hizo asilimia lakini ninachojua ni kwamba wanajituma.

Kwa hiyo basi, tunaomba huo mkakati uwepo, pembejeo zitolewe, ruzuku ipatikane kwa muda muafaka ili tuweze kumudu kukingana na wadudu waharibifu wa zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwamba kilimo cha pamba kiendelezwe, nina maana mkakati wa umwagiliaji ndiyo hoja yangu ya msingi na ndiyo hoja ya wakulima wa Shinyanga na Mwanza kuhusu pamba.

Umwagiliaji yaani miradi mikubwa kama ile ya Kanda nane, ile mikakati ya umwagiliaji basi na mikoa hii iunganishwe kwa zao la pamba kuwe na Kanda maalumu ya kilimo cha umwagiliaji kwa ajili ya pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili iko katika Sekta ya Ardhi. Katika kuupunguza umaskini ni pamoja na matumizi bora ya ardhi kwa kuzingatia sheria za ardhi zilizopitishwa ili Mtanzania aweze kuinua kipato chake ni pamoja na matumizi ya ardhi. Tumekuwa na zoezi la ukopeshaji kwa kupitia *SACCOS* lakini sehemu kubwa ya wakulima na wafugaji wameshindwa kukopesheka kwa sababu hawana dhamana.

Sasa kwa kupitia Sheria ya Matumizi ya Ardhi ninaomba Serikali iweke mkakati maalumu kama kweli tunataka kufanya mapinduzi ya Watanzania, Serikali iweke mkakati maalumu vijiji vipimwe na watu wapate hatimiliki ili waweze kukopesheka kwa sababu sasa hivi bado tupo nyuma sana.

Nimeangalia na kupekua katika vitabu kwa uwezo wangu nimeona suala la upimaji wa ardhi lipo lakini kama bado lipo mbali. Sasa pamoja na kuwa tuna vipaumbele naomba basi na hili suala la ardhi liwekewe mkakati maalumu hata kama itashindikana kubadilisha mafungu kipindi hiki lakini kwa bajeti ijayo basi kati ya vipaumbele vitakavyokuwa vimewekwa ardhi na yenyewe iwe ni mojawapo ili hivi vitu tuvikamilishe yaani tukamilishe zoezi la upimaji wa mipaka ya vijiji na nchi nzima.

Katika mipaka ya vijiji kuna watu wameongea kuhusu mipaka ya nchi lakini pamoja na hayo mimi nimelenga kuangalia mwananchi ambaye tunamwakilisha ana maisha ya dhiki, sasa ni vema kama tunavyozungumza kwamba watu warasimishwe, naye rasilimali zake zirasimishwe, hii itapendeza sana. Lakini sasa hivi ukiangalia katika bajeti tengeo ambalo limetolewa kwa Wizara ya Ardhi linakidhi lakini ni kama halikidhi yaani tuseme tu halikidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo basi naiomba Serikali ione umuhimu wa kuweka tengeo kubwa ili kukamilisha mipango yote hii, unasema utapima mipaka lakini fungu hujatoa kwa hiyo, unaipimaje hiyo mipaka? Tuna matatizo mengi katika sekta hii ya ardhi, sasa tutayamalizaje kama hatuwezi kufunga mkanda na kuweka fungu la kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hayo maeneo yawekewe mkakati maalumu ili tuweze kuondokana na hayo matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba nimalizie hoja ya tatu ya elimu. Pamoja na shukrani nilizozitoa hapo awali, naiomba Serikali bajeti ijayo iweke pia mkakati wa kujenga mabweni kwa ajili ya hizi sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekondari tumejenga nyingi sana lakini mazingira yaliyopo kule watoto wetu hayapendezi itakuwa ni vema kama Serikali itaendelea kuuendeleza huo mpango kwa kuweka mabweni ili tuweze kuwaweka watoto wetu katika mazingira mazuri na waweze kukidhi kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie sitaki kugongewa kengele ya pili kwa kusema kwamba naweka angalizo katika kitabu cha Waziri wa Fedha ukurasa wa 59 kuhusu upitishaji wa bidhaa bandarini. Naomba Serikali iwahakikishie Watanzania suala la wawekezaji waliodhaminiwa au waliosajiliwa na *TIC* kupitisha bidhaa bila kukaguliwa je, hakutakuwa na madhara? Kwa mfano, mizigo imepitishwa bila kupekuliwa je, silaha zikiingia kwa hali hii ya dunia ilivyo ngumu tutajihami vipi? Au bidhaa nyingine zikiingia kama madawa ya kulevya kwa sababu pamoja na kumwamini binadamu lakini si mwaminifu kama tunavyotarajia tutafanyaje? Kwa hiyo, naomba hilo angalizo Serikali

iweze kutoa majibu ili kuwatoa wasiwasi Watanzania na mimi mwenyewe ambaye nimechangia hiyo hoja nijiridhishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kutoa ushauri kwa Serikali. Tunapokuwa tumepanga mikakati yetu kwa mfano bajeti inayoishia na mwezi huu tathmini ya miradi iliyokuwa imepangwa kitaifa itolewe kwa kuainishwa iwe imefanikiwa au haikufanikiwa basi ieleweke ili kuondokana na suala la kuwa tunatekeleza miradi ileile ambayo imekuwa ni kero, kwa mfano, barabara ya Dodoma – Singida, Tabora – Shinyanga – Mwanza imekuwa ni ya muda mrefu. Sasa tathmini yake kwa ujumla inatakiwa iwekwe wazi ili na Watanzania waelewe kinachoendelea ili kupunguza kero kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa kuunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana sasa nimwite Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela jiandae na Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina yuko kwenye orodha.

**MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti zetu mbili zilizopo mbele yetu.

Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza timu yetu ya Tanzania kupata ushindi wa kishindo na bado tunawaombea wakielekea huko Mwenyezi Mungu atawasaidia tunaweza tukarudisha kombe hapa nyumbani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uwezeshaji na Uchumi pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa kweli mimi naipongeza sana Serikali hasa kwa kuamua. Kwanza, Waziri wa Mipango amekuja na mkakati maalum na Waziri wa Fedha naye ametueleza kwamba kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii sasa kuishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Nne kuja na mikakati mitatu, mimi nimeitembea nikaona ni mikakati muhimu mitatu ambayo inamgusa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja na suala la barabara, Serikali imeainisha barabara, kilimo na elimu, ukizingatia sekta hizi tatu zinamgusa Mtanzania wa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nizungumzie suala la barabara. Unapotengeneza barabara na zinapitikitika kwa muda wote, mambo yote ya Mkukuta azma yake tunaweza kuifikisha mahali pake. Unapofungua barabara kwa mfano kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma ikawa shwari kabisa, basi wawekezaji watawekeza mahali popote.

Utakapofungua mkoa wa Dodoma, Singida unakwenda Tabora, Shinyanga na Mwanza wawekezaji watakuwa wameleekeza uwekezaji maeneo yale. Unapofungua njia ya Dodoma, Kondoa, Babati kwenda Arusha utakuwa umefungua na wawekezaji waelekee maeneo hayo. Unapofungua njia ya Dodoma unakatisha Mtera kwenda Iringa utakuwa umefungua maeneo yote ya kuwawezesha wawekezaji waendelee maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nilizozitaja ni baadhi ya barabara ambazo zinaelekea kwamba Watanzania watakapofunguliwa barabara hizi na zikapitika kwa saa zote nafikiri na wawekezaji tutakuwa tumewapa njia rahisi zaidi ya kuwekeza katika maeneo hayo na tutakuwa tumefungua Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya, wananchi wetu watalima mazao yao na watasafirisha kwenye barabara safi na tutaweza kujikwamua katika hali ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji ambao sasa kwenye bajeti yetu tutauza mazao mengi nchi za nje wakati tutakapokuwa tumefungua barabara nilizozitaja, uzalishaji wa mazao yetu utaongeza na pato la Taifa litakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la kilimo kwa sababu utakuwa umeshafungua suala la barabara, kwa vyovyote vile kilimo wananchi na wawekezaji wataelekea kwenye maeneo ambayo Tanzania tuna bahati nzuri, tuna maeneo mengi sana ambayo yanaweza yakatumika katika kilimo cha umwagiliaji baada ya kufungua barabara hizo nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kikizingatiwa nina uhakika kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Nne imeliona tatizo hili la kuwekeza katika Kilimo. Wananchi wetu wengi wapo vijijini wanategemea kilimo, nitaomba sasa tuandae maeneo hususan kwa kupangilia kabisa kwamba mikoa fulani tutalima mazao ya biashara na maeneo fulani mazao ya chakula. *(Makofi)*

Nitashukuru sana kama tutaigawa nchi yetu katika suala la kilimo tukaweka kipaumbele kuhakikisha wananchi wetu tunawapa elimu ya kutosha kwa kupeleka pembejeo muhimu na ruzuku kama wenzangu walivyozungumza na pia mazao mengine ya biashara ambayo maeneo mengine hayakutengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika suala la elimu. Katika suala la elimu naipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Nne kuanzia kwenye Awamu ya Tatu iliamua kuwashirikisha wananchi katika kuchangia suala la elimu na wananchi walilipokea sana. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana ambao walielewa jinsi ya kuchangia suala la elimu, wamejitolewa kwa nguvu zao wenyewe, wamejenga sekondari kwa wingi, wameboresha shule za msingi na Serikali yao imeweza kuwasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi niongezee kwa kuiomba Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwa sababu wananchi wanaelewa kwamba suala la elimu ndilo muhimu zaidi kwani ukimsomesha mtoto wako ndiyo utakuwa umempa urithi wa kudumu kuliko

kumjengea nyumba. Ukimpa elimu atakuwa na elimu ya kutengeneza barabara na kuboresha kilimo. *(Makofi)*

Naomba basi, kwa bajeti ya mwaka 2007/8 Serikali ilete mkakati wa kuwashirikisha Watanzania ambao ni wananchi wanaojua lengo la elimu ni nini, yaani wajenge hosteli kwa jinsia zote kwamba isibague walemavu, wavulana na wala isibague wasichana bali ijenge hosteli ili kuwawekea mazingira mazuri wanafunzi waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba Wizara ya Elimu safari hii imetengewa fedha nyingi sana, ninaomba sana walimu wapelekwe kwa wingi katika shule ambazo zimejengwa kwa kushirikiana na wananchi ili watoto wetu wasikae tu kwenye madawati na madarasani bila ya kufundishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria unakatisha kati ya Spika na msemaji.

**MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa suala la kupeleka walimu nafikiri Mheshimiwa Waziri atakuwa amelipokea lakini bado naomba nilete ombi kwenye Wizara yako ya Elimu.

Ili tuwape motisha walimu watakaopelekwa kwenye maeneo yale ya Kata zetu, naomba basi ile *teaching allowance* irudishwe kwa walimu ili iweze kuwapa motisha vijana wetu kwa sababu usipomwekea mazingira mazuri mwalimu itakuwa ni bora tu atakuwa amekwenda pale lakini hawezi akatilia maanani kazi aliyopewa. Basi naomba sana Mheshimiwa Waziri anayehusika katika Wizara kwamba tuwape walimu wetu motisha wa ile *teaching allowance* irudi tena kama zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Wizara ya Fedha. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa ukusanyaji wa mapato, mimi naomba niwaeleze Watanzania wenzangu kwamba hatuwezi kuishi bila kodi, nakubaliana naye tena nawaomba wananchi wote wa nchi hii ya Tanzania tumuunge mkono na tuunge Mamlaka yetu ya Mapato kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yanakusanywa kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua *TRA* wanafanya kazi nzuri sana, mwaka 2007/8 tumewapangia trilioni 3 wao wakusanye kwa mapato ya ndani. Lakini najua Mheshimiwa Naibu Waziri kazi ile ni ngumu sana lakini *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawasadia sana na watapata hizo ila ninamwomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha aongeze wigo kwa maeneo ambayo wenzangu wameshayataja kama Kamati ya Fedha na Uchumi, suala la magogo na kwingine kokote ambapo wapo watu ambao wanakwepa kulipa kodi. Suala la mafuta ya taa na suala la soda naomba aliangalie upya. Naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la upelekaji wa fedha kule kwenye Halmashauri za Wilaya, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza

kwamba watapeleka wahasibu 204 na ninashukuru kwamba Halmashauri zetu ziko 124 katika nchi yetu na wakaguzi 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi ni nyingi sana nitamwomba sana ahakikishe kwamba wakaguzi wanaongezwa zaidi. Halmashauri zetu ni 124, wakaguzi ni 64, hawatoshi na wahasibu nina hakika kwamba 207 watafika kwenye Halmashauri zetu. Lakini namwomba sana Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali awe karibu sana na Halmashauri zetu, sisi tunazifahamu huko nyuma lakini nina uhakika kwamba Wizara hii itahakikisha kwamba inapeleka wahasibu wa kufunga vitabu vyetu vizuri na wananchi niwahakikishie kwamba tuwe na ushirikiano katika kuhakikisha fedha ambazo zinaletwa kwetu tunazisimamia na sisi wenyewe tusiiachie Serikali peke yake.

Naomba adhabu kali kufuata Kanuni na Sheria za Fedha zitolewe kwa wale wote wakaofuja fedha za wananchi na ninaomba sana hao watakaofuja hizo fedha wafilisiwe siyo kumfunga tu kwani ukimfunga tu anaitumikia jela akirudi na mali zake zinaendelea tu nitaomba na mali zao zifilisiwe. Ufanisi ni lazima watendaji wetu na uwajibikaji utekelezwe na hatimaye sisi Watanzania nafikiri tutakuwa na imani na watendaji wetu, wasimamie fedha zetu na wao wawe ndiyo mfano bora wa kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa miradi ambayo imeelekezwa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la pensheni. Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake ametueleza kuwa malipo ya uzeeni sasa yanahamishiwa kwenye mashirika ya mifuko hii ya jamii ya *NSSF, PCSPF, PPF* lakini ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri awaeleweshe vizuri wastaafu hawa kwamba utaratibu ambao utatumika wa kuwahamishia kule, maana yake walizoea kwamba wanalipwa na Wizara ya Fedha, sasa unasema kwamba wanalipwa na mifuko basi elimu itumike sana kuhakikisha kwamba wanawaeleza utaratibu kamili ili wasije tena wakaanza kuhangaika.

Mtu anatoka Mwanza kuja Wizara ya Fedha ndiyo anapata maelezo ndiyo tena arudi kwenye mkoa wake na bahati nzuri sisi pale Mkoa wa Mwanza PPF wako pale, sasa ni maelekezo tu ya wewe Mheshimiwa Waziri kwamba hawa watu wa Kanda ya Ziwa waende *PPF* pale Mwanza au wale wote waliopo karibu na eneo lile la *PPF* lililopo Mkoa wa Mwanza waelekee sehemu hii.Basi nikuombe Mheshimiwa Waziri utoe ufafanuzi ndiyo utakaowasaidia sana Watanzania waelewe, maana yake hawajui hatima yao itakuwa vipi na bado ninaomba tu kwa sababu tukishafanikiwa kukusanya fedha nyingi basi waendelee kufikiriwa hawa wastaafu waweze kuongezewa angalau hata kidogo tena ili kiweze kumudu katika maisha yao. Naomba kuzungumzia suala la uwezeshaji. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais katika kuona jinsi ya kuwawezesha wajasiriamali katika maeneo tulipo na ninashukuru sana kwa huruma yake Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliamua kupeleka fedha kwenye maeneo yetu kila mkoa zisizopungua shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa suala hili kwa kweli limetuchanganya, hata mimi limenichanganya sana kama Mbunge. Wanawake kule mkoa wa Mwanza nimewahamasisha sana wakaingia kwenye *SACCOS,* basi naomba

kupitia Bunge lako Tukufu utaratibu uliotumika kwa awamu ile nusu iliyotoka wauchambue upya.Niombe kwa sababu Watanzania wengi wako kwenye *SACCOS,* utaratibu wa kumpa mjasiriamali mmoja, naomba fedha zipunguzwe kwa mjasiriamali mmoja ziende kwenye *SACCOS,* wananchi wengi wamejiunga kule na ninashikuru kwenye bajeti wameeleza kwamba wataimarisha *SACCOS* zetu.

Niombe sasa fedha zilizobaki ambazo zilikuwa ni dhamana katika benki ya *NMB* na *CRDB* zielekezwe kwenye *SACCOS* na bado namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia kwako Serikali iangalie upya suala la riba kwenye taasisi zake. Taasisi za mabenki hizi ambazo zimewakopesha Watanzania naomba basi kwa sababu Benki Kuu ina uwezo huu wa kuzungumza na hawa wenye mabenki isaidie sana kupunguza riba ambayo inaweza kuwagandamiza Watanzania wengi wakashindwa kukopa hiyo mikopo na kuhakikisha kwamba wakajiimarisha kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kuzungumzia barabara ambayo kila mtu kwa kweli anazungumza. Nilizungumza mkoa kwa mkoa lakini suala la barabara ya Kisesa,Usagala kwenda Geita ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu spika, naunga mkono hoja zote mbili na ninaomba wapewe fedha zote hizo walizoziomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumzia bajeti zote mbili kwa wakati mmoja. Bajeti ya kwanza ni ya Wizara ya Fedha na taarifa ya pili ni Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika 15 ni ndogo, ningeomba niende moja kwa moja kwa yale ambayo nimeona ni muhimu niyaongee. Nilipokuwa napitia bajeti ya Wizara ya Mipango, Uchumi wa Uwezeshaji nikaenda ukurasa wa 54 kifungu cha 77, pale Serikali imeongelea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji ni tatizo ambalo liko Tanzania nzima. Lakini mimi nikisimama ni vyema nizungumze pale ambapo pananihusu. Mimi ni Mbunge wa Same Mashariki. Kwa hiyo, naomba niongee yanayonihusu mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza bajeti tulizonazo mikononi, za mwaka 2007/2008. Lakini mimi naomba nirudi nyuma kama ambavyo Mheshimiwa Mgana Msindai alifanya. Nirudi nyuma kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007 ambayo ndiyo tunayomaliza sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika kipindi kilichopita nilitengewa fedha za miradi ya maji katika Jimbo langu la Same Mashariki, miradi 10. Kule ile ilikuwa miradi ambayo ni papo kwa papo na kuna miradi mingine ambayo inatoka Serikali Kuu na miradi mingine ilitoka Wizarani, lakini kwa kweli ilikuwa miradi kumi.

Mheshimiwa Spika, sasa tunamaliza bajeti mwaka 2006/2007 hakuna mradi hata moja ambao ulipata fedha. Miradi yote ninayo mikononi na ni vijiji vingapi ambavyo vilifanya sherehe vikitegemea kupata kidogo japokuwa kupungukiwa na matatizo ya maji. Nina kijiji cha Miyombo, Karamba, Sambweni, Bendera, Lunguru, Ivunga, Kalemawe, Kabeni, Makokane na Maole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kijiji cha Maole kilikuwa kimepangiwa shilingi milioni 20 katika bajeti ya mwaka 2005/2006. Bajeti ya mwaka 2006/2007 nikaja hapa nikapiga kelele kwamba kilikuwa hakikupatiwa zile fedha. Serikali ikaniambia, hapana, hatukupi tena shilingi milioni 20, tunakuongezea shilingi milioni 10 kwa sababu tulikucheleweshea fedha zako. Kwa hiyo, wakaahidi kutoa shilingi milioni 30. Nakumbuka aliyenipa ahadi hii alikuwa ni Mheshimiwa Stephen Wasira na yupo hapa ndani. Lakini nilisumbuka kweli kuzipata hizo fedha na hazikufika shilingi milioni 30 kama Mheshimiwa Stephen Wasira alivyoniahidi, zilifika shilingi milioni 20 juzi juzi tu na ndiyo zimenisaidia. Sasa mradi ule umekwama, ninaziomba hizo shilingi milioni 10 ambazo alikuwa amesema ameziongezea ziende ili ule mradi ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba hapa nipaongelee kidogo. Wananchi ukishawaahidi kupitia Bunge hili wakifurahi, wakikaa wakifanya sherehe, halafu bajeti inakwisha hawaoni chochote, hii ni hatari kubwa. Nimewaandikia Naibu Waziri wa Maji barua, amenijibu matatizo ni fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwanza ninamshukuru sana baada ya mimi kumwandikia barua nyingi alikuja Jimboni kwangu akaenda akaona chanzo cha matatizo ya maji Jimboni kwangu. Nilimwambia wananchi wangu wengi wanakufa kwa kansa ya tumbo kwa sababu wanakunywa maji ambayo sio salama. Alikwenda na ndoo kwenye chanzo cha maji akachota yeye mwenyewe akayaleta kwa Mkemia Mkuu wa Serikali akayapima maji ambayo ndiyo ninayolalamikia Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeletewa majibu na Serikali, ninayo hapa kuhusu maji wanayokunywa wananchi wangu. Serikali imetoa majibu kwamba yale maji sio salama. Ninayo majibu hapa kutoka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo amenipa Mheshimiwa Waziri. Sasa hivi vijiji nilivyovitaja hapa vinaendelea kutumia hayo maji.

Mheshimiwa Spika, iwapo tumefikia hatua hii, Mheshimiwa Naibu Waziri amechota maji na yamepimwa, Serikali imekiri kwamba hayo maji sio salama, ninaisihi Serikali, katika kipindi hiki kwa sababu maji yamepewa kipaumbele, basi hivi vijiji vyangu kumi pamoja na vijiji kumi vingine vitakavyopewa kwenye bajeti hii, ifike mahali sasa iwafanyie wananchi wangu nao waone kwamba wanastahili kupewa huduma bora. Nafikiri hapo Serikali imenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie suala la pili la Wizara ya Fedha. Lakini niende ukurasa wa 59, ameongelea Mheshimiwa Joyce Machimu, lakini naomba mimi niliongelee kwa sura tofauti kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu kunukuu kauli moja ya Marehemu Mahatma Ghandi ambayo niliisoma katika kitabu kinachoitwa *The Power of a Positive No*. Hiki kitabu kimeandikwa na Mwandishi mzuri sana anaitwa William Harry. Hii kauli inasema hivi, naomba kuinukuu: "A *no altered from deepest conviction is better and greater than a yes merely altered to please or what is worse to avoid trouble*." Hii ni kauli nzito sana kwa sisi viongozi. Sisi Wabunge tuna kazi mbili kuu, kuishauri Serikali na kuisimamia mahali ambapo tunaona hapako sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 59 kifungu cha 55 kinasema: "Umeanzishwa utaratibu wa kupitisha moja kwa moja *(fast tracking)* bila ukaguzi bidhaa zote zinazoagizwa na wafanyabiashara ambao tayari wameainishwa kama wawajibika wazuri katika kulipa kodi." Ahaa! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kubwa kwa Taifa letu. Naomba niwaambie na mimi ni mfanyabishara. Wafanyabiashara wote kuanzia mfanyabiashara mdogo mpaka mkubwa sana nia yake ni moja ku-*maximize margin*, hakuna mfanyabiashara anayefanya biashara kwa nia nyingine, *I beyond there*. Ku-*maximize margin*, sasa jamani Serikali imefikia hatua imechagua inaona wapitishe bidhaa zao bila ya kukaguliwa, wametumia kigezo gani? Mmeingia kwenye mioyo yao lini? Hii ni hatari kwa Taifa letu. Mimi naomba niseme *No! A powerful No*! tunaimaliza nchi sasa hivi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa *TRA* wako hapa wana kesi nyingi sana za kupokea makontena ambayo mtu ameandika kwenye *document* kwamba ameingiza *used* sijui *deep freezer*, *used computer*, wakifungua ndani sivyo, wanakuta bidhaa nyingine tofauti kabisa. Sasa jamani Serikali inakwenda wapi? Yaani sasa hao wafanyabiashara walioteuliwa kwa sababu wao wanalipa sana ushuru *may be,* lakini siku zote hakuna kikubwa ambacho hakijengwi na kidogo. Hao wafanyabiashara wakubwa na wadogo wanajenga nchi. Sasa nyie mmewachagua kwamba makontena yao sasa yakija moja kwa moja yanapita, hivi mnajua jamani kwamba hiyo ni hatari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatari kuliko hatari zote. Mimi naomba hili tafadhari Waziri wa Fedha akaliangalie upya. Kwa upande wangu mimi hili nimelikataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna neno ambalo naomba nilizungumzie kwa viongozi wote wa nchi yetu. Watendaji wote wa Serikali jamani hata Mheshimiwa Rais amechoka. Mheshimiwa Rais kwa kweli yuko *serious* kweli kweli! Ukimwangalia kweli ana dhamira nzuri sana. Mheshimiwa Rais juzi nimemnukuu mimi mwenyewe akizungumza kwamba umaskini wa watu wake unamkosesha raha. Sio yeye tu! Mimi umaskini wa wananchi wangu unanifanya pia nisilale. Lakini jamani huu umasikini wa wananchi wakati mwingine ni sisi wenyewe watendaji tuna-*contribute*. Bajeti hii kukosa fedha kiasi hiki na sisi pia tuna *contribution.* Watendaji wenzetu huko wanaosaini mikataba wana-*contribute a lot.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimnukuu Mheshimiwa Rais, siku ya kwanza alipotuhutubia hapa, alisema: "Lakini katika harakati za kupambana na rushwa, yapo mambo mawili muhimu ambayo tutaangalia kwa karibu. La kwanza, ni Mikataba." Alipozungumza hivyo alikuwa ameona kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninawasihi ndugu zetu wote viongozi ambao mna dhamana ya kusaini Mikataba, hebu waweke uzalendo mbele kwanza. Wekeni uzalendo ili nchi hii isiishie.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano mzuri, mimi nimefanya kazi katika Shirika la Ndege la Tanzania kwa muda wa miaka minane, nilikuwa na Mheshimiwa Lucas Selelii, nilikuwa *Finance Department*, tulikuwa ndiyo tuna-*control* fedha ya Shirika la Ndege la Tanzania. Kazi yangu ya mwisho baada ya miaka nane nikawa *Financial Controller* wa Shirika la Ndege la *Gulf* kwa miaka minne. Shirika letu limekufa lakini ni Mkataba mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze la kwanza kwa nini Mkataba ule ulikuwa mbaya. Tulipoingia kwenye Muungano na *South Africa Airways,* kosa ambalo tulifanya ni ku-*surrender* tiketi yetu. Tiketi yenye *code* 197 tukaiacha tukaenda kwenye tiketi 083 ya *South Africa Airways*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya vile haikuwa lazima, tungeweza kuungana na *South Africa Airways*, lakini tukaendelea kutumia tiketi zote kwa wakati mmoja kama ambavyo Kenya *Airways* na *KLM* wanafanya mpaka leo. Sasa hii mikataba tusipoiangalia tukawa tunakwenda tuna-*sign*, jamani itafika wakati tutakuwa hatuna hela hata za kuja kupelekea wananchi wetu. Mimi nina *data* zote ambazo *of course* ziko wazi. Mwaka wa kwanza tulipata hasara kiasi gani *ATCL*? Mwaka wa pili tulipata hasara kiasi gani? Mwaka wa tatu, mahesabu hayakuwa *audited*. Tulikwenda kwenye mkataba ambao hatukuweka uzalendo kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumza mikataba, jamani wenzetu Serikali wasikasirike. Mheshimiwa Rais alipozungumza siku ya kwanza alizungumzia mikataba, mbona hawakukasirika? Mimi ninawasihi jamani kila ambaye ana-*sign* mkataba amweke Mwenyezi Mungu mbele, amwogope Mwenyezi Mungu. Hii nchi siyo masikini kiasi hiki. Katika nchi bora tano za Afrika zenye *natural resources* za uhakika Tanzania *is among them*, hata ukisema tatu, Tanzania tupo. Jamani hivi kwa nini sisi ni masikini? Ni kwa sababu ya utendaji wetu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ifike mahali niiombe Serikali *seriously,* unajua ukimwangalia nyani usoni wakati analia, anatia huruma kuliko mwanamke aliyefiwa na mume wake. Nyani akila mazao yako ukitaka kumuua usimwangalie usoni, utamwonea huruma. Huu umasikini wetu tulionao unachangiwa na watendaji wenzetu ambao Mheshimiwa Rais amewaamini akawaweka na bado wanamfanya akose raha. Kauli zake zote anazozungumza Waheshimiwa Wabunge, tumwonee huruma Mheshimiwa Rais wetu. Kila mtu mahali pake pa kazi atimize wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa wasemaji wetu wa mwisho watakuwa Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na tutamalizia na Mheshimiwa Fred Mpandezoe Tungu kwa mchana huu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Mawaziri wawili. Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha kwa kazi waliyoifanya wakatuletea hapa ili kuweza kuichambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya bajeti ni kubwa ambayo inaanzia katika kaya zetu. Kwa hiyo, ukiwa na bajeti nzuri katika mji wako ujue utaendelea vizuri na kazi itafanyika kama inavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia ni kwamba, nilikuwa naomba sana kwa Watanzania wote tujielekeze katika kufanya kazi. Tukifanya kazi hata Wizara zitafanya kazi nzuri sana ya kutengeneza bajeti zake. Kitu kinachotusababisha sasa hivi Watanzania tumekuwa wavivu. Nayazungumza haya kulingana na maeneo ambayo nayajua. Sasa hivi tunakimbia kutoka vijijini tunakimbilia Mjini, na tunapokimbilia Mjini kitu tunachoenda kukifuata hakuna, sana sana tutaanza biashara ndogo za kuuza karanga ambazo hazina pato la Taifa. Ninachowaomba tujikite na Serikali isisitize sana katika suala la kilimo. Serikali ikishasema nadhani hakuna mtu ambaye atabisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kila mkulima anaona kwamba maisha bora yako Mjini. Kwa hiyo, wanakimbilia kwenda Mjini, wengine wanakosa sehemu ya kukaa, basi wengi wao wanakaa vijiweni, vijiweni ndiyo wanaanza kuijadili bajeti. Sasa hivi utawakuta wako vijiweni wanaijadili bajeti hii, wao ndio wanaotoa mwelekeo na wao ndio wanaotoa kila kitu. Sasa naiomba Serikali ikasisitize kuwaambia wananchi warudi vijijini kwenda kufanya kazi. Bila hivyo tutakuwa tunalaumiana hapa bila kufikia malengo yanayohitajika. Hilo lilikuwa la mwanzo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona katika maeneo mbalimbali hasa katika Wilaya zetu, kila mmoja hapa ana uhakika kabisa kwamba hata akienda katika Wilaya yake atakuta kuna vijiwe vingi tu wanatengeneza vijiwe vya kahawa. Utakuta kuanzia asubuhi watu wanakunywa kahawa mpaka jioni. Watazalisha nini? Huo kwa kweli siyo uzalendo. Wananchi wa Tanzania tuwe wazalendo katika kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuja katika suala ambalo ni muhimu. Tutakumbuka kabisa kwamba mwaka 2006 tulivyokuwa hapa Waheshimiwa Wabunge wa Sengerema, Misungwi, Magu, Geita na maeneo mengine yanayoelekea kule, tulidai barabara ya kutoka Usagara kwenda Geita na kutoka Kisesa kuja Usagara. Ninashukuru sana kwa sababu tuliweza kuambiwa maneno mazuri. Hayo maneno nayafananisha na sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa; Wasukuma kukiwa na njaa ili uweze kuhimili nyumba yako utafanya kitu ambacho ni cha kuwadanganya. Unaweza ukainjika chungu, mle ndani ukaweka hata kitu chochote unaanza kuchemsha ukawaambia tulieni mtapata

chakula hivi karibuni. Lakini kile chakula hakitaweza kuiva mpaka jioni unapoweza hata kuwapa uji watu wakanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii sisi tulipewa ahadi, tukapewa ahadi tukadanganywa chungu kimechemka mpaka leo hii hata kidogo hakuna. Kwa kweli hili suala linasikitisha. Tunaomba barabara ya kutoka Kisesa-Usagara- Geita ili tuweze angalau na sisi tukajikwamue katika uchumi wetu wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalizungumza hili, lakini mwenzangu amelizungumza kwa uchungu sana mpaka akataka kulia hapa. Lakini sisi wengine tunazungumza kwa ujasiri ili Serikali itusikie. Bila kuyazungumza haya utakuta tumepewa kitu ili tuweze kuanza kumlaumu hata Waziri wa Miundombinu wakati sio hivyo. Waziri wa Miundombinu wa sasa hivi ameyakuta haya hatuwezi kumlaumu. Lakini tunailaumu Serikali kwa ujumla kwamba lazima itutengenezee barabara Usagara-Geita *by pass* Kisesa, bila hivyo ni tatizo.

Naiomba Serikali itusikie, ituelewa ili tuweze kwenda kuwaambia wananchi kwa sababu katika maeneo yote tunawaambia wananchi kwamba tumeshakubaliwa kuna barabara hiyo. Leo hii tunakwenda kuwaambia kwamba mpaka mwaka kesho. Haya yatakuwa ni maneno gani? Naiomba Serikali ituelewe kwa hilo, bila hivyo utakuta kwa kweli masuala yatakayokuja kujitokeza hapa tusilaumiane. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nitazungumzia miradi ya maji. Miradi ya maji yote ya fedha za Serikali za ndani itatekelezwa, lakini kwa fedha ambazo ni za kutoka nje hasa *Millennium Challenge Co-operation* walisema kwamba hazijapangiwa chochote. Sisi Wilayani Geita tuliambiwa mradi wa kuleta maji Geita utatokana na *Millennium Challenge Co-operation*. Je, hao *Millennium Challenge Co-operation* wasipoleta fedha ina maana Geita haitapata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku ninachokiomba ni kwamba itakuwa ni vizuri zaidi tunapotegemea miradi kutoka nje, basi tuitegemee na Serikali itakuwa inatenga kiasi gani. Nataka kuuliza kwamba katika mradi huo Serikali imetenga kiasi gani ili kuweza kutekeleza mradi wa maji Geita ambao utagharimu shilingi billioni 18.5? Serikali imetenga kiasi gani katika hizo hata kama *Millennium Challenge Co-operation* itashindwa, basi tuanze kwa awamu kwamba tuanzie wapi na tutaishia wapi. Lakini tunapotegemea tu mradi, wasipoleta hizo fedha wananchi wa Geita watapata wapi maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tunasema kwamba maji ya Geita karibu visima vyote au maeneo yote yana zebaki: Je, hao wananchi wa Geita tunategemea kwa muda wa miaka mingapi watakuwa wamekwisha katika eneo hilo? Ukiangalia hakuna mji mwingine katika Tanzania hii ambao uko kwenye machimbo ya madini kama ilivyo Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Geita ni eneo mojawapo ambalo lina machimbo ya madini. Nyumba zote ziko juu ya dhahabu, lakini unakuta kwamba wananchi wake hata maji wanakosa Serikali inasema nini? Kwa sababu huu mradi

unaonekana mtu anaweza akasema, basi sisi hatuleti fedha, ina maana wananchi wa Geita watakuwa wamekosa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaahidi miaka mitatu iliyopita kwamba *UN Habitat* walikuwa na mpango wa kuleta maji Geita, lakini mpaka sasa hivi wametekeleza katika Wilaya moja tu ya Muleba. Lakini katika hizo Wilaya tano, nyingine hazijapata. Je, na huo mradi ukiwa kama *UN Habitat* tutafanya nini? Naiomba sana Serikali itusaidie kwa hili, itenge fedha za ndani ili kuweza kutekeleza suala hili la maji katika Mji wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni la usafiri wa majini. Usafiri wa maji umeshakuwa kero kubwa. Wakati ule ule utaona kwamba Mkoa wa Mwanza asilimia 45 ya Mkoa wote umezungukwa na maji. Sasa ujue kabisa kwamba kama kuna asilimia 45, asilimia 55 ndiyo nchi kavu, wananchi wanategemea sana Ziwa lile na kama wanategemea Ziwa lile wanalitegemea kwa usafiri, lakini ukiangalia vyombo vyote viliachwa miaka ya sitini ndiyo hivyo hivyo vinaendelea kutumika na vimechakaa na Serikali haijafanya mpango wa kuweza kununua vyombo vingine vipya. Je, Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi vivuko vyote, kivuko cha Kome hakuna, kivuko cha Chato ambacho kinaitwa Njuzi hakipo, kivuko cha Busisi-Kigongo hakuna, kivuko cha Ukerewe hakuna. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usafiri ndani ya Ziwa Victoria? Hilo ni moja kuhusu usafiri.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Ziwa Victoria tunahitaji ulinzi. Wavuvi waliomo ndani ya Ziwa Victoria hawana ulinzi wowote, Ziwa limekuwa la kila mtu. Kuna wananchi kutoka nchi mbalimbali wanatoka Zaire, wanatoka Burundi wamo ndani ya Ziwa Victoria. Kuna ulinzi gani ndani ya Ziwa Victoria? Ninaiomba sana Serikali iangalie na ilinde rasilimali zake kwa sababu hao wanakuja kuvua na kusafirisha samaki bila hata kulipia ushuru kwa sababu hakuna ulinzi wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna visiwa ambavyo sasa hivi hujui ni vya Serikali gani! Watu wanaishi kama wanavyopenda, wakati ni visiwa vya Tanzania. Je, kweli Serikali inaweza ikaviachia visiwa hivyo vikakaa tu bila kuwa na utawala wa aina yoyote? Naiomba sana Serikali iangalie usalama katika maziwa yetu. Nina uhakika ninapozungumzia Ziwa Victoria hata Maziwa mengine kama vile Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa yatakuwa na matatizo kama hayo hayo. Kwa hiyo, naomba mipaka yetu ilindwe ndani ya Maziwa na ndani ya Bahari zetu. Hilo lilikuwa ni la kuweza kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kuhusu pensheni. Tatizo la pensheni limekuwa ni tatizo kubwa sana. Kuna watu wanaostaafu sasa hivi wanakwenda kufa, lakini si lengo la Serikali au sio lengo la mtu yeyote anapostaafu eti akafe, ni kubadilisha uelekeo tu kwamba anakwenda kufanya kazi yoyote ile. Ninazungumzia wastaafu ambao wamestaafu kuanzia mwaka 1996 kurudi nyuma. Hao wameonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iwaangalie kwa huruma hao wastaafu. Wastaafu hao wengine walikuwa wana vyeo vikubwa, lakini aliyestaafu leo hii

kama dereva anamzidi kipato, itakuwa vipi? Kwa hiyo, wastaafu wanakuwa na ile hali ya kuichukia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kusiwe na utaratibu kwa waliostaafu wa miaka ya nyuma wakalinganishwa mapato yao na waliostaafu hivi karibuni ili malipo yao yaende sambamba kulingana na jinsi hali ya uchumi inavyokwenda ya Serikali. Mtu alikuwa Katibu Mkuu miaka ya themanini, leo hii analipwa Sh. 20,000/= eti kwa sababu wakati ule malipo yake yalikuwa hivyo. Kwa nini kusiwe na mabadiliko kutokana na hali ilivyo sasa? Ninaiomba sana Serikali ibadilishe utaratibu kulinganana muda unavyokwenda. La sivyo, utakuta kwamba mtu anapostaafu analazimika kuichukia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Magu kwa kunichagua tena kwa kishindo kwa kuwatumia katika awamu ya 2005/2010 naahidi kwamba nitawatumikia kwa nguvu zangu zote kadri ambavyo Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda niwapongeze Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri waliyoifanya ambayo sasa tunajadili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe rambirambi kwa waliopata ajali katika basi la *Mohamed Trans* pale Singida. Naomba Mwenyezi Mungu, awarehemu na matarajio yetu ni kwamba tutakuwa tumejifunza yale yaliyosababisha vifo hivyo ni kwamba yatachukuliwa na Serikali kwa ajili ya kurekebisha kwa mfano magari mengi sasa hivi nyuma yamechorwa sanamu mbalimbali ambazo kwa kweli ilitakiwa iwe ni milango ya dharura. Hilo ni fundisho ambalo inabidi tulichukue kama nchi na kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nipongeze Serikali kwa mambo matatu. Kwanza katika ukurasa wa sita wa Bajeti ya Waziri wa Fedha, kuna taarifa kwamba misaada na mikopo kutoka nje mpaka Machi mwaka huu ilikuwa imetolewa asilimia 93. Kwa hiyo, hiyo nafikiri ni kwa mara ya kwanza, haijawahi kutokea kwamba tumekuwa tukipokea ripoti, hata ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ilikuwa inasema kwamba fedha za wafadhili zilikuwa hazifiki. Lakini mpaka Machi, tulikuwa tumepata asilimia 93. Nafikiri makubaliano ambayo yamefikiwa hivi karibuni kupitia *JUST* yamewezesha hali hii. Kwa hiyo, naamini kwamba hata miradi ambayo ilikuwa haitekelezwi kwa sababu ya kukosekana kwa fedha ya wafadhili itaanza kutekelezwa. Tunaamini kwamba sasa hivi asilimia hii itaongezeka kufikia asilimia 100 na ikiwezekana kuzidi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nipongeze Serikali kwamba imeongeza fedha kwenda mikoani mara mbili katika bajeti hii. Napenda niipongeze Serikali kwa ajili hiyo. Tunaposema *decentralization by devolution* ni kwamba sasa Serikali inatekeleza hilo kwa vitendo. Lakini sasa sambamba na hili tuweze kuboresha utendaji wa Mikoa

yetu na Halmashauri zetu ili fedha zinapokwenda huko zisiende kuishia kutokutumika vibaya ama kutokupata *value for money. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, napenda niipongeze Serikali kwa ubunifu wa kubadilisha mfumo wa kutoza ada za mwaka kwa magari, kwamba sasa katika *categories* tatu kwamba CC mpaka 1500, 1500 mpaka 5000 na zaidi ya 5000. Lakini napenda niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Gairo, kwamba watu wengi wa kipato cha chini wako *up to* CC 2000. Najua mtakuwa mmefanya hesabu kwamba magari ambayo yako mpaka CC 1500 yako mangapi na 1500 mpaka 5000 yako mangapi na kadhalika na kuweza kubaini kwamba chanzo hiki cha mapato kitaipa Serikali kiasi gani. Lakini nilikuwa naomba CC 1500 iongezwe iende mpaka 2000 kwa sababu watu wengi ambao wanahangaika kutafuta mapato kuweza kulisha familia zao na kutimiza mahitaji mbalimbali wako mpaka CC 2000. Naomba sana hilo Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilipoangalia kutoka 20,000 kwenda 80,000 kwa mwaka maana yake nini 80,000? 80,000 kwa mwaka maana yake ni shilingi 219 kwa siku. 230,000 ni shilingi 630 kwa siku na 100,000 kwa mwaka ni shilingi 274 kwa siku. Sasa hii kama mtu una gari lenye CC 5000 wewe siyo mtu mwenye matatizo na hela shilingi 630.

Lakini fedha hizi napongeza Serikali kwa sababu fedha zitakazopatikana kutokana na chanzo hiki cha kodi zitakwenda kuhudumia barabarani vijijini, barabarani mikoani, zitakwenda kutatua matatizo ya usafiri na kila Mbunge akisimama kilio kimojawapo ni barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni Magu barabara kutoka Makao Makuu ya Tarafa kwenda Makao Makuu ya Kata na kutoka Makao Makuu ya Kata kwenda kwenye vijiji na zinazounganisha vijiji na vijiji yamekufa na hazijajengwa muda mrefu sana. Ukiangalia Tarafa moja ya Ndagalu ukitoka Kabila kwenda Ntobola hakuna barabara. Utoke Ntobola kwenda Mahaha hakuna barabara na hali ni hiyo hiyo Majimbo yote nchi nzima. Kutoka Makao Makuu ya Kata kwenda kwenye vijiji kutoka Kijiji kwenda Kijiji ambako ndio kuna uzalishaji, naamini kwamba fedha hizi zitachangia sana kwenda kutatua matatizo ya kero za barabara katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hizi fedha zitakazopatikana zilikuwa hazitoshi. Ningependa ziongezwe zaidi kwenye barabara. Pamoja na hizi barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri, barabara za Mikoa zingetengenezwa na namshukuru sana Waziri wa Miundombinu kwamba ameangalia upya barabara na *category* zake zipi za Mikoa na kama zilikuwa za Mikoa zamani sasa hivi zinaweza zikawa *up-graded* kutoka Wilaya kwenda kuwa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuunganisha Wilaya kwa mfano hakuna barabara ya uhakika inayopitika mwaka mzima kutoka Wilaya ya Bariadi kupitia Magu kupitia Kwimba kwenda Maswa. Hizi Wilaya zinazalisha, zina uzalishaji mkubwa na unaweza ukakuta kuna upungufu wa chakula mahali kwa sababu tu barabara hazipitiki. Ukitoka Bariadi kuja Magu hakuna barabara ambayo inaunganisha moja kwa moja.

Labda hii ambayo itajengwa kupitia Lamadi, upite Lamadi ndiyo uje Magu lakini hiyo siyo ya mkato. Itafutwe njia ya mkato ambayo itapita Bariadi ije Kasoli ipite Magu, Lumeji ipite Kadashi iende mpaka Maswa. Nchi nzima barabara za namna hiyo zitafutwe ambazo zitaharakisha usafiri na usafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la barabara limekuwa ni kilio kikubwa na Serikali yetu tunajua ina masikio na inasikia barabara ya kutoka Dodoma kwenda Mwanza ikamilike. Ikiwezekana kwenye bajeti hii ikamilike. Barabara ya kutoka Babati kuja Dodoma ina tatizo gani kukamilika na kujengwa na kutengewa fedha kutoka Dodoma kwenda Iringa tuunganishe nchi hii na barabara kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha miaka 40 ya uhuru bado hatujaamua kufanya maamuzi ya msingi kama tulivyofanya maamuzi ya msingi kwenye Shule za Sekondari na tunajenga kila mahali MMEM, MMES, kwa nini hatuamui kutenga hela mara moja tunaamua kwenye makabrasha lakini fedha hazitengwi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali hii inatia aibu na Serikali ijue kwamba wananchi wanasubiri barabara hizi na wamefikia mahali wanachoka.

Barabara ya kutoka Kisesa pale Magu *by pass* kupitia Usagala kwenda Geita wenzangu wamelizungumza lakini naomba pia nisisitize kwamba barabara hii ni muhimu sana kama zilivyo barabara nyingine na naamini kwamba kilio cha Wabunge kuhusu barabara hii Kisesa, *by pass* Usagala Geita Serikali imesikia na kwa sababu Waziri wa Fedha ana madaraka ya kuhamisha fedha kutoka kifungu kimoja kwenda kingine ndani ya bajeti tunaamini Waziri wa Fedha atafanya hivyo. Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, tafadhali tusaidie kuweka fedha zaidi hiyo bilioni nne uliyotenga Usagala Geita, haitoshi. Ongeza fedha nyingi barabara iishe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamba, haipati ruzuku yoyote Serikalini. Tunaomba tusaidiwe Serikali iwaunge mkono wakulima kwa kuwapa ruzuku kwenye mbolea. Najua sasa hivi kuna ruzuku kwenye mbolea lakini wengi hawanunui mbolea ambayo ina ruzuku. Shida kubwa iko kwenye mbegu na kwenye madawa ya kuulia wadudu. Mkulima anatakiwa anyunyizie mpaka mara nne ili aweze kupata mavuno mazuri. Sasa hivi ananyunyizia mara moja/mbili. Tunaomba Serikali iliangalie hili na iongeze fedha huko kwenye pamba. Tunashukuru wenzetu wakulima wa kahawa wamepata mwaka huu bilioni 1.76 *STABEX COFFEE* lakini wakulima wa pamba hawana *STABEX* yoyote. Tunaomba hilo nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha amesema kwamba mahitaji jumla yalikuwa trilioni 12 zimepatikana trilioni sita. Hizi trilioni sita ambazo fedha zimekosekana tunafanyaje? Haikuwa miradi muhimu? Hayakuwa mahitaji muhimu? Sasa Serikali imechukua trilioni sita, trilioni nyingine tutafanyaje? Amesema Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha katika hotuba zao kwamba lazima tushirikishe sekta binafsi. Sekta binafsi zimeshirikishwaje? Sijaona mahali ambapo kuna mpango madhubuti wa kushirikisha sekta binafsi. Siyo tu katika maeneo haya ambayo

yameachwa lakini hasa kwenye miundombinu. Miundombinu inahitajika lakini miuondombinu bado inapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe mfano na nipongeze kwa kweli Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kimefanya ubunifu ambao ungeigwa sasa mahali pote tungeweza kufaidika na kuharakisha maendeleo ya nchi. Gharama ya Mlimani *City* ni shilingi bilioni 80. Sasa hivi wametekeleza robo ya mradi shilingi bilioni 25 lakini Chuo Kikuu wameshapata shilingi milioni 60 mpaka hivi sasa bila kutoa hata senti tano, wameshapata tayari. Mlimani *City* ile sasa hivi imebadilisha mazingira na itabadilisha mazingira pale.

Sasa *airport* ya Mwanza tunasubiri mpaka Serikali ipate fedha, *airport* ya Mbeya Songwe mpaka Serikali ndiyo itoe hela. *Airport* ina vitu vingine, ina maduka ina kila kitu. Ile Mlimani *City* tungeweza kuibadilisha kuwa *airport* kule *swimming pool* ukaweka uwanja wa ndege. Sasa kwa nini tunasubiri mpaka Serikali itoe hela kwa kila kitu? Sekta binafsi ina hela ambazo inatafuta mahali pa kuelekeza. Tukisubiri Serikali ifanye mambo yote nchi hii, itachukua muda mrefu sana kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Serikali iainishe maeneo hayo na kabisa ijipange na hata kuna viwanja vya ndege duniani siyo mara ya kwanza vimeshajengwa kwa fedha za sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wanafanya kazi kubwa waongezewe angalau shilingi 200,000 kwa mwezi. Hii posho wanayopewa sasa hivi hailingani na majukumu na kazi wanayofanya pamoja na kwamba kisheria kwamba wana kazi nyingine za kufanya. Lakini pamoja na kazi nyingine za kufanya, kazi wanayofanya ni kubwa. Naomba wafikiriwe waongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la awali, nashukuru Serikali Wizara ya Mipango imetoa sera ya Taifa ya idadi ya watu na wamesema kabisa kwamba kama tunaendelea kuzaana hivi, maendeleo na mambo yote tunayofanya ya kimaendeleo ya kuwaletea wananchi haitawezekana. Naomba sera hii itekelezwe. Sikuona kwenye bajeti kama kuna mahali ambapo pametajwa kwamba bajeti hii inatekeleza vipi sera ya idadi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho mijini yapunguzwe, maboresho ndani ya Serikali yapunguzwe. Kila mahali Wizara wamejenga nyumba mpya wameleta kompyuta, wameleta viti wamebadilisha, lakini mbona yanabadilika mjini tu kwenye Wizara, vijijini hakuna maboresho? Nafikiri sasa mpunguze, nasema hii ipunguze siyo isimamishwe, ipunguzwe kidogo ili maboresho nayo yaonekane vijijini ambako ndiyo kuna Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho bajeti hii ni nzuri, naamini kwamba ikisimamiwa vizuri, ikitekelezwa vizuri na tukapata thamani ya fedha hizi trilioni sita tuzione zimeingia na zimeleta mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba Serikali ya Awamu ya Nne, imejipanga vizuri sana na itatekeleza bajeti hii kwa ufanisi mkubwa na nina hakika kwamba baada ya mwaka huu wa fedha kwisha tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magu napenda kutamka kwamba naunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hii bajeti ya Wizara ya Fedha iliyowasilishwa mezani. Kwanza kabisa, naomba na mimi niungane na Watanzania wengine kutoa pole kwa wote waliohusika na msiba kutokana na ajali ya gari ilitokea pale Singida.

Vile vile naomba niungane na Watanzania wote kwa kuipongeza Timu ya Taifa kwa kufanya vizuri kule Burkina Faso. Lakini kutoka katika sakafu ya moyo wangu kabisa, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kutia msukumo mkubwa katika suala zima la michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha Zakia Meghji na Waziri wa Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Alhaj Dr. Ngasongwa na viongozi wote katika Wizara husika kwa hotuba nzuri zilizowasilishwa mezani ambazo zinajadiliwa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika Sekta ya Madini na muda ukiniruhusu nitachangia katika sekta ya pamba. Tanzania ni nchi ya nne Afrika kwa uwingi wa utajiri wa madini. Nchi nyingine ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afrika Kusini na Nigeria. Lakini pamoja na uwingi wa utajiri huu, mchango wa Sekta ya Madini katika pato letu la Taifa bado ni mdogo. Haulingani kabisa na utajiri tulionao.

Kwa mfano mwaka 2003 Sekta ya Madini ilichangia kwa asilimia tatu katika pato, mwaka 2004 asilimia 3.2, mwaka 2005 asilimia 3.4 na mwaka 2006 asilimia 3.7. Utaona ongezeko ni dogo sana, mchango bado haujawa mkubwa. Ijapokuwa kwa mwaka jana ongezeko ni kubwa kidogo na ni dhahiri kwamba ni kutokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM iliyoungwa mkono na Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na makabrasha mengi rasmi ya Serikali, lengo la Sekta ya Madini kuchangia katika pato la Taifa inatakiwa ifikie asilimia 10 ifikapo mwaka 2025. Kwa hiyo, ukiangalia mserereko huu inaonyesha kwamba kuna changamoto kubwa ili tufikie asilimia 10 mwaka 2025. Kwa kuzingatia mserereko huu wa takwimu, naomba nitoe ushauri kwa Serikali ambao unaweza ukasaidia kuongeza pato la Taifa kutoka katika Sekta ya Madini. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 Serikali iliahidi kwamba wachimbaji wadogo watasaidiwa kupata teknolojia, mikopo na masoko ili waweze kuchangia katika kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga na Wilaya ya Kishapu, tunao wachimbaji wadogo wa madini wapatao 20,000 na hasa katika Wilaya ya Kishapu katika

vijiji vya maganzo, Buchambi, Songwa, Idukilo, Utemini, Nyenze, Umbula, Seseko, Mipa, Mwigumbi, Steleja, Naseke kijiji kule nilikozalisha kuna wachimbaji wadogo wengi. Hawa wachimbaji wadogo wa almasi wanaweza kupata karate 20,000 kwa mwaka zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 14. Lakini pato hili au fedha hizi haziingii katika pato la Taifa kutokana na utaratibu ambao upo.

Wachimbaji wadogo hawa vile vile hawapati faida kwa sababu ya utaratibu wa ununuzi. Wanapata tu moja ya sita ya thamani ya almasi wanazoziuza. Tano kwa sita inakwenda kwa watu wengine. Kwa hiyo, hawa wachimbaji wadogo kwa ujumla hawaongezi pato la Serikali na wenyewe hawanufaiki. *(Makofi)*

Lakini ukiangalia uzalishaji au fedha zilizopatikana kutokana na uuzaji wa almasi kwa mwaka 2003, almasi zilizouzwa ziliingiza dola milioni 28.6. Mwaka 2004 ziliingiza dola milioni 26, mwaka 2005 ziliingiza dola milioni 24.4 na mwaka jana dola milioni 22.4. Kwa hiyo, ukiangalia wachimbaji wadogo kama wanaweza wakazalisha dola milioni 14 lakini haziingii katika pato la Taifa kama kutakuwa na utaratibu, wachimbaji wadogo wanaweza wakawa na mchango mkubwa katika kukuza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Septemba, 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa *De beers* ambayo inamiliki mgodi wa Mwadui walikutana *New York.* Pamoja na mambo mengine walikubaliana kuanzisha mpango ambao utawasaidia wachimbaji wadogo wa almasi katika Wilaya ya Kishapu. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, kwa kuamua kuchukua hatua hizi ambazo zitasaidia wachimbaji wadogo katika Wilaya ya Kishapu. *(Makofi)*

Lakini vile vile napenda kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini na Hususan Waziri Karamagi na Naibu wake Mheshimiwa Ngeleja wamekuwa karibu sana kuhakikisha kwamba yale waliyokubaliana na Mheshimiwa Rais wetu na Mwenyekiti wa *De beers* yaweze kutekelezwa ili wachimbaji wadogo waweze kuchangia katika pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya habari njema kwa Bunge lako Tukufu napenda kueleza kwamba mazungumzo kati ya Watalaam wa *De beers* Wizara ya Nishati na Madini, uongozi wa Mkoa wa Shinyanga na mimi mwenyewe *personally* tunaendelea katika mazungumzo kuhakikisha kwamba mpango ambao Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa *De beers* walikubaliana uweze kutekelezwa na kuwasaidia wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopenda kuomba, Serikali katika mazungumzo haya ambayo yanakaribia kutia kwamba wasimamie kwa karibu na kuweza kuhakikisha kwamba maslahi ya wachimbaji wadogo na wananchi kwa ujumla yanaweza kupatikana kama ilivyokusudiwa na kiongozi wetu Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ambalo linaweza kuchangia ambalo linaweza kuongeza pato la Taifa letu, ni kuhusu uchambuaji

wa almasi zinazouzwa nje kutoka katika mgodi wa Mwadui. Almasi hazichambuliwi kama karanga au njugu, choroko. Kuna utaratibu na vigezo kama 3000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachopenda kusema ni kwamba almasi za Mwadui zinakwenda kuuzwa katika soko la *London* chini ya Kampuni ya *DTC,* ni asilimia 15 tu zinachambuliwa, baadaye zinauzwa kwa bei wastani. Ni dhahiri kwamba Serikali inapoteza fedha nyingi. Kwa hiyo, naiomba Serikali pamoja na hatua za Wizara iliyokwishachukua ya ku-*train sorters* karibu kumi ya mwaka huu waongeze kuimarisha hicho kitengo cha *tansort* ambacho kinahusika na uchambuaji wa almasi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kushauri ni kuhusu mkataba wa mwaka 1994. Kulingana na mkataba huu ambao ni kati ya Serikali ya Tanzania pamoja na *De beers, De beers* wanamiliki asilimia 75 ya hisa katika mgodi huu, Tanzania asilimia 25 na almasi zinazouzwa nje lazima ziuzwe kupitia kampuni ya *DTC.* Ni kampuni tanzu ya *De beers.* Kwa hiyo, hapa kuna wingu la utata. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie mkataba huo katika majadiliano yanayoendelea.

Lakini la pili ninachoomba, asilimia 25 wakati ardhi ni yetu na almasi ni zetu, naomba tuangalie katika majadiliano yanayoendelea turekebishe na tufanye maamuzi wakati mwingine magumu. Kuna msemo unaosema *where there is no pain there is no gain, no gain no pain* na inasemekana vile vile kwamba wanyenyekevu watarithi kitu chochote hapa duniani, lakini siyo madini, kwenye madini kuna ubabe tu. Sasa tunatakiwa twende kujadiliana tukijua sisi tuna utajiri wao, hawana utajiri japokuwa wana teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nafasi zilizobaki, naomba kwa kasi kabisa tuchangie sekta ya pamba. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kampeni aliahidi kwamba CCM ikishinda itaunda Serikali. Suala la bei ya pamba atahaingaika nalo. Serikali ya Awamu ya Nne ilipoanza kazi imetoa agizo kwamba uzalishaji wa pamba upande kutoka kilo 300 mpaka 1000 katika ekari moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamba inalimwa na mikoa 13 na Wilaya 42 lakini kuna matatizo mengi ambayo yametajwa. Kwa mfano wakulima wanatumia jembe la mkono tu, miundombinu katika maeneo wanayolima pamba ni mibovu. Wakulima wanategemea mvua za msimu na bei ni ndogo. Ili ahadi ya Rais itekelezwe na agizo la Serikali la kupandisha uzalishaji kutoka kilo 300 mpaka 1000, napenda kushauri mambo yafuatayo na naomba kwanza tuelewe kwamba sisi tunazalisha asilimia 29 tu ukilinganisha na uzalishaji wa nchi nyingine. Ni uzalishaji mdogo sana. Wakulima wanaolima pamba wanalima katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitalinganisha wakulima wa pamba na mshumaa unaowaka. Mshumaa unaowaka unawaangazia wengine, wenyewe unateketea. Wakulima wa pamba kulingana na mazingira wanayolima na miundombinu mibovu na bei ndogo lakini pamba ni zao la pili katika kuliingizia Taifa pato kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 lilikuwa la kwanza lakini wenyewe wanateketea katika umaskini wakiwatajirisha wachache. Kwa hiyo, ni sawa na mshumaa, lakini kuna wakulima wa pamba 500,000 katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo kufuatana na muda uliobaki. Cha kwanza, naomba Bodi ya Pamba iliyotengewa fedha kidogo katika bajeti hii yafanyike marekebisho iongezewe la sivyo ahadi ya Rais na agizo la Serikali inaweza lisiweze kutekeleza. Chuo cha Ukiriguru ambacho kinafanya utafiti wa zao la pamba na chenyewe kinatengewa fedha kidogo kiongezewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki ni mdogo, naomba kuunga mkono hoja na kutoa sababu tatu tu za kuunga mkono.

Kwanza, naunga mkono bajeti hii kwa sababu imetekeleza ilani ya uchaguzi asilimia mia moja na ilani ya uchaguzi iliungwa mkono na Watanzania zaidi asilimia 90.

Pili, bajeti hii imegusa sekta ambazo zinawagusa Watanzania wote kutoka vijijini mpaka mijini na imegusa Sekta ya Elimu. Mara ya kwanza imepata fedha nyingi, imegusa Sekta ya afya ambayo inagusa wananchi wote na Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wanaosema kwamba haijagusa wananchi sijui wana maana gani. Lakini la mwisho na zuri sana ambalo sijawahi kuona na ninampongeza sana Waziri wa Fedha ni kuanza kujitegemea tusitegemee wahisani, baadaye wafadhili ambao hawatusaidii sana tukope. Hakuna mtu yeyote atakayetajirika bila ya kukopa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi mliyoifanya asubuhi hii. Tukirudi mchana tutaanza na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Elizabeth Batenga na wengine wajiandae. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**Hoja za Serikali**

**Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji**

*(Majadiriano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Natamwita Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindaka, simwoni; Mheshimiwa Juma Killimbah, hayupo; Mheshimiwa Raphael Chegeni, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Lyimo halafu Mheshimiwa Elizabeth Batenga ajiandae.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti. Kwanza, awali ya yote, naomba niseme kwamba napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na Mheshimiwa Waziri wa fedha kwa kuweza kuandaa Bajeti ambayo mimi nasema *is an obviously budget*. Ni bajeti ambayo ni ya kufunga mkanda na ni ya kuambizana ukweli. Kabla sijakwenda mbele zaidi, naomba nithibitishe kwamba naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi wachangiaji wengine wamesemaje, lakini naamini kabisa kwamba mtazamo mzima wa Watanzania na sisi tuliomo ndani ya Bunge hili tunaunga mkono kabisa kwamba Bajeti hii imeandaliwa kinamna yake na ndiyo maana imeleta mtikisiko mkubwa sana. Katika kuandaa Bajeti hii, nadhani wote tunaungana au tunakubaliana kwamba Bajeti hii imewekwa katika misingi mikuu mitano. Wa Kwanza ni kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, hiyo haina ubishi. Pili, ni Mpango wa Taifa wa maendeleo na tatu imezingatia masuala ya MKUKUTA na nne imeangalia masuala mazima ya mambo ya Malengo ya Milenia na tano imeangalia mfumo mzima wa Uchumi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sielewi! Kila mmoja ana tafsiri yake katika Bajeti. Lakini Bajeti hii *is an incremental budget. Incremental budget* maana yake ni kwamba unakuwa kila mwaka unaongeza Bajeti yako kulingana na mahitaji uliyonayo. Sasa haiwezekani kuruka kutoka kwenye hatua moja kwenda kwenye hatua kumi kwa mara moja wakati unajua kabisa kwamba *resources* zako ziko vile vile *accountable*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema *it can be done, play your part* kwa maana ya kwamba inawezekana iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake. Sasa kupitia Bajeti hii, napenda niseme kwamba Bajeti hii kwa kweli mimi binafsi nasema kwamba imengalia mambo mbalimbali. Kwanza ukiona kwenye Bajeti hii kuna suala la uendeshaji wa Serikali, tunaona ndiyo imepanda lakini Serikali imekuwa na watu, tumeongezeka na nchi yetu ni kubwa. *There is no way* kukwepa hizi gharama za uendeshaji wa Serikali.

Lakini pili huwezi kuendesha miradi ya maendeleo kwa kutegemea bajeti hii peke yake. Kuna haja ya kuangalia mpango mbadala kwamba masuala ya miundombinu, masuala ya kilimo yanapewa mtazamo tofauti, *may be complementary budget* ambayo inakuwa na mtazamo wake. Tukianza kubanana kwenye bajeti ya kila mwaka hapa hatuwezi kupiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ambacho ningepaswa kushauri ni kwamba kwa mfano sasa hivi tumekuwa tukielezwa kwamba kumekuwa na *excess liquidity* katika nchi yetu na mfumo mzima wa *financial system* hapa nchini. Lakini *excess liquidity* hii inaweza ikatumika tu iwapo tunaweza tukaitumia sisi wenyewe kwa kutumia *financial*

*instruments*. Tuka *mop-up* hizo fedha na tuka-*invest* katika miradi kama hii ya ujenzi wa barabara na ujenzi wa miundombinu na kuboresha kilimo kwa urahisi zaidi. Lakini tukitegemea tupate pesa kwa ajili ya kilimo kutokana na Bajeti hii na pesa ya miundombinu kutokana na Bajeti hii tutakuwa tunajidanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba, Bajeti hii ni lazima iwe na mfumo ambao unaitwa *trickledown effect*. Ile *macroeconomics* iweze ku-*reflect microeconomics*. *The trickledown effect* inapokuwepo na ndiyo maana Mtanzania ukimwambia kwamba uchumi umepanda ataelewa kwamba umepanda. Leo ukisema kwamba bajeti hii inamlenga mtu huyu kumwondolea umasikini kweli kunakuwa na *impact* yake. Lakini bila kuwa na hayo, bado inakuwa ni tatizo.

Ukiangalia uchumi wetu unategema sana suala la ku-*export traditional goods* au kuuza nje yale mazao yetu asilia. Muda umefika, sasa tubadilike. Lazima tuanze kuuza na huduma. Tuuze *services* ambayo hata ukiangalia kwenye baadhi ya sekta ambazo zime-*perform* pamoja na *service sector* ime-*perform* sana. Lazima tuanze kwenye mambo ya *services* ili tuweze kuuza na kuweza kupata fedha nyingi kama Taifa. Bado tuna tatizo moja la kutokuwa na *road map*.

Suala la kipaumbele nadhani Mheshimiwa Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji hakuliainisha vizuri sana. Mipango yetu unapaswa tuwe tunakubaliana kwamba mwaka hadi mwaka tunapaswa tufanye nini. Kama ni kilomita tano za lami, basi lazima tujenge kilomita tano za lami kwa mwaka huu tumalize mwaka kesho tufanye kitu kingine.

Tunapoanza kupangiliana namna hii inatupa shida sana na ndiyo maana leo hii ukisema kwamba tumejenga kilometa ngapi kwa kipindi cha mwaka mzima uliopita, bado inakuwa vigumu kuweza kuelezea. Nakumbuka Mheshimiwa Mramba aliulizwa na Waziri Mkuu ile barabara ya Sam Nujoma akasema itakwisha Novemba. Lakini mpaka leo hii barabara haijaisha, tupo mwezi wa sita sasa hivi, lakini kwa sababu unakuta kwamba pengine fedha hazikutosha kuweza kufanya ile kazi. Sasa haya ni mambo ambayo lazima tujaribu kuyangalia tuwe na vipaumbele, vitasaidia kuijenga nchi. Bila kuwa na vipaumbele itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *TRA* wanakusanya sana fedha. Napenda kuwapongeza sana ndugu zetu wa *TRA*. Kama ni Taasisi ambayo imefanya kazi nzuri ni pamoja na *TRA*. Wamekusanya mapato vizuri sana. Sasa tatizo ni kwamba, makusanyo ya mapato yakiwa makubwa, matumizi yake yanakuaje? Hiyo ndiyo lazima tupeane mkakati hapa kwamba iweje leo matumizi ya Serikali yawe yana matatizo? Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesema kwenye Ripoti zake. Lakini ningependa kupitia Bajeti hii, hili suala tuliache kwa sababu haina maana, kuna baadhi ya Halmashauri hapa kwa sababu hazikupata hati safi zikapata hati chafu wakanyimwa fedha za maendeleo. Hivi kweli huyu mwananchi ambaye hajui hata maana ya hati chafu akanyimwa fedha za maendeleo, hujamsaidia hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Wilaya yangu ya Magu tulipata hati chafu, lakini baadaye tukaambiwa kwamba hatukupata fedha za maendeleo milioni zaidi ya 900. Sasa milioni 900 ingekwenda Kijijini kule, ina maana wale Wasukuma wote wa Busega wa Jimbo la Magu wangeweza kupata maendeleo kwa urahisi zaidi. Lakini wameyakosa kwa sababu aidha Mkurugenzi au Mtendaji katika Ofisi ile hakutimiza wajibu wake na tatizo kubwa lilikuwa ni kwamba hawakuthamini majengo inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unawakosesha wananchi shilingi milioni 900 za maendeleo, pengine kwa sababu majengo hayakuthaminiwa vizuri au kasoro ndogo ya kihasibu. Naomba hilo tujaribu kuliangalia. Kingine katika suala zima hili la kupunguza gharama ya uendeshaji wa Serikali, mimi nashauri sana suala zima ambalo limejiuhusisha sasa hivi ni suala ambalo watu wanalalamika. Hata mimi nalalamika kwa sababu nimepigiwa simu na wapiga kura wanasema kama tumekuchagua kweli kuja Bungeni tunaomba upinge Bajeti hiyo. Kipengele kikubwa ni kwamba mmepandisha bei ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukipandisha bei ya mafuta ambayo inahusisha bidhaa mbalimbali lazima ume-*affect the entire equilibrium* ya *economics*. Ina maana kwamba, uchumi sasa bado utakuwa ni tete. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili suala aliangalie na napendekeza kwamba hivi kwanini sasa *TPDC* tusiipe uwezo ili iweze kuagiza mafuta yote na yasambazwe hapa nchini kuliko hali ilivyo sasa? Kwa sababu hawa wa vituo vya mafuta wanapanga bei zao, matokeo yake bei zinapanda kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala tuliangalie na ningeomba kupitia Bajeti hii Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili suala la kupandisha bei ya mafuta alingalie. Tunaomba kwa kweli ujaribu kuondoa hilo ongezeko la kodi kwenye mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ni cha msingi sana na napenda kukizungumzia hapa ni suala zima la mfumo wa biashara ya ushindani. Lazima ifikie mahali sasa tujue kwamba sisi kama nchi tuna wafanyabiashara ambao wanafanya biashara ya ushindani na nchi iwasaidie kufanya biashara zao. Haiwezekani leo hii umemu-*expose* Mtanzania katika *International Trade* ambazo *competition* zake hauwezi ku-*match* nazo. Ningeomba sana hili suala tujaribu kuliangalia.

Lakini kingine ambacho ningependa kusema haraka pamoja na yote, chondechonde suala la barabara. Barabara ni tatizo, lazima tuongeze fedha kwa ajili ya miundombinu. Haiwezekani miaka yote nenda rudi barabara ya kwenda Kanda ya Ziwa haishi, Singida hakukamiliki, kwenda Kigoma hakupitiki, kutoka Dodoma kwenda Arusha hakuendeki, kutoka Dodoma kwenda Iringa hakuendeki na kusini baadhi ya maeneo bado hakupitiki. Huwezi ukafanikiwa katika uchumi kama miundombinu hii haijaboreshwa. Ninaamini miundombinu pamoja na ile *feder roads* kwa sababu yote inachangia katika kusafirisha bidhaa mbalimbali kwa ajili ya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba sana kwa msisitizo. Haiwezekani mwananchi wa Meatu, Bariadi kupitia sehemu za Ramadi uende sehemu za Ngasamo hata kule Rorya kwa akina Profesa Sarungi kule wanahitaji barabara wasafirishe bidhaa

zao kama inavyotakiwa. Bila kufanya hivyo ni ndoto. Tutakuwa tunabanana hapa, Bajeti haitoshi, gharama zinaongezeka na hatupati fedha za kuweza kuendesha Serikali. Kingine ni suala la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamba haipati ruzuku ya kutosha. Hivi mkulima wa pamba ana makosa gani katika nchi hii? Wengine mazao yao wanapata ruzuku ya mbolea na ruzuku nyingine mbalimbali. Mkulima wa pamba siku zote sasa hivi anasema kwamba gharama ya kuzalisha kilo moja ya pamba ni zaidi ya Sh. 250/= anauza kwa Sh. 210/= au Sh. 220/=. Hivi inaingia wapi akilini, huyu mkulima aweze kufanya biashara ya kulima pamba? Lakini tunahitaji tulime pamba na licha ya kulima pamba hawa watu ni lazima tuwafundishe namna ya kutunza pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamba hii mwaka jana tu katika Mkutano wa Nyanza tulisomewa kwamba zaidi ya marobota 1000 yalikataliwa kwamba yalikuwa ni marobota chafu. Hii ni hasara kubwa kwa nchi, lakini ni kwa sababu gani? Kwa sababu tumejikuta kwamba hawa wakulima wameanza nao kuwa wajanja wanachofanya siku hizi wakilima pamba wanaweka magadi wakati wa kuuza. Magadi yakikaa kwenye pamba, baada ya muda pamba inaharibika. Hii ni hasara kwa nchi. Ninachoomba sana, hizi *control measures* zifanyike ili kuwasaidia hawa watu. Tuwape bei ambazo zinaridhisha katika kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, tumeona kabisa kwamba katika suala zima hili la uchumi, bado tunahitaji Balozi zetu tuzibadilishe. Zamani Balozi zetu tulikuwa tunapeleka watu Ubalozini watu wenye mambo ya *Intelligence*, wanajeshi na kadhalika. Hizi siasa zimeshapita, tupeleke vijana wachumi waweze kusimamia Balozi zetu na wasaidie kuiunganisha nchi yetu na nchi mbalimbali ili tuweze kweli ku-*attract* wawekezaji na kuweza kuitangaza nchi yetu inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja zote hizi, napenda kuunga mkono kwamba mimi binafsi ninakiri kabisa kwamba Bajeti hii imejaribu kuzingatia mambo mengine yafuatayo:-

Makusanyo mapato ya ndani ya nchi yameongezeka, hili halina ubishi. Ndugu zangu wengine wanasema kwamba tuuze ndege ya Rais. Sasa ukiuza ndege ya Rais mwaka kesho utauza nini? Utauza tena kitu kingine mwaka kesho kutwa utafanya nini kingine? Suala sio kuuza ndege ya Rais, suala ni kuja na mpango mbadala ambao kweli unasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, kwanza naomba nimpongeze sana Kiongozi wa Upinzani kwa Hotuba yake nzuri na ile pia ya Waziri Kivuli wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie mambo machache, lakini hasa nitaanza kuzungumza kwamba mimi sitaunga mkono hoja hii kwa sababu kuu nne. Kwanza, Bajeti hii ina-mapungufu makubwa. Moja, imeshindwa kabisa kujikita kwenye *microeconomy* na imekwenda zaidi kwenye *microeconomy* kwa maana ya kwamba haijamuangalia mkulima wala mwananchi wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba Bajeti hii imejikita zaidi na imekuwa tegemezi hasa kwa nje hasa tukizingatia kwamba asilimia 40 ya Bajeti inatoka nje ya nchi. Kwa hiyo, ninashangaa kama ikitokea kuna tatizo, hizo nchi wafadhili je, Tanzania itategemea kitu gani? Lakini la tatu ni kwamba imeshindwa kuibua vyanzo vya mapato wakati vipo na ninaamini wakati Waziri wa Fedha atakapokuwa anajibu atatuambia ni kwa kiasi gani basi atachukua yale ambayo Kiongozi wa Upinzani aliyoyasema ambayo kwa kweli tunadhani ameibua vyanzo vingi sana vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kwamba Bajeti hii itachochea mfumko wa bei. Kwanini nasema hivi? Nasema hivi kwa sababu kuu mbili. Kwanza kupanda kwa bidhaa za mafuta. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea na hata aliyesema sasa hivi amesema wananchi wake walimwambia akija akatae Bajeti, lakini ameiunga mkono.

Kwa hiyo, nadhani wengi hapa tumekuja, tumechaguliwa au tumeteuliwa na hivyo wananchi tunaowawakilisha wengi ni wa kipato cha chini na ninaamini wengi hawatakubaliana na hii Bajeti. Kwa hiyo, sisi Wabunge tunaendelea kuwawakilisha na ndiyo sababu nasimama hapa kusema kwamba sitaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la kupanda kwa bei za mafuta. Itaeleweka wazi kwamba mafuta ndiyo uhai wa Mtanzania *weather* ni tajiti au maskini. Kupanda kwa bei ya mafuta athari yake kisera inajulikana lakini pia tukiangalia wananchi wengi wanategemea sio tu kusafiri kwa mabasi, lakini pia kusafirisha mazao yao.

Kwa hiyo, basi kama bei za mafuta zinapanda utakubaliana nami kwamba wananchi sio tu kwamba watashindwa kusafiri, lakini pia watashindwa kununua bidhaa kwa sababu bidhaa hizo zitakuwa na gharama kubwa kwa kuwa zimesafirishwa na usafiri ambao umepanda bei. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie vyanzo vingine na aache kupandisha bei za mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, kila siku hapa Bungeni tumekuwa tukiambiwa ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nakubaliana nayo kwa sababu ndiyo chama kinachotawala na bahati nzuri sana nimekuja nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na ahadi nyingi na ahadi hii inatolewa na kiongozi wa nchi kwa mfano, "Maisha Bora kwa kila Mtanzania." Tukiangalia ilani ya CCM ni kweli inasema hivyo, lakini tunapoangalia hii Bajeti na tuka-*reflect* na maisha bora kwa Watanzania tunaona kuna *contradiction* kubwa sana.

Nikisoma hii ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 164, naomba ninukuu, inasema kwamba: "Kuongoza ni kuonyesha njia na kuwa Mfano bora ni kuwafanya wananchi waridhike kukuona uko mbele na wao wanafuata. Wanakufuata si kwa sababu wanakuogopa ni kwa sababu wanakuamini na imani ya kweli haitapatikana kwa kauli tu bali hasa kwa vitendo mwelekeo na kuwajali wananchi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya maneno yamesemwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na wala sio Profesa Lipumba wala sio Mheshimiwa Mbowe.

Kwa hiyo, kama nia ni kuwajali wananchi, nilikuwa naomba basi hii Bajeti kweli iwajali wananchi. Kwa hiyo, kunukuu kwangu hapa nilikuwa naeleza kama kweli hii ilani ya Chama cha Mapinduzi ndiyo tunaifuata, basi ninaomba na matendo pia yawe hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala zima la kilimo. Nakumbuka mwaka jana katika Bajeti iliyopita tuliongelea sana suala la kilimo na tukasema kwamba kilimo kipewe kipaumbele na kweli kikapewa kipaumbele. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba hatujaambiwa kilimo kimefaidika kiasi gani mpaka sasa hivi, kimeshushwa na kupewa asilimia 6.2 tu ya Bajeti wakati katika nchi za *SADC* ilikubalika kwamba angalau Sekta ya Kilimo ipate asilimia 10. Kwanini Tanzania tunaipa asilimia 6.2 huku tukijua kabisa ziada ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na ndiyo sekta peke yake ambayo inatoa ajira nyingi kwa Watanzania, kwanini tunaamua kufanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia itakumbukwa kwamba miaka ya nyuma tuliweza kuwa na kilimo cha umwagiliaji hekta 450,000, lakini kwa sasa hivi zimeshuka mpaka 250,000 wakati kila siku kukiwa na ukame tunakwenda kuhemea nchi za nje. Kwanini tusiendelee kukipa kipaumbele kilimo ambacho Wabunge tulikubaliana kwamba ndiyo sekta muhimu ambayo inaweza kutoa ajira na ukiangalia kwenye Ilani ya CCM pia wameongelea kuhusu ajira 1,000,000. Sasa tunaomba kujua, kwanini Ilani ipo lakini bado utekelezaji unakuwa ni tofauti?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee tena katika suala zima la uchumi. Wataalam wanasema kwamba iwapo tunaweza kufanya kilimo kikue kwa asilimia kumi kwa miaka mitatu mfululizo, basi umaskini utapungua kwa asilimia 50. Lakini bado hilo halijafanyika na hata tukisoma katika Ilani, narudia tena maana yake ndiyo imekuwa inatumika sana hapa ukurasa wa 163. Kwa ridhaa yako, naomba niisome. Ukurasa huu unazungumzia kuhusu kilimo na unasema hivi: "Viongozi wavivu, wababaishaji na wanaotosheka na hali duni ya maisha ni kipingamizi cha mapambano hayo. Kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa. Viongozi ambao hawatekelezi Kanuni za kilimo cha kisasa katika mashamba sio chachu ya mapinduzi katika jamii."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa tunasema kwamba ni lazima tuwe na *Agriculture Revolution,* lakini haya yamezungumzwa hapa lakini sasa hivi haitekelezwi. Bado nazungumzia ile asilimia 6.2 ambayo kwa mantiki yoyote ile kilimo cha Tanzania hakitaweza kuwa cha kisasa. Kwa hiyo, tunaomba Waziri aliangalie hilo ili aweze kuwasaidia wananchi ambao asilimia 80 ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la mazingira na Bajeti iliyopo. Viongozi wetu kwa hali na mali wamekuwa wakizunguka nchi nzima kuzungumzia suala la mazingira. Mimi nakubaliana nao *hundred percent*. Lakini sasa hivi kwa kupanda kwa bei za mafuta ni kwamba wakulima na wananchi wa kawaida wanategemea zaidi mafuta ya taa, si tu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, lakini pia kwa shughuli mbalimbali. Kwa mfano jana wavuvi wadogo wadogo wanatumia mafuta ya taa kwa ajili ya zile boti zao. Sasa suala hapa kuna watu wanasema mafuta ya taa yanapanda bei ili wafanyabiashara wasiweze kuchanganya na *diesel*. Lakini hapa hatumkomoi mfanyabiasha tunamkomoa mwananchi wa kawaida. Kwa hiyo, naomba suala hilo pia liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niende kwenye suala la matumizi. Ni kweli Serikali kwa awamu zote tumekuwa tunaambiwa tukaze mikanda, tumeikaza sana. Lakini Kambi ya Upinzani tuliwahi kusema, Serikali imekuwa na Baraza kubwa sana la Mawaziri na tukaambiwa kwamba Baraza hilo ukubwa wake ni kwa sababu ya ufanisi. Sisi hatukatai, lakini wananchi wangefurahi sana pale wakiona kwamba Serikali nayo inakaza mikanda. Kama tutakuwa tunawaachia wananchi tu hapo tutakuwa tunafanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano mdogo. Nchi ya Ufaransa ambayo ni nchi tajiri sana, dunia yenye watu zaidi ya milioni 64, sasa hivi Baraza lao la Mawaziri, ni Mawaziri 15 tu. Kwanini Tanzania tushindwe na hao ndiyo wanaotupa misaada? Sasa hivi tunaambiwa Serikali Kuu inatumia zaidi ya shilingi trilioni 3.8 karibu trilioni nne. Lakini fedha za maendeleo ni shilingi trilioni mbili. Je, hatuoni uwiano huu ni mkubwa sana? Kwanini Serikali isikaze mikanda na yenyewe? Maana yake wananchi wakiona Serikali imekaza mikanda na hakika wao wataikaza zaidi hata ikatike. Kwa hiyo, ninaomba hilo pia liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililotaka kuchangia ni kuhusu ushuru wa magari. Katika ukurasa wa 56 wa hotuba ya Waziri wa Fedha ameongelea suala la kushusha ushuru kutoka asilimia 25 mpaka kwa asilimia 10 kwa mabasi yanayokwenda kasi, lakini si kwa mabasi mengine. Utakumbuka kwamba tumeliongelea sana suala la ajali na tukaambiwa takwimu zinatolewa na tafiti hizi zimefanywa kwamba ajali nyingi zinazotokana na mabasi ni kwamba mabasi hayo ni malori. Lakini sioni ni hatua gani inachukua ili wapunguze ushuru wa mabasi yale ambayo kweli ni mabasi na si malori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekaa kimya na hapa hawajaonyesha chochote, wameongelea tu kuhusu mabasi yanayokwenda kasi. Je, mabasi mengine tutaendelea kuzika watu wetu hadi lini? Kwa sababu tunawazika wa UKIMWI, tunawazika wa Malaria sasa tena na ajali ambazo kabisa Serikali inaweza ikazuia. Nilitegemea kabisa wakati tumeelezwa hili, basi Serikali ingefanya juhudi ama kuweka *governors* kwenye haya mabasi ambayo ni malori ama kupunguza ushuru ili wafanyabiashara wa mabasi waweze kuleta mabasi na sio malori au vinginevyo wapandishe ushuru kwa malori ili washindwe kufanya hiyo biashara kichaa ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuliongelea ni suala zima la Elimu. Labda hapa niipongeze Serikali kwa kuweza kuweka Bajeti nzuri ya Elimu ambayo kwa sasa inaongoza, ni shilingi trilioni moja. Lakini Bajeti hii ni kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo, lakini sijaelewa Elimu ya Juu imepewa kiasi gani? Kwa sababu kusaidia sana huku chini elimu ya Sekondari na Vyuo vya Ualimu halafu ukaacha Elimu ya Juu maana yake ni kwamba huku juu kutakuwa na matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kwamba hii Bajeti ya Elimu na ile ya Elimu ya Juu angalau zingekwenda sambamba ili huku juu wanafunzi wasiwe na matatizo ya kugoma na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la Miundombinu. Jana wakati Waziri Kivuli wa Uchumi anazungumza, alisema kwamba, kwa mwaka mzima Serikali haijajenga hata kilomita moja ya lami. Sasa mimi nikajaribu kuangalia na kuuliza, nikaambiwa ni kweli. Sasa mimi naomba kujua.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 50. Naomba Mheshimiwa Mbunge atoe ufafanuzi anachomaanisha kwa sababu anachosema ni kwamba Serikali haikujenga hata kilomita moja. Sio kweli. Akanushe *statement* yake.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika ni kweli na kitabu cha hali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, Naibu Spika ndiyo ameombwa utaratibu. Kwa hiyo nataka ufafanue.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba, jana wakati Waziri Kivuli akizungumza alisema hivyo na hiyo ipo katika Taarifa ya Hali ya Uchumi na kama anataka nitaweza kumletea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kilichosemwa ni kwamba Serikali haikujenga barabara mpya. Yeye anachosema Serikali haikujenga hata kilomita moja! Tumeendelea kumalizia barabara zilizokuwa zikianza na tumejenga kilomita nyingi sana! Naomba afute *statement* yake!

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kukarabati na kujenga…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, tulia kwanza. Ukipigwa *point of order,* ni kwamba yule aliyepiga *point of order* anaomba *guidance* ya Spika, kwa hiyo, wewe unakaa chini mpaka Spika, mwenyewe atakuambia, ama anakubaliana na hiyo ama anaweza kusema endelea. Lakini, sasa naomba utoe ufafanuzi kwamba ni kweli kuwa hata kilomita moja haijajengwa!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, tulia kwanza. Ukipigwa *point of order* ni kwamba yule aliyepiga *point of order* anaomba *guidance* ya Spika. Kwa hiyo, wewe unakaa chini mpaka Spika mwenyewe atakuambia, ama anakubaliana na hiyo, ama anaweza kusema endelea. Lakini, sasa naomba utoe ufafanuzi kwamba ni kweli kuwa hata kilomita moja haijajengwa!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli na naomba nitoe tofauti. Nimesema kujenga na sikusema kukarabati. Nilichokisema ni hicho hicho. Kujenga mpya na kukarabati ni vitu viwili tofauti na mimi ninachokizungumzia ni kwamba Serikali haijajenga hata kilomita moja mpya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Miundombinu, kweli haujajenga hata kilomita moja? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna usemi kwamba: "Akutukanaye, hakuchagulii tusi."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa ya Bunge hili, ni vizuri viongozi tunaposimama kutoa kauli zetu tuwe na uhakika wa hayo ambayo tunayasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Nne ichukue madaraka ya nchi hii na katika huu mwaka wa fedha ambao tunauongelea na kwa taarifa ambazo tumetoa humu Bungeni kwa miradi inayoendelea ya ujenzi wa barabara, tumejenga kwa upande wa barabara kuu zaidi ya kilomita 285. Kwa barabara za Mkoa tumesema tumejenga Kilomita 15 na ushee na tunaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, siyo sahihi katika kipindi hiki hakuna hata eti hata kilomita moja iliyojengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika. nakushukuru sana. *(Makosa)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Utaratibu wa mwanzo sijamaliza! Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunatafuta kubishana bila sababu. Kwa sababu tukisema *obviously* kwamba hakuna hata kilomita moja iliyojengwa, hii sio kweli. Kwa hiyo, mimi na-*rule out* kwamba Mheshimiwa Susan endelea kuzungumza. Lakini, kusema hakuna kilomita hata moja iliyojengwa, sio kweli. Kwa hiyo, naomba uendelee Mheshimiwa Susan.

**MBUNGE FULANI:** Afute usemi!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kuhusu utaratibu!

**NAIBU SPIKA:** Kwanza, Mheshimiwa Susan futa usemi!

**MBUNGE FULANI:** Usifute!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Kumalizia hoja yangu!

**NAIBU SPIKA:** Kwamba hakuna barabara hata moja iliyojengwa, kwa sababu sasa waki-*prove* unafanyaje?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Waziri wa Ujenzi anasema na kwa sababu katika kitabu nilichokisoma inasema tofauti, nadhani sitafuta usemi labda nilete kilichosemwa kwenye taarifa ya uchumi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA:** Aha! Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 55, ni marufuku kwa Mbunge yeyote kusema uongo Bungeni ikiwemo Waziri. Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ametoka kuzungumza hapa sasa hivi kwamba toka Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani imejenga jumla ya kilomita 200 na ushee za barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Miundombinu athibitishe kwa sababu kwa mujibu wa kitabu cha taarifa ya hali ya uchumi wa nchi, toka Serikali ya Awamu ya Nne imeingia madarakani, imekarabati kilomita 9000 za barabara kuu na imekarabati kilomita 18,000 za barabara za Mikoa. Kitabu kizima hakina taarifa ya barabara hata moja ambayo Serikali ya Awamu ya Nne imejenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba ama Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu alithibitishie Bunge hili kwamba kuna Barabara hata moja ambayo imejengwa mpya tofauti na kukarabati, au afute usemi wake!

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza usemi wangu. Mimi ndiye mwenye dhamana ya Hekta ya Miundombinu na tunaposafiri barabara kutoka Mbwemkulu kwenda Lindi – Mingoyo, tumejenga kwa kiwango cha lami na siyo kukarabati. Ukitoka Kamiyolwa kuelekea upande wa Geita, tunajenga kwa kiwango cha lami, na siyo kukarabati. Ukitoka Dodoma kuelekea Manyoni, tunajenga kwa kiwango cha lami na siyo kukarabati. Ukitoka Singida kuelekea Isuna, tunajenga kwa kiwango cha lami na siyo kukarabati na ninaweza kuendelea *on and on*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri hawa viongozi wakaelewa mazuri ambayo yanafanywa na Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi/Kigelegele)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Kanuni hizi hizi, kuna Kanuni inayosema sio vizuri kupeleka Bunge kuanza kubishana kuhusu mambo yaliyo wazi. Halafu pia, pamoja na hiyo taarifa mnayosema, Serikali hii ni *on going*, ni Serikali inayoendelea. Kwa hiyo, ukisema kuna *cut frame*, unaanzia Serikali hii, unaanzia hapa, nadhani ni tafsiri mbovu. Kwa hiyo, mimi naomba tuendelee tu na mjadala, hili swali limefungwa. Mheshimiwa Susan una dakika mbili tu.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuendelea kunipa muda. Naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala zima la vyanzo vya mapato. Kama nilivyoanza kusema, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliongelea vyanzo vingi vya mapato. Lakini, tumekuwa tunaona kwamba bajeti kila mwaka tumekuwa tunapandisha sigara, bia, mpaka yaani imekuwa ni mazoea. Kwa hiyo, mimi nilikuwa ninashauri na kuomba sana Serikali kweli iweze kuangalia vyanzo vipya vya mapato ambavyo kwa kiasi kikubwa kitawapunguzia makali ya maisha wananchi wa kawaida ambao hata mlo mmoja kwa wengine ni mgumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ieleweke kwamba tumekuwa na mikakati mizuri sana ya Elimu, hilo nimelizungumzia na naendelea kulizungumza. Lakini, kwa mwananchi wa kawaida ambaye anaweza walau kumsomesha mtoto wake shule ya msingi, shule za kawaida, kwa hali hii mtoto huyu atashindwa kusoma kwa sababu yule mzazi atashindwa kwenda kufanya biashara ndogo ndogo mbali kutokana na nauli kupanda, lakini pia kusafirisha zile bidhaa zake za kuchuuza. Lakini, hata wale watakaoweza kufika Darasa la Saba wakafaulu, tatizo litakuwa pale pale kwa sababu tunajua kwamba watoto wengi hasa wa kike, wanaosoma shule za Sekondari za kutwa, nyumba usiku ndio muda wao kwa sababu wanapofika nyumbani wanafanya kwanza kazi za nyumbani, kukata majani na kazi zingine. Kwa hiyo, muda wao pekee wa kujifunza ni usiku na usiku watoto hao mpende msipende wanatumia vibatari na vibatari vinatumia mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakishindwa hata kusoma kwa vibatari, tunapata watoto wa namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kwamba hata hao watakaofanya vizuri, watakwenda Vyuo Vikuu, lakini Vyuo Vikuu bado watakutana na asilimia 40 ambayo itabidi mzazi yule yule ambaye ni wa kipato cha chini ashindwe kumsomesha mtoto wake wakati tunasema tunataka wanafunzi wetu wasome.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano, tumeona ni jinsi gani wanafunzi wetu katika masuala ya elimu wamekuwa wakifanya vizuri, lakini wakifika Vyuo vya Juu, kulikuwa na haya mashindano ya Juzi yaliyokuwa yanafanywa na *CELTEL*, tumeona ni jinsi gani Tanzania ime-*perform* vibaya kwa sababu ya mazingira mabovu. Lakini sasa kama huku chini hatujawapa msingi, wanasomea vibatari, lakini hata vibatari tunawanyang'anya, sio haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na kama nilivyosema sitaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja hizi mbili zilizowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa niwapongeze sana kwa namna walivyoziwasilisha, hata kwa namna zilivyoandaliwa vizuri, zinaeleweka sana na sisi tunapenda kuwapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli mbiu ya maisha bora kwa kila Mtanzania au dhamira, ni dhamira ambayo ni thabiti na ambayo ni matarajio kwamba wote tunalenga huko kwa maisha bora ya kila Mtanzania. Lakini sidhani kwamba tutalala, tuamke kesho asubuhi tuseme Mtanzania au Watanzania wote wamepata maisha bora kwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata maisha bora kwa kila Mtanzania, tunahitaji nguvu ya pamoja, tunahitaji mshikamano, tunahitaji nguvu ya pamoja, kwa kweli na kushirikiana vizuri ili tuweze kumsaidia mwananchi wa Tanzania aweze kupata maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kama hapa sisi Wabunge tutajigawa makundi tuanze kusema kwamba tunapinga bajeti, wanasema hatuungi mkono bajeti. Katiba ya nchi inasema, kama Bunge zima tungeamua kukataa bajeti, basi tunajiuzuru wote pamoja na Rais wetu, tunaingia uchaguzi. Sasa wenzetu wanapopinga bajeti, sijui wanajipa adhabu gani! Basi wajiuzuru! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazoea niliyoyaona, sana sana ni kupinga kwa kutoka nje au kwa kusema hapana. Lakini, kesho yake pale kwenye dirisha tunaandamana wanakuwa wao mstari wa mbele. Haya yamekuja tu, hayakuwa katika mpango wangu wa kuyazungumza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo langu lilikuwa ni kuzungumzia miradi ya kuimarisha Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari. Mipango hii imefanikiwa sana kwa kiasi kikubwa . Nami hapa ningependa kuipongeza Serikali, ningependa kuwapongeza wananchi kwa mshikamano wao kwa kukubali kuweza kushiriki katika hii mipango ya kuimarisha Elimu ya Msingi na baadaye Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi yote hii imekumbana na changamoto mbali mbali. Changamoto kubwa tuliyoipata katika mradi wa MMEM ni kupata watoto wengi sana waliofaulu, ndipo basi tukaanzisha mradi wa MMES ili kuweza kupata Shule za Sekondari za kuwapokea watoto walioshinda mitihani ya Darasa la Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu jinsi tunavyoendelea na shule zinavyoendelea kujengwa, pia zipo changamoto mbali mbali ambazo zinakabili huu mradi wa MMES au ujenzi wa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto moja kubwa na ninayoiona katika shule hizi za Sekondari ni mazingira ambayo hayajaridhisha, mazingira ambayo yanaweza yakamfanya mwalimu kufanya kazi yake vizuri, mazingira yanayoweza kumsaidia mwanafunzi naye akaweza kujifunza vizuri na kuelewa masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyojua shule hizi nyingi sana ziko vijijini na vijiji vingine viko mbali sana na maeneo ya mijini ambako watoto wala hawajawahi hata kupanda magari, hawajawahi kuona umeme, hawajawahi kuona vitu kama hivyo. Mimi nazungumza nikijiuliza kwa mfano mtoto aliyeko katika shule za Sekondari kwa mfano ya Mgoma, Kirusha, Urusagamba na sehemu nyingine mbali mbali zilizo mbali yaani niseme *remote areas*, labda ndio nitaeleweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hao watoto, kwanza tunasema Tanzania hatuna ukabila, lakini watoto hawa wanaozaliwa ndani ya vijiji au ndani ya kata, wanasoma shule ya msingi na wanasoma shule ya sekondari katika maeneo hayo ya nyumbani, bila kutoka nje kukutana na watoto wengine wa makabila mengine au wa maeneo mengine mbali mbali. Utakuta kwamba kama hatutaangalia tutajenga ukabila bila kutambua.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa napendekeza kwamba Serikali ianze kufanya utaratibu wa kuzigeuza shule hizi ziwe shule za bweni ili kwamba watoto waweze kuchaguliwa, mtoto atoke labda Morogoro aende Kagera, wa Kagera anaweza kwenda Mbeya, anaweza kwenda seheemu nyingine ili tuweze kuendeleza ule utaifa wetu bila kujali ukabila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira mengine ambayo naona hayaridhishi, ni kwamba shule hizi ni za kutwa. Lakini, kutwa wanaweza kusoma hata usiku, lakini mazingira hayaridhishi. Kwa hiyo, mimi naomba kwamba ufanyike utaratibu, sehemu ambazo zinaweza zikapatiwa umeme wa gridi au umeme wa jenereta, basi shule hizo ziwekewe umeme. Lakini, kwa maeneo ya vijijini, Mpango huu wa MMES uweze ukazisaidia hizi shule ziweze kuwa na umeme wa Jua. Kwa kweli itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto wanapokuwa katika shule za Bweni ni tofauti sana na wale wanaosoma kutwa. Wanakuwa na mambo mengi mbali mbali ambayo wanaweza kufanya au kujifunza kwa pamoja bila kujali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba watoto wanapokuwa katika shule za bweni wana nafasi nzuri zaidi ya kujifunza mambo mbali mbali kama tunavyoona, kuna shughuli nyingine ambazo watoto walikuwa wanajifunza na zinawasaidia, sasa zinaanza kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vuguvugu la Maskauti wa Kike hatulioni. Maskauti wa kiume na lenyewe hilo hatulioni lakini yalikuwa ni mambo ambayo yanamsaidia sana mtoto kuweza kujifunza kwa mazingira na kuweza kujifunza kutumia mazingira yake na kutumia vitu mbali mbali ambavyo vinaweza vikamsaidia katika maisha yake, kwa sababu kujifunza siyo kusoma darasani tu, lakini kimazingira pia anaweza akajifunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuzungumzia upangaji wa mipango na ugawaji wa rasilimali. Jinsi ninavyoona ni kwamba huenda labda takwimu hazipo, lakini nina hakika kipo kitengo cha takwimu. Kwa hiyo, takwimu mbalimbali zipo ambazo zinaweza kusaidia Serikali ikagawa rasilimali kulingana na takwimu hizo. Hivi Serikali

kwa mfano, haijui kwamba Mkoa wa Kagera uko mbali sana kutoka Dar es salaam ambayo ndiyo ina viwanda vya kutengeneza vifaa mbali mbali vya ujenzi.

Kwa mfano, mnapogawa Sh. 3,100,000/= kwa ajili ya ujenzi wa darasa la shule ya msingi, ukampa mtu wa Kagera kiasi hicho na wa Dar es salaam akapata hizo hizo. Hivi kweli hapo Serikali inakuwa imetenda haki? Kwa sababu bei za vitu Dar es salaam na Mkoa wa Kagera au Wilaya ya Ngara au Wilaya ya Karagwe ni tofauti sana hata Mjini Bukoba. Bati moja shilingi 20,000/=, Mfuko mmoja wa saruji shilingi 20,000/=. Lakini, Dar es salaam kuna nafuu.

Kwa hiyo, mimi ninadhani kwamba ifike wakati tuzigawe rasilimali kulinga na hali halisi ya maeneo, kulingana na umbali, uwingi wa watu na takwimu nyingine mbali mbali ambazo zinaweza zikasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kwa hali tuliyofikia sasa, ifike wakati sasa Serikali ianze kuangalia maeneo ambayo yamenyimwa haki au yamenyimwa maendeleo kwa muda mrefu. Sio vizuri katika Taifa moja, Taifa ambalo tuna amani na utulivu, basi kukawa na watu wengine wanaolalamika kwamba hawajapata maendeleo. Kwa mfano, wengine tulalamike kwamba hakuna lami kwenye barabara zetu, lakini sehemu nyingine lami imeingia mpaka vijijini. Sehemu nyingine hakuna umeme, kwa mfano Wilaya za Ngara na Biharamulo zilinyimwa umeme kwa muda mrefu sana, walipokuja kupewa umeme wa jenereta, mara kwa mara zinazimika. Lakini unakuta pia ni sehemu ndogo tu ka mjini wamepewa.

Kwa mfano Ngara, wangepeleka umeme Lulenge, wakapeleka Kabanga ambako kuna Ofisi za *TRA*, kuna Ofisi za Uhamiaji. Lusumo pia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wengine wanalilia umeme kwenda vijijini, sehemu zingine hawajapata umeme. Kwa hiyo, mimi naomba tunapogawa rasilimali, basi ziangaliwe mwingine asionewe au mwingine akapunjwa na tukaanza kuwa tunalalamika.

Mheshimiwa naibu Spika, tunajua kwamba nchi yetu ni kubwa na sisi ni maskini. Lakini pia, kama kuna utaratibu mzuri, rasilimali zinaweza zikagawanywa vizuri na watu tukafanya kazi na kupata maendeleo bila kunung’unika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi natanguliza shukrani kwa kunipa nafasi ya kuzungumza kuhusu bajeti hii ya Mipango pamoja na Fedha. Kwa ujumla mimi nawapongeza Mawaziri wote wawili kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na watendaji wao kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa uelewa wangu naelewa kwamba bajeti ni kupata hela na kutumia hela. Maana yake ni kwamba tunachohitaji hapa ni kukusanya hela ili tuweze kuzitumia kwa manufaa mbali mbali ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wenzetu walioandaa bajeti hii ndivyo walivyoandaa na ndivyo walivyoandika katika vitabu vyao vyote viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pengine nianze kwa kuunga mkono hii hoja moja kwa moja maana nisije nikasahau huko mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na kusema kwamba mimi ninavyoamini kwamba kutokana na utaratibu huu na kutokana na mapato yaliyopangwa hapa ya kukusanya, uhakika wa kutoa huduma kwa wananchi kwa kipindi hiki cha mwaka huu wa 2007/2008, utakuwa mkubwa sana kwa maana kwamba yale yote yaliyoandikwa humu, mimi natazamia kwamba yatatekelezwa kwa uhakika. Naamini kabisa kabisa itakapofika mwishoni mwa mwaka 2008, tutakuwa na uhakika kutokana na mapato haya yaliyopangwa kukusanywa na jinsi mipango hii ilivyopangwa, mengi yatakuwa yametekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nianze na lile la kwanza kabisa ambalo kwa kweli mara nyingi tunakuwa tunalizungumza na naamini baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameishaligusa tayari.

Sisi wa Mkoa wa Dodoma na baadhi ya mikoa na hata mikoa mingine, suala la Barabara ya kutoka Arusha – Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa, ni suala ambalo ni la muhimu sana, ni suala ambalo kwa kweli kwa wananchi wa maeneo hayo wakiona barabara hii inatengenezwa, tuna uhakika sasa kwamba mafanikio tutakuwa tumepta na tutakuwa tunafuarahia bajeti hii. Vinginevyo, ni kwamba pengine isipofanyika hivyo, tutakuwa tunashindwa kuelewa kwamba Serikali yetu imeshindwa kuona suala hili na kwamba hatutakuwa na uhakika kwamba barabara hii itajengwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoelezwa katika kipindi kilichopita kwamba barabara hii ilikuwa inafanyiwa upembuzi yakinifu, ningependa kujua na ningependa Serikali itueleze kwamba ule upembuzi yakinifu umefikia wapi na uko kwenye hatua gani na Serikali inajiandaaje kujenga barabara hii. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile ni kwamba makusanyo haya mimi nina uhakika, sasa watumishi wetu wa Serikali wataongezewa mishahara kama ilivyoelezwa katika kitabu hiki cha fedha. Kwa hiyo, hilo mimi sina wasi wasi nalo na kwa kuwa tayari limeishaandaliwa, basi sisi kazi yetu ni kuipongeza Serikali kwa maandalizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba bajeti hii na mapato haya ya bajeti hii, mimi nina uhakika kwamba hospitali zetu sasa hazitakosa dawa na shule zetu zitajengwa. Ila nianze kuzungumza na mimi kuhusu suala la shule za Sekondari.

Kwanza, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ndiye aliyeanza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kupokea hilo na hatimaye Mheshimiwa Waziri wa Wizara hiyo na hatimaye mikoani kwa Wakuu wa Mikoa, na hasa nimpongeze Mkuu wa Mkoa wetu wa Dodoma, Mheshimiwa William Lukuvi, alisimama kidete na sisi wa Dodoma tunasema kwamba

kwa kweli tunamtakia afya nje ili aweze kuendelea kuchapa kazi katika Mkoa wa Dodoma. Kwa kweli tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lililobaki katika shule za Sekondari ni kuhusu ujenzi wa hosteli. Ni shule chache ambazo kwa kweli mpaka sasa hivi zimeishakuwa na hosteli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina uhakika kwamba kutokana na mapato haya, sisi wananchi ambao tumejitahidi kuiunga Serikali mkono, ninaomba vile vile niwapongeze wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa kazi nzuri waliyoifanya na naamini hata hili suala la ujenzi wa hosteli kama Serikali ikatuunga mkono, tuna uhakika kwamba tuna uwezo wa kujenga hosteli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme juu ya suala la maji: Suala la maji ni muhimu sana katika nchi yetu na katika vijiji vyetu. Maji yakienezwa katika vijiji vyote, tuna uhakika sasa akina mama watakuwa wamepata nafuu na kwamba hawatasafiri kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie tu kidogo kuhusu Bwawa moja la Kisaki ambalo liko Wialaya ya Kondoa. Bwawa hili ni kubwa na huwa linasaidia sana baadhi ya vijiji vinavyolizunguka Bwawa hili. Vijiji hivi ni:- Kisaki, Maono, Mahonko, Chubi, Itaswi na baadhi ya vijiji vingine vinavyozunguka Bwawa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kwa Serikali ni kwamba Bwawa hili lilikuwa hata lina samaki wengi na wananchi walikuwa wanavua kipindi cha mwaka mzima na walikuwa wanaweza kujipatia kipato kutokana na samaki kutoka kwenye Bwawa hilo.

Sasa kwa taarifa zilizopo kwamba bwawa hili baada ya mvua kubwa kunyesha kwamba limeshapasuka na bwawa hili halina maji tena. Kwa maana hiyo basi vijiji vinavyozunguka bwawa hili na vile vile shule zinazozunguka bwawa hili na ikiwepo Shule ya Sekondari kwa bahati mbaya kabisa kwamba sasa inawezekana kabisa kipindi kijacho wakakosa maji ya kutumia. Sasa mimi niiombe Serikali kama inajua basi itakuwa vizuri, lakini kama bado ilikuwa haijajua naomba kabisa iweke Bajeti ya dharura kwa ajili ya bwawa hili vinginevyo vijiji vyote hivi na shule zote hizi na Sekondari hii ni uwezekano wa kuweza kufungwa upo kabisa kwa sababu hakuna maji ya kutumia. Naiomba Serikali kwamba iweze kuweka Bajeti ya dharura kwa ajili ya bwawa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naiomba niipongeze Serikali kutokana na mpango wake, imejiwekea utaratibu wa kukopesha wananchi fedha kwa ajili ya kuendesha miradi mbalimbali na kwa maana hiyo basi ni kuendelea kuunga mkono suala zima la mikopo kwa wananchi. Kama ilivyohimiza Serikali kwamba tuanzishe *SACCOS* ili waweze kukopesha wananchi katika mifuko hiyo.

Mimi naishukuru Serikali kwa sababu baadhi ya vikundi vingi na baadhi ya *SACCOS* nyingi zilishakosa fedha katika mfuko ambao tayari ulishaanzishwa na Mheshimiwa Rais wa shilingi bilioni moja moja kila mkoa. Kwa hiyo, kutokana na

nyongeza hii tuna uhakika sasa wananchi wetu wataendelea kukopa na akinamama ambao kwa kweli ni wakopaji wazuri na walipaji wazuri wataendelea kukopa na wataendelea kujikwamua katika suala zima la kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala zima Serikali iko tayari na kuendelea kuandaa utaratibu wa kuwakopesha wananchi fedha kwa ajili ya kujenga nyumba. Hili ni suala jema na ni suala zuri sana na mimi nasema kwamba suala hili litawakomboa wananchi ambao kwa kweli pengine hata uwezo wa kujenga nyumba ilikuwa hawana. Kwa hiyo, haya masuala ambayo yanawagusa wananchi, mimi binafsi kwa kweli yamenifurahisha na tutaendelea kuyasemea na kuwahimiza wananchi waunge mkono Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuboresha pensheni kwa wastaafu. Sisi wote baadhi yetu hapa ni wastaafu. Mimi nilitaka kujua tu mmesema kwamba mtatuingiza katika Mashirika ni pamoja na *NSSF* na mengine. Sasa pengine ningependa baadaye Serikali inisaidie nielewe kwamba kupelekwa huko faida yake ni nini? Tutakuwa tunakopa huko, au tunapata faida ya ziada au ni nini? Mimi nilikuwa naomba pengine Serikali inisaidie kuelewa hilo na naamini Serikali ikieleza na wazee wote wa pensheni wataelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa naomba nizungumzie ni juu ya suala la kilimo. Wote tunaamini na tunafahamu kwamba suala la kilimo ni uti wa mgongo. Sisi wa Mkoa wa Dodoma ni wakulima wazuri sana, shahidi Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amejionea mwaka huu kwamba tumelima, kipato tutakachopata cha kilimo mazao yetu yatakuwa ni pamoja na ziada. Kulima huku ni kwamba wananchi wetu si kana kwamba hawawezi kulima, wanalima na kila mmoja analima kulingana na uwezo wake. Sasa nilikuwa naomba Serikali inisaidie kwamba suala la kilimo wananchi wanalima kama wanavyoweza lakini tunachotakiwa ni kuboresha kilimo, kuboresha mazao, mazao ambayo yanaweza yakaingia katika masoko mbalimbali na yakaonekana kwamba ni mazao. Ili tuweze kufanikiwa kwa hilo ni suala la watumishi wa Idara ya Kilimo kuweza kuwatembelea wananchi ili waweze kuwaelimisha wananchi na kusimamia suala zima la kilimo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua tu kwamba je, hawa watumishi tulionao sasa wa kilimo uwiano ukoje na wananchi wanatosha ama hawatoshi na kama hawatoshi mimi niiombe Serikali iendelee kuajiri watumishi hawa ili wawe karibu na wananchi waweze kuwasaidia wananchi. Kwa utaratibu wakiwepo watumishi wa kilimo wa kutosha uwezekano wa ufuatiliaji ni mkubwa. Kwa sababu sasa hivi wananchi wanalima, hakuna Afisa Kilimo anayefuatilia kuona kwamba mwananchi huyu amelimaje, amepandaje, ametumia mbegu za aina gani na kwa kweli matokeo yake mtu analima eka mia moja anavuna gunia 200 ni kitu ambacho kwa kweli si kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mazingira. Katika vitabu hivi nimesoma suala la kwamba Serikali inaandaa utaratibu wa matumizi ya gesi la *LPG.* Vile vile inaandaa utaratibu wa mionzi ya jua na *biogas*. Kwa sisi wa Mkoa wa

Dodoma gesi ya *biogas* ilishaanzishwa na ilishajaribiwa na watu walifaidika. Tatizo la gesi ya *biogas* ni kwamba inahitaji maji mengi. Sasa vijiji vyetu kwa kuwa havina maji ilifika mahali kwamba wananchi wakashindwa kuendelea kuitumia teknolojia hii ya *biogas*. Sasa pengine kama kuna uwezekano wa Serikali kutusaidia hasa katika suala la maji itakuwa vizuri zaidi na niilitaka kuelewa juu ya suala la hii gesi la *LPG.* Mmesema kwamba itaanza kutumika katika maeneo ya mijini na naomba kabisa kwamba iwe ni pamoja na vijijini. Hii ya jua kwa sababu itawasaidia akinamama kuweza kupata muda wa kufanya shughuli nyingine. Kwa sababu kuni na mkaa sasa hivi ndizo zinazoweza kutumika.

Vile vile kuni na mkaa maana yake ni kwamba ndiyo tunaendelea kuharibu mazingira. Sasa kama *biogas* itapatikana kama mionzi ya jua itapatikana na kama hiyo gesi ya *LPG* itapatikana, mimi nina uhakika utunzaji wa mazingira utakuwa mzuri zaidi na baada ya miaka kumi nchi yetu itaonekana, miti imeenea kila mahali. Sasa niiombe Serikali kwa utaratibu wake huu uliojiwekea basi ifanye juhudi za kutosha ili ikiwezekana teknolojia hii ienee katika vijiji vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya suala la Shirika la Bima. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mada hizi mbili ambazo zimetolewa na Mawaziri wetu. *(Makofi)*

Ninaomba kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha nichukue fursa hii kutoa pole kwa ndugu zetu wale waliopata msiba, kumetokea ajali kule Singida na sisi wananchi wa Siha tunaungana na wenzetu katika msiba huu. Mwenyezi Mungu awaweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yanayozungumzwa hapa ni masuala ya msimamo, si masuala ya barabarani. Ni masuala ambayo sasa hivi Taifa zima linatuangalia na linatusikiliza. Sisi ndio ambao tumepewa dhamana ya kufanya maamuzi kwa niaba ya Watanzania wote. Msimamo maana yake ni kutetea jambo ambalo unaliamini. Kama jambo unaliamini unalitetea unasema mimi nitalitetea hata kama mbele ya watu halipendwi, unalitetea kwa sababu unajua kuna kitu unacholenga. Nataka tuelewane hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi tulionao, uchumi huu wa kwetu na *almost developing countries* nimewahi kusema mara nyingi ni uchumi wa nyuma, duni na wa kikoloni mamboleo. Ni uchumi ambao haujitegemei, ni uchumi ambao pampu yake ya kuendesha uchumi huo iko nje. Asilimia 40 ya fedha tutakazopitisha hapa haitoki humu ndani, inatoka nje. Uchumi wetu sisi ni uchumi tegemezi, ni uchumi ambao unategemea

Mataifa mengine yatusaidie. Ukishakuwa na uchumi wa namna hiyo na wale wanaotutawala ambao wanatupa hiyo misaada wanapenda uendelee kutegemea hivyo kwa sababu kwa kufanya hivyo ndiyo unatawalika. Kama unajitegemea hivi unasomesha watoto, unatibu wagonjwa hospitali, barabara zako ni nzuri na kila kitu kinakwenda vizuri huwezi kunitawala, nitakwambia mimi sili kwako. Lakini kama unanitegemea maana yake ni kwamba uhuru wako unapungua na ndiyo *dillema* tunayoiona hapa. Wabunge wenzangu na Wabunge wa Upinzani nawaombeni, tunaondoka hapa tunakwenda kwa wananchi twendeni tukawaambie wananchi ukweli wa mambo, uwezo wetu tulionao hapa, tumeambiwa walipopeleka maombi ya fedha walitaka trilioni 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo trilioni 12 hazikupatikana. Fedha za hapa ndani zimepatikana trilioni 3 na za msaada kutoka nje trilioni 2 kuna upungufu wa trilioni 7, unaambiwa tengeneza Bajeti hapa ili Watanzania kwa mwaka mmoja unaokuja waishi, wale, wanywe utengeneze, unafanyaje? Mimi nataka niseme kwa sababu najua baadaye nitasahau kusema kwamba naunga mkono jambo hilo. Kwa niaba ya wananchi wa Siha nasimama hapa kusema kwamba mimi naunga mkono hotuba zote mbili na Bajeti hii na nitaeleza. *(Makofi)*

La kwanza nililokuwa natafuta humu ndani nilikuwa natafuta kama Bajeti hii inafanya kazi ya kujenga ujamaa. Ndani Mzee Kingunge anafahamu nilikuwa natafuta humu ndani hii Bajeti inajenga ujamaa, la kwanza hilo. Nasema Bajeti inafanya kazi ya kujenga ujamaa nita- *quantify* mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nilitaka kuona na Katibu Mkuu upo hapa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatekelezwa hapa, inatekelezwa. Kwa hiyo, naunga mkono hayo mawili. Nikienda Siha nitaeleza kwamba mimi nimekwenda pale nimepitisha Bajeti ile kwa sababu Bajeti ile mle ndani ilikuwa inazungumza habari ya barabara. Iko barabara inayotoka Bomang'ombe mpaka Sanyajuu mpaka Ngarinairobi mpaka Kamwanga ipo imetamkwa kwamba itajengwa na nilisikia kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi akizungumzia Waziri halafu leo unaniambia mimi nisipitishe kwa sababu mafuta yamepanda, nitaeleza watakaokuja kule watakuta nimeshaeleza, kwa sababu nisipopitisha hapa barabara ile haitajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nieleze, mpango ni *component* ya kijamaa. Mpango sio *component* ya Kibepari. Mabepari huwa hawapangi, Mabepari wanaoendeshwa kwa sheria ya utashi na urari, sheria ya mashindano na sheria ya thamani, *below demand and supply*, *below competition and the law of value* ndiyo inayofanya kazi ndicho kinachozungumzwa hapo. *Let us talk economics*. Tuzungumzie hapa. Wanakugawia ule mtaji wa kutengenezwa pale, tajiri anachotafuta mle ndani kuna kitu kinachoitwa *constant capital,* jumlisha na *valuable capital*, mle ndani unatakiwa uweke na kitu kinachoitwa *surplus labour* ndiyo unapata kitu kinachoitwa *value,* unapata thamani; nitaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima upate fedha ya kuweka katika mtaji kwa maana ya mashine, lazima upate fedha za kulipa mishahara, lakini ndani yake lazima upate nguvu kazi ya ziada ndiyo unapata thamani. Unakwenda unafika mahali unasema nataka

kuendeleza nchi hii. Umelipa majeshi, umelipa shule, umelipa kila kitu halafu huna ziada, *development* ni *surplus*. Kama huna ziada huna maendeleo, ni mpaka ufike mahali useme nimekula, nimevaa nimekula chakula nimejenga nyumba lakini nimeweka pembeni ziada hii ndiyo una *develop,* unajenga barabara. Bajeti za kwetu zilikosa kitu kinachoitwa mtekenyo wa ndani, hazina kitu kinachosukuma, ndiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hamna kitu kinachosukuma mle ndani. Sisi tunachofanya sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kusema hivi pamoja na kula na kusomesha watoto na majeshi yamelipwa na mishahara imeletwa humo humo zungusha hiyo fedha ili ufike mahali urudishe katika lile eneo ambalo imezalisha. Ukila zote ukamaliza umekwenda na maji. Hakuna *development* na hiyo *dependence* iliyozungumziwa kutegemea Mataifa kutoka nje itaendelea milele na milele. Ni mpaka ufike mahali useme hivi sasa mimi nitafunga mkanda, nihakikishe kwa kufunga mkanda huu najiondoa hapa nilipo na ndicho kilichofanyika kwenye Bajeti ya Mama Zakia Meghji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusikae hapa Serikali mkajikunyata hapa. Waziri Mkuu songambele, Mawaziri songambele, Mheshimiwa Jakaya Kikwete songambele. Nendeni mbele wala msijikunyate mkaogopa mkasema ooh, kuna matatizo. Miaka mitano tukienda hivyo tunavyokwenda hapa nataka niwaambie Watanzania watarudi watasema *we have a government* na sasa hivi tayari wameanza kukiri na nitakuambia, nisikilize, nikupe takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba nichukue Bajeti iliyopita, miezi sita tulipata ripoti sisi kutoka kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi inasema watoto waliofaulu walikuwa 468,252, waliopata nafasi ya kwenda Shule za Sekondari ni 235,905, sawa na asilimia 50 ambayo inatamkwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu na Serikali, Mawaziri wakakimbia Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wamepita nchi nzima kuhimiza Shule za Sekondari, matokeo yake zikajengwa Shule za Sekondari 1,040. Watoto wakatoka, kutoka hapo tukapeleka watoto 416,363 sawa na asilimia 89, wakaenda Shule za Sekondari. *(Makofi)*

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ilisema asilimia 50. Tumekwenda tumekuta wanafunzi waliobaki asilimia 14. Mkoa wa Arusha asilimia 100, Tabora asilimia 100, Singida asilimia 100, Shinyanga asilimia 100 halafu tunapita tunakuja Dodoma hapa asilimia 100 tumewapeleka. Halafu tunaambiwa Bajeti hizi ni za kitapeli. Jamani jamani tunakaa hapa tunasikitika tunasema tumefanya mambo makubwa Watanzania leo tunaambiwa Rais yetu wanamwita New York kuna *Institute* inaitwa *Africa American Institute* inatoa tozo kwa Tanzania kwa jitihada tulizozitoa katika elimu. Ngoja kwanza, nakuelezea. Leo tunakuja hapa tunasema hamna kitu bwana pale. Mimi siwezi kusema maneno namna hiyo hata kidogo. Siwezi kusema maneno namna hiyo. Nasema naunga mkono Bajeti hii mkono nimeambiwa asilimia 18 ya fedha tunazopitisha hapa zinakwenda kwenye elimu ni hatua kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu kinaanzishwa hapa Dodoma tunapeleka watoto 40,000 tatizo tulilonalo katika nchi hii ni tatizo gani. Tatizo letu sisi ni *contradiction* yetu sisi ni kati ya *labour* na *label of the productive process*. Ni kati ya nguvukazi na kiwango cha kutendea kazi. Tatizo la Tanzania ni umaskini. Bunge hili lazima lifike mahali lianze *with a full acceptance of our own poverty,* lazima liseme hivyo. Liseme sisi ni maskini, lifike mahali liseme tuna *sacrifice poverty*. Lazima liseme hivyo, liseme sisi ni maskini. Lifike mahali tuseme tunawapeleka tunawaambia wananchi tutatoza dizeli, wananchi tutatoza sisi petroli. Lakini tukiwa na hakika kwamba mbele ya safari tutawaletea maisha mazuri zaidi ndicho tunachotaka.

Sasa nisikilizie tunasema tunataka barabara *Mtwara corridor* utaipelekaje kule sasa kama huna fedha, tunasema Kigoma hapa tunataka tuunganishe na Kongwa utapelekaje sasa kama huna fedha, unatoka hapo unakwenda Horohoro tunataka kupeleka barabara. Dodoma, Iringa, Arusha tunataka kuunganisha Arusha na Dodoma, *how?* Hapa hakuna habari ya lelemama, wewe kama unafuga kuku na ndani ya banda la kuku unaweka pale mifugo kumi. Ukisema napunguza mifugo ile itakuwa nitapeleka mitano na kuku wana *respond immediate* wanapunguza mayai kama ulikuwa unapata *tray* kumi zinakuwa tano, zinakuja sita ukija kuanza tena wala huwezi kuwahi. *(Makofi)*

Tunazungumza habari ya Kikoloni, Karl Max alisema *always the economic base determined the superstructure,* ndivyo alivyosema.

Namalizia, naomba nimalizie tusaidiane hapo. Mimi nataka niwaambie mambo yafuatayo, la kwanza tunakwenda katika suala la mafuta. Ni kweli nakubali kwamba ukishapandisha bei ya mafuta maana yake ni kwamba gharama za uzalishaji zimeongezeka. Ni kweli *it is true* hiyo kabisa, *there is no dispute about it*. Lakini unasema maneno yafuatayo, mimi nasema ongeza bei ya mafuta lakini wakati huo huo simamia sasa watu wasitumie mwanya huo kusema kwamba ipande tu ovyo ovyo. Kama wewe umeongeza shilingi 100 pale zimekuwa 200 Mheshimiwa Zakia Meghji hakikisha kama tulikuwa tunauza shilingi 1,250 tunategemea kitakachokuwa kimeongezeka pale itakuwa 1,350. Lakini kesho utasikia watu wanakwambia mafuta yamepanda 1,800, 1,900 ndipo hapo *EWURA* inaingia hapo na akina *SUMATRA* wanaingia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kamulize David Licado, nenda kamuulize Adam Smith, nenda Lord …..mahali popote kwenye *market failure,* Serikali itaingilia kati. Serikali hii mimi najua ni makini. Sisi tunapitisha Bajeti wananchi wanatuogopa, vijana wetu waliopo Serikalini wanajua kwamba sisi tunafikishwa hapa, sisi tunawaomba Serikali mbebe jambo hili na wajibu ndani yake, *you must treat this thing with a high sense of responsibility*. Mnaondoka hapa mnakwenda, twendeni tukasimamie.Tukisema hapa tunakwenda kutengeneza sisi, Mheshimiwa Andrew Chenge amesema hapa anakwenda kutengeneza hapa kilomita 500 tuzione kilomita 500. Tuzione hizi hapa ukasimamie. *(Makofi)*

Mimi naomba nimalizie, naomba niseme maneno yafuatayo, Bajeti hii mimi naipitisha, Bajeti hii mimi ina baraka zangu. Mimi naamini kwamba mtakwenda kusimamia, mimi naamini kwamba Serikali itakwenda kufanya na kwa Tanzania kesho

na kesho kutwa watageuka watasema kweli tunayo Serikali makini ambayo inafanya kazi yake.

Mimi nawaomba mkafanye kazi hiyo. Nina hakika nawaomba *opposition* ndugu zangu akina Mheshimiwa Zitto Kabwe, tupitishe Bajeti hii msiikatae. Tutakwenda mbele ya safari tutakuja kufika mahali tutaona. Yapo mambo yamezungumzwa humu ndani mmesema kwamba mnataka wapitishe pale bandarini wasipime mpeleke moja kwa moja, hapana. Piga darubini pale angalia vizuri. Hakuna mambo ya urafiki, hakuna *compliance* hapa katika mambo ya *business.* Pima pale, weka *camera* kila mzigo unaopita pale unahakikisha kwamba unaupima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la mafuta ya taa tunaweza tukaliangalia katika hili tulilozungumza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tutaliangalia vizuri ni jambo ambalo linahusu lakini tunaweza tukaliangalia vizuri. *(Makofi)*

Mwisho naomba nirudie eeh, ndiyo mimi hapa nabeba wajibu, nimeletwa na wananchi wa Siha hapa. Mimi naomba tusaidiane kidogo. Mlima Kilimanjaro pale ile barabara pale peleka barabara izunguke Mlima Kilimanjaro. Asilimia 50 ya Bajeti yetu itatoka pale kwenye Mlima Kilimanjaro kama miundombinu inapelekwa pale. Watalii waende pale sisi hapa tunakaa tunapiga kelele, unajua Kenya wanasema mlima uko kule unayo *infrastructure*. Barabara ile ya kwangu Mzee Chenge peleka barabara pale Mlima Kilimanjaro pale Mzee. Naunga mkono Bajeti hii ipite. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa siku ya leo ili na mimi niweze kuchangia katika suala zima la Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni furaha ilioje kwamba nimo Bungeni humu leo baada ya misukosuko ambayo ilinipata ambao nadhani wote nilishawaelezeni. Basi nipende kutoa shukrani zangu mbele yenu na hasa hasa mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba niko hai na kweli nina afya njema na sasa naongea na ninyi naomba mnisikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la michango ya wenzangu mimi ninachotaka kuzungumza, kuna msemo ambao huwa unazungumzwa tu na walio wengi ambao wamepitia misemo wanasema hata Roma haikujengwa kwa siku moja. Sasa katika msemo huu maana yake ni kwamba tunapashwa kuibeba Bajeti yetu kama ilivyo pole pole mpaka hapo Tanzania yetu itakavyoona kuitekeleza badala ya kuikanusha hivi hivi bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote huwa zina Bajeti. Kokote pale, ulimwengu wote wana neno hili Bajeti. Leo sisi Tanzania tunapobeba neno Bajeti ni kama vile tunalibeba basi kulisubiri kuona nini kilichomo na kupinga.

Mimi ninaamini tunapobeba neno hili basi tuone kilichomo tuweze kukitafakari na kuona tuweze kufanya nini kwa manufaa ya wananchi wetu. Sio kusubiri tu ngoja

tuone tutafanya nini, kama vile tunajitungia wenyewe Bajeti kwa manufaa yetu, hapana. Hawa waliokaa Mawaziri pamoja na Kamati zao wamekaa kwa muda mrefu na kuona tufanye nini kwa manufaa ya wananchi wetu. Kwa hiyo, mimi nichukue kwanza nafasi ya kwanza kabisa kuwapongeza kwa sababu wamechukua muda mrefu kwa manufaa ya nchi nzima. Leo hapa sisi tunakuja tunajiandaa kuja kupinga hatutakuwa wastaarabu hata kidogo. Lazima tukubaliane kujadili kuona tunagusa wapi, wapi ni vyema na wapi pamejikunja kidogo si tunapanyoosha tu mambo yanajipa. Lakini ni mbaya kujiandaa kuipinga Bajeti bila ya sababu. Mimi nawapongeza na nitamke tu mapema kwamba hii Bajeti mimi naiunga mkono tu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninatokana na Chama cha Mapinduzi. Niko tayari kabisa kutekeleza yote ambayo yamo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu Bajeti yenyewe imezingatia kikweli kweli Ilani ya Chama cha Mapinduzi yaliyomo ndani. Ila ninachotaka kuzungumza kidogo tu ni upande hasa hasa wa mambo kama mawili matatu hivi.

La kwanza napenda nigusie suala la kilimo, tunazungumza kwamba nchi yetu ni asilimia 80 ambayo ni wananchi wanaotegemea kilimo ni kweli. Sasa tunawaandaa vipi hawa wakulima ili kweli wafike mahali waweze kuiona nchi hii nao ni watu ambao wanapaswa kuthaminiwa. Wanayo ardhi na wanayo nguvu kazi, lakini wanapolima wananchi hawa wanapeleka wapi mazao yao na ni kwa thamani gani hapo ndipo tatizo lililopo. Wanalima kweli, mimi juzi nitoe mfano ambao pamoja na kwamba si kwetu, lakini nilikuwa Mbeya. Wananchi wanalima viazi hivi vya mviringo gunia moja shilingi 10,000 hee, Mungu. Anakuja kulanguliwa na tajiri mmoja mpaka litakapofika Dar es Salaam linauzwa shilingi 100,000. Sasa kutoka shilingi 10,000 mpaka shilingi 100,000 hivi huyu mkulima sasa anafaidika nini? Tufika mahali tunapoongea kuwasogezea masoko wauze wapate faida hivi kweli tuliweke katika utekelezaji ili na yeye mkulima huyu aone jasho lake linazaa matunda. Tusiyaweke tu katika maandishi. Tena huyu mkulima mimi huwa nambeba pamoja na mfugaji, hawa watu huwa ni marafiki lakini inapofika mahali Serikali inapowaweka sawa ndiyo inayowagonganisha hawa watu.

Lakini hawa watu mimi huwa ninawaona ni marafiki kwa sababu mkulima mwema huwa lazima aende akanunue mifugo madume ili kusudi aweze kuja kulima vizuri, kupata maksai ili aweze kupata kilimo bora sasa katika hili huyo huyo pia mfugaji naye mnamhangaisha hangaisha tu kumpeleka mpaka maeneo ambayo si halali anapopaswa kuuishi. Sasa katika hili ninachotaka kusema mkulima tumjali, tumjali kabisa ili aweze kupata soko la uhakika, ajikwamue mahala alipo. Haya tuliyoyaandika kwenye vitabu vyetu hivi, tuyaweke katika utekelezaji. Mimi huwa najiuliza hivi Bajeti huwa haiwezi ikakaliwa kila mwaka kila mwaka tukakaa kujiuliza tunaendeleaje na utekelezaji wa Bajeti hii. Ili tufike mahala, mahala ambapo tunaona haiendi vizuri tukarekebishana sisi wenyewe, tukaambizana tu kwamba hapa mbona tuliandika hivi. *(Makofi)*

Hivi mbona hatuendi hivi? Nadhani tukikaa kwa namna hiyo, kila leo tukakaa tuka-*review budget* yetu na tukaiona na kuizungumza na wananchi wetu wakajua tunaiongelea na kuizungumza vizuri nadhani wanaweza wakaamini kwamba tunafuatilia

mahitaji yao na kwamba tuna njia ya kuwapa imani au amani katika suala zima la utekelezaji wa Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda niliongelee ni suala la afya. Mimi afya sina tatizo nalo kwa kweli, lakini tufike mahali basi hebu katika Bajeti zetu tuzingatie hasa hasa masuala ya kinga kulikoni kutibu. Katika nchi zingine ukienda unakuta maeneo ambayo yanaongelewa kabisa kwamba yako huru na malaria. Lakini nchi yetu ya Tanzania jamani, moja ya tatizo na gonjwa ambalo linatusibu ni malaria. Je, hili gonjwa tunali-*handle* vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo linalotudhoofisha na hasa hasa akinamama zangu wajawazito wanahangaika na watoto hao hata akizaa na wenyewe wanahangaika na gonjwa hili. Kwa nini hatushughulikii kuzuia tunang'ang'ana na kutibu na hii inasababisha wananchi wengi Tanzania wamekuwa madaktari na maduka haya ambayo ndiyo yako holela mitaani kila mmoja anakwenda anatamka dawa ambayo anaweza akaifikiria kichwani ya kutibu malaria, *so longer as* mtoto au mama au baba ana homa anasema naomba dawa fulani. Lakini mimi ningeishauri Serikali itenge kabisa na ifikirie kwa makini kabisa kwa Bajeti zingine zijazo kama siyo hii kwamba tuwazie kukinga kuliko kutibu, tutaifikisha mahala kabisa nchi hii kuwa huru na maradhi ikiwemo malaria. Malaria ndiyo inayotudhoofisha kabisa Watanzania. Hatuwezi tukafika mbali kama kila leo unakwenda kulala unaumwa na mbu hata hii ngao tunaoisema, kwanza hata elimu ya matumizi haya na yenyewe ni hafifu tu. Watu wengi hawajui jinsi ya kutumia dawa hizi za kujikinga hizi. Niombe katika hili nalo tulifikirie badala ya kung'ang'ania na matibabu, hebu tung'ang'anie na suala zima la kuzuia, maana kuzuia ni bora kuliko kutibu. *(Makofi)*

Mimi sina mengi zaidi, lakini ninazidi kusema Bajeti hii na tuipitishe na mimi naiunga mkono kwa sababu tunapaswa sisi wenyewe tuione tu ndani badala ya kung'ang'ania kuipinga wala haitatusaidia lolote. Tuone undani wa kuweza kwenda nayo moja moja ili mradi sisi tuone wapi tunaweza tukanyoosha, wapi tunaweza tukasema sasa hapa tumefika hapa na kuwa na maamuzi yetu ya busara. Naishia hapo, nakaa kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia juu ya hoja mbili ambazo ziko mbele yetu kwa maana ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji lakini pia na Bajeti iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nianze kwanza naiunga mkono Bajeti kwa sababu ni Bajeti yetu. Naomba nianze kwanza na mimi kwa kutoa pole sana kwa wale wananchi ambao walipata ajali mbaya ya basi la *Mohamed Trans* kule Singida na tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema Peponi, *Amin.*

Lakini pia awape nguvu ili waweze kupona wale ambao walipata majeraha katika ajali hiyo. Naomba pia nichukue nafasi hii kwa sababu pia nimepigiwa simu na wapigakura wangu baadhi yao wakisema kwamba wamefurahishwa sana na jinsi Serikali ilivyoienzi Timu yetu ya Mpira wa Miguu yaani *Taifa Stars.* Wamefurahishwa sana na

jinsi tulivyoichangia na wanasema ile ilikuwa ni chachu kwa mashirika mengine na taasisi za Serikali kuweza kuichangia ile timu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze mambo ambayo yapo kwenye Bajeti. Kwanza naunga mkono jambo ambalo ndilo lililopewa kipaumbele katika Bajeti yetu. Suala hili ni kipaumbele kwenye elimu ya Sekondari katika nchi hii. Naomba niishukuru sana Serikali, nina hakika pesa ambazo zimepewa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zitajibu kero nyingi ambazo zilikuwa zinatokea kwenye Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kabla sijaja hapa Bungeni nilifanya ziara katika Sekondari nyingi mpya. Matatizo yaliyokuwepo ni yale ambayo yameainishwa kwenye Bajeti. Moja, vifaa vya kufundishia na kujifunzia havipo. Nimeona baadhi ya shule ambako walimu wanaazima vitabu na vifaa vingine vya kujifunzia na kufundishia kwenye shule jirani ambazo zinawezekana zimeanza kitambo. Lakini pia ni ukweli ambao uko wazi kwamba walimu ni wachache, shule nyingi hazina samani. Lakini pia hazina nyumba za walimu na mambo kama hayo.

Mimi niliwaambia wananchi nilipokuwa natembelea shule zile kwamba nina hakika Serikali inaelewa, Serikali inasikia na nina hakika wao sasa wanaona kwamba Serikali imejibu yale mambo ambayo yalikuwa yanawakereketa kwa sehemu kubwa sana.

Jambo ambalo mimi naliomba sasa ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iweke mpango mzuri wa matumizi ya pesa hizo. Haitakuwa busara tena tuje tuone pamoja na pesa zilizotengwa tushindwe kuelewa kazi gani imefanywa katika kuendeleza na kutatua matatizo mbalimbali katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningependa pia nizungumzie suala la kilimo. Mimi ambaye natoka Mbozi na Mbeya hususan kule Mbeya siwezi kuacha kuzungumzia kilimo hata siku moja. Kilimo kimepewa *priority* ya nne au kipaumbele cha nne katika Bajeti yetu. *(Makofi)*

Mimi naomba niseme bado siyo jambo baya kwa sababu kupanga ni kuchagua kama alivyosema Mheshimiwa mwenyewe Waziri wa Fedha. Lakini naomba tusisitize mambo haya, kwamba ili wananchi waweze kuzalisha vizuri lazima wawe na mbolea, wawe na uhakika wa kupata mbolea ya kutosha. Lakini pia lazima wawe na uhakika wa kupata mbegu bora kwa ajili ya kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mwaka jana pamoja na Serikali ku-*commit* shilingi bilioni 21 kwenye ruzuku ya mbolea na mbegu lakini bado hatukukidhi haja ya Watanzania na hususan wananchi wa kule Mbeya na Mbozi. Mahitaji ya mbolea katika Mkoa wa Mbeya ili wananchi waweze kuzalisha vizuri ilikisiwa kuwa tani 70,000 na mahitaji katika Wilaya ya Mbozi ili wananchi waweze kuzalisha sawa sawa walikuwa wanahitaji tani karibu 18,000. Lakini kwa bahati mbaya sana Mkoa mzima wa Mbeya ambao ulihitaji tani 70,000 za mbolea ulipata tani 18,000 tu na Wilaya ya Mbozi ambayo ilihitaji tani 18,000 ilipata tani karibu 6,000 tu. Sasa katika hali hiyo tunategemea

mwananchi huyo azalishe namna gain? Sisi kule tunalima mahindi sana, tunalima kahawa kama zao kuu la biashara na mazao mengine kama maharage na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili wananchi wazalishe, wanahitaji hivyo vitu, wanahitaji mbolea na wanahitaji mbegu. Kwa hiyo, ukiangalia mbolea tuliyoipata ilikuwa chini hata nusu ya kiwango ambacho walistahili waipate. Sasa pamoja na kilimo kupewa kipaumbele cha nne katika Bajeti yetu mimi naiomba sana Serikali na wananchi wana matumaini, na wananchi wetu wakati wote wanakuwa na matumaini kwamba Serikali yao hapa inawezekana haijafanya vizuri. Lakini wakati huo huo bado wana matumaini kwamba tunaweza tukafanya vizuri zaidi.

Kwa hiyo, naomba niiombe sana Serikali iangalie namna ya kuwaongezea ruzuku ya mbolea pamoja na mbegu kwa wakulima wetu ili waweze kuzalisha vizuri zaidi na hasa ukizingatia kwamba kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi tunasema kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. Sasa hatuwezi kuwa na kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa lakini ndiyo uti wa uchumi wa Taifa hili lakini bado pesa zinazoelekezwa huko zinakuwa kidogo sana. Mimi naiomba sana Serikali izingatie hilo na tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia nizungumzie suala la nishati mbadala. Hili wananchi wamelizungumza sana, wenzangu Wabunge wamelizungumza sana. Lakini pia na hili kwa sababu wananchi wangu wamenipigia simu na wenyewe pia wakasema tumeridhishwa kwa sehemu kubwa na Bajeti. Lakini kupandishwa bei ya mafuta hususan mafuta ya taa, wamelizungumza wengi sana. Lakini hapa mwisho amelizungumza sana kwa unyenyekevu Mheshimiwa Aggrey Mwanri, amelizungumza sana kwa unyenyekevu na mimi nina hakika kwa unyenyekevu ule basi Serikali itakuwa imesikia na sina sababu pengine ya kulizungumzia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba mafuta ya taa kwa vijijini ni nishati muhimu sana. Lakini pia tulisema ili tutunze mazingira yetu lazima tuwe na vyanzo mbadala kule vijijini. Mafuta ni moja ya chanzo mbadala ya nishati kule vijijini. Lakini unapoipandisha tena bei yake na matumizi ya umeme vijijini ni *almost* hakuna. Ukienda katika mkakati ule wa Taifa wa MKUKUTA tuliambiwa hapa mwezi wa nne usambazaji wa umeme vijijini ni karibu asilimia moja, kwa maana nyingine ni kwamba hakuna umeme vijijijini na hii ilikuwa nishati muhimu sana. Tuna hakika Serikali italiangalia hili ili wananchi wetu wapate nafuu, lakini pia ili waweze kutunza mazingira kitu ambacho tusipofanya hivyo, wananchi wetu wakawa hawana jinsi, wakaendelea kutumia mkaa, wakaendelea kutumia kuni na kwa maana hiyo kuendelea kuharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie suala la uwezeshaji wananchi. Wananchi wetu walikuwa na matumaini makubwa sana juu ya pesa zile shilingi bilioni 21 ambazo zimetolewa karibu nchi nzima na kwa maana ya shilingi bilioni moja kila Mkoa. Tumehamasishwa sana ili tuhamasishe *SACCOS* kule vijijini na tumefanya hivyo kwa ufanisi mkubwa sana. Mimi naweza nikasema Wilayani kwangu au Jimboni kwangu karibu Kata zote zimeanzisha *SACCOS.* Lakini kilichojitokeza ni tatizo la

upatikanaji wa mikopo limekuwa gumu sana na hili naomba nilizungumze na wenzangu wamelizungumza na Serikali ikaelewa vizuri kwamba utaratibu wa upatikanaji wa mikopo ni mgumu kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali imfikirie huyu mkulima, tunaposema tunataka kuboresha maisha kwa sehemu kubwa tunawazungumzia wananchi wetu wa vijijini ambao wengi wao ni wakulima na wafugaji na wanaofanya pengine na shughuli za uvuvi au zinazofanana na hizo. Mkulima tunavyoelewa, ni kwamba huyu anavuna mazao yake mara moja kwa mwaka. Masharti ya benki yanamtaka huyu mwananchi anapokopa maana yake arudishe kila mwezi, sasa huyu mwananchi anayevuna mara moja kwa mwaka atarejeshaje mkopo kama tunaweka sharti hilo?

Mimi naomba Serikali iangalie masharti ya kumsaidia mwananchi huyu. Iangalie utaratibu na izungumze, najua mabenki yanafanya biashara, maana yake naweza nikaulizwa. Waziri anaweza kujibu tu kwamba mabenki yanafanya biashara. Tunaelewa hilo, lakini ili tumsaidie mkulima huyu na kama kweli fedha hizi Serikali ndiyo imezitoa basi inufaishe makundi yote wakiwepo wakulima ambao hawana uwezo wa kurudisha kila mwezi bali wana uwezo wa kurudisha pengine mara moja kwa mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la utaratibu wa huduma ya pensheni. Kwenye Bajeti mimi nafurahi kusikia kwamba wananchi wale ambao walistaafu ambao wametumikia nchi yao kwa muda mrefu, watapata nafasi ya kupewa pesa kutoka kwenye Mfuko wa Pensheni ya Taifa ambayo ipo. Lakini wenzangu hili wamelizungumza.

Naomba na mimi niitahadharishe Serikali tunaweza tukafikiri kwamba tunatatua tatizo, lakini pengine tukazalisha tatizo likawa kubwa zaidi. Nasema hivyo kwa sababu sina hakika kama mifuko yote hii ina Ofisi huko Mikoani na Wilayani, sina hakika na kama haiko hivyo, tunaomba Serikali iandae utaratibu mzuri zaidi, mbali ya elimu hii kuwafahamisha kwamba kuna utaratibu huu sasa kama wenzangu walivyozungumza. Lakini tuhakikishe kwamba hakuna matatizo yatakayojitokeza kutokana na baadhi ya taasisi hizi kutokuwa na Ofisi huko Mikoani na Wilayani.

Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali ihakikishe mifuko yote hii ina ofisi Mikoani na ina ofisi Wilayani ili watu ambao wamelitumikia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa wasiendelee kupata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie kwa ufupi sana ni suala la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Hapa ningependa nizungumzie *TAZARA*. Suala la ubinafsishaji *TAZARA* limekuwa ni suala la wimbo, limekuwa ni kama hadithi ya muda mrefu. Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji aliitaja *TAZARA* kama moja ya Taasisi ambayo inabinafsishwa. Lakini mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu ya Bunge, naomba niseme hivi, tulikutana na Waziri, akatuambia kwamba bado suala la ubinafsishaji wa T*AZARA* ni gumu kwa sababu bado kuna madeni makubwa ambayo inatakiwa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia iwe na mkakati sasa wa kuiomba Serikali ya China kuweza kufuta madeni haya. Ina

maana hata madeni hayo bado mpaka leo hayajafutwa lakini tunasema kwamba tuna mkakati wa kuibinafsisha *TAZARA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba niseme tu kwamba wafanyakazi wa *TAZARA* wana hali mbaya sana na hali mbaya hiyo inasababisha wafanyakazi wale waihujumu *TAZARA* kwa sehemu kubwa sana na kwa maana hiyo kuidhoofisha haiwezi kuwa na uwezo mkubwa wa kusafirisha bidhaa kutoka Tanzania, kutoka Dar es Salaam kwenda nchi jirani kwa mfano Malawi, Zambia na *DRC*. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue mkakati madhubuti na pengine ilieleze Bunge lakini pia iwaeleze Watanzania, iwaeleze na wafanyakazi wa *TAZARA* mpango huu tunaouzungumza utafikiwa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mwisho kama muda utaniruhusu na hili suala la ukamilishaji wa uwanja wa ndege wa Songwe kule Mbeya. Wenzetu wa Kanda ya Ziwa wanaposimama na kuzungumza, wanazungumza barabara hizo hizo, ni haki yao kwa sababu ni lazima wananchi wapite, lazima watu wasafirishe bidhaa. Mimi kama Mbunge ninayetoka mkoa wa Mbeya siwezi nikaacha kuzungumzia uwanja wa ndege wa Songwe kwa sababu kwa kujengwa ule, najua tutakuwa tunafungua uchumi kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, lakini pia tutawezesha mizigo na abiria kwa mikoa ya Nyanda za Juu na nchi jirani za Malawi, Zambia, *DRC* pengine na Zimbabwe huko kuweza kutumia uwanja wa ndege pale Songwe. Sasa kumekuwa na kuahirisha kukamilishwa kwa ujenzi huu, tumeahirisha, tumeahirisha, tunaendelea kuahirisha. Lakini nafurahi mwaka huu kwenye Bajeti naona kuna pesa zimetengwa ingawa muda wa kukamilika kwa kiwanja hiki naona umesukumwa mbele tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiomba Wizara ijitahidi kuona kwamba ukamilishwaji wa uwanja wa ndege wa Songwe unakuwa ni kipaumbele kwa Wizara na kwa Serikali kwa ujumla kama nilivyosema ili tuweze kufungua uchumi wa Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa na mimi napenda niungane na wenzangu waliozungumza kuwaomba wenzangu wa Kambi ya Upinzani kwamba hii Bajeti ndiyo Serikali iliyoileta, ndiyo uwezo wa Serikali, hata tukiipinga namna gani lakini Serikali huu ndiyo uwezo wake, tunataka Serikali ifanye nini. Sisi tuiombe na kama wenzangu walivyosema, kuiomba Serikali isimamie haya ambayo yametangazwa, narudia tena kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Bajeti pamoja na kwamba wenzangu wamesema mengi, kila nililokuwa nataka kulizungumzia nakuta wenzangu waliotangulia wamezungumza. Lakini nitajaribu na mimi kusema machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na mfuko wa barabara. Nadhani tatizo kubwa sana hapa ni barabara zetu ambazo tunajua kwamba zote, iwe ni barabara za vijijini, iwe ni za mkoa, iwe ni za Taifa zote zimeharibika. Mvua iliponyesha mwaka jana, barabara zote zilizotengenezwa mwaka huo na barabara zilizokuwa zinasubiri

kutengenezwa zote zikarudi kuwa na hali mbaya. Nadhani tusipotafuta namna ya kutengeneza hizo barabara, nadhani Bunge lijalo Serikali itapata matatizo sana, wala siyo Serikali tu hata sisi wenyewe tutapata matatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa la kufanya ni nini, la kufanya ni kutafuta namna ya kupata fedha za kutengeneza barabara, hakuna njia nyingine. Huu umaskini tunaouzungumzia umaskini huu hauwezi ukatoka kwa sababu nchi yenyewe ni maskini. Serikali kama ni tegemezi asilimia 40 unategemea fedha kutoka kwa wafadhili, kwa madeni, kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, nakubaliana na mimi hili ongezeko nadhani tumekaa hapa siku moja tukazungumzia tukasema lazima huu mfuko wa barabara uongezwe. Kwa hiyo, ni kitu ambacho tumekaa na kufikiri na kusema ni lazima mfuko wa barabara uongezwe. Usipoongezeka kwa kweli hata kilimo hatutazungumzia jambo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bila ya barabara utafikaje huko? Kwa hiyo, hata wananchi watatuelewa kabisa kwamba tatizo la barabara zetu, hakuna kijiji ambacho kina barabara nzuri. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba kwa kweli kuwategemea wafadhili ni umaskini mkubwa sana. Nakumbuka fedha za *Quick Wins* ambalo niliulizia juzi, za maji, hatujapata hizo fedha na miradi inakaa tu inasubiri fedha kutoka kwa wafadhili, kutoka *World Bank* mpaka leo, miradi hatukuweza kufanya kwa sababu ni fedha za nchi nyingine.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono kutokana na hii Bajeti na ule utegemezi tunataka kuondokana na huo utegemezi. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa, naunga mkono kwamba huu mfuko wa barabara tuuboreshe. Ni jambo ambalo tuliwaambia Serikali nendeni mtafute namna, na wote tumezungumza hapa, imeletwa unasema tena sitaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kama unaumwa na umeambiwa kwamba utapigwa operesheni, ukikataa operesheni ni kwamba utakwenda kufa na kama operesheni ni chungu lazima ufanye nini, lazima uvumilie na sisi kama tunataka barabara zetu ziwe nzuri lazima tuvumilie ongezeko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya ushuru wa magari. Huu ushuru tulioongeza sipingani nao, lakini magari hayafanani, kuna magari mengine mabovu ambayo wananchi wanatembelea nayo lakini yako katika hali mbaya, kila siku ni matengenezo, hata kwenye *insurance* kila wakati inapunguza uchakavu wa gari, sasa kama *VX* ni shilingi 280,000/=, maana ndiyo iliyoko kijijini ambayo ina *capacity engine* yake unaipiga naye shilingi 230,000. Hivi kweli hawa wananchi waliopo kule vijijini ambao ndiyo wananchi wengine wanawategemea. Hivi si wataweka magari juu ya mawe? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tungeangalia na uchakavu wa magari, tungeangalia na *size* ya magari, aina na tuangalie na uchakavu ule. Kama gari ni laki nane, wewe kila mwaka unachukua tozo, kodi shilingi 230,000 wananchi wengi wataweka magari juu ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, naomba Serikali kila mara mimi naisifu *TRA* kila Bajeti nawasifu watu wa *TRA* kwa ajili ya makusanyo mazuri wanayokusanya na mpaka sasa nawasifu. Lakini kuna jambo moja wamelikosea na nilistuka, hivi wanajaribu kuangalia kama Wabunge wataona?

Haya makontena asubuhi Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, amezungumzia sana, nilikuwa nampigia makofi kwa sababu ni ajenda ambayo nilisema kwamba nitalizungumzia. Hiyo ni *deal,* ndiyo imetengenezwa pale. *(Makofi)*

Kwanza milango, magari mengine yapite mlango mwekundu, mengine mlango wa kijani bila kupekuliwa, hiyo naomba Serikali muifute hiyo na naomba mafuta ya taa tunayozungumzia hapa yapelekwe huko kwenye hayo makontena. Sina matatizo na dizeli, lakini mafuta ya taa, tunayotafuta au mtafute sehemu nyingine ya kupeleka lakini hiyo hatukuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama ni zuri sidhani, ni asilimia ndogo ya Wabunge wameelewa hayo makontena yanatokaje, wala hakuna kiwango cha kodi, hebu mtoe ufafanuzi vizuri. Naomba mtoe ufafanuzi kwa sababu hatukuelewa jambo hilo.

Jambo lingine ni matumizi, kwa kweli matumizi ya fedha za Serikali zinatumiwa kwa njia isiyofaa na nashangaa Serikali sijui kwa nini, kuna wahujumu wengi waliopo katika Serikali, watendaji. Mimi nashangaa kila siku mtu amepoteza fedha, amekula fedha lakini Serikali inamwonea huruma. Nitoe tu mfano, kuna mwaka dawa zote zimeibiwa, zimeletwa kutoka Moshi *MSD* kufika Arusha gari ikapata pancha, wakabadilisha kutoa dawa kuweka kwenye gari nyingine ndiyo dawa zote zikapelekwa sehemu nyingine ambayo haikufika, tumekaa miezi sita, wananchi wamekaa miezi sita bila kuwa na dawa, Wilaya nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wamemsimamisha Daktari, baadaye huyo Daktari akahamishwa akaletwa Simanjiro, Simanjiro amekuja tena kuiba, amesimamishwa. Sasa nimetoa mfano wa huyo mmoja katika Halmashauri zote wako watu wa aina hiyo, katika kila Halmashauri na kila Wizara kuna watu siyo wote lakini kuna watu wabaya, bado tunawalea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo ambalo halijazungumziwa wala sikuona katika Bajeti hii hapa, nalo ni suala la mifugo. Wasukuma wenzangu nilidhani bado ni wafugaji, kumbe wameacha ufugaji. Wasukuma karibu 10 wameamka leo wamechangia hakuna hata mmoja aliyezungumzia mifugo. Mama Maria Hewa tu ndiye nilimsikia kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Serikali ituelewe na ninaomba mtusikilize, naomba mtusikilize. Suala la wafugaji kutowajali katika Bajeti hii nao ni wananchi kama wale wanaotegemea korosho, pamba na mazao mengine yote. Kuna fedha ambazo hatujui sisi wafugaji ziko wapi, fedha za ruzuku, nisikilize sana Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Fedha za ruzuku, kuna kampuni ambayo imepewa fedha za ruzuku kwa ajili ya kununua dawa, kwanza hayo makampuni hatujui ni akina nani, dawa hatujui ni nani anatuuzia na wamegawanywa kwa Kanda. Hakuna

Mbunge hata mmoja anayejua kwamba mfanyabiashara fulani ndiye ana fedha za ruzuku na ndiye anayenunua dawa katika ukanda wetu, hakuna anayejua.

Sasa hizi fedha tunataka tujue utaratibu wake, haiwezekani kwamba kuna mfanyabiashara ambaye anahudumia ukanda wa Kaskazini, Manyara, Arusha, Kilimanjaro lakini sisi hatumjui na amechukua milioni kama sikosei ni milioni 440 ndiye amepewa ukanda wetu lakini hatumjui ni nani. Hivi kweli ni sahihi kutomjua mtu ambaye unamtegemea kwa dawa za mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabwawa, hatuna mabwawa ndiyo maana tunahama kila wakati lakini Serikali haitujali, hatuna masoko, soko la korosho tu ndiyo linazungumzwa katika Serikali, soko la pamba tu ndiyo linazungumzwa katika Serikali hii. Jamani katika mifugo na sisi wafugaji tunataka soko, tunategemea nchi ya Kenya lakini tunateswa na Kenya, hao Kenya hawana mifugo kama sisi wanatutegemea lakini bado wanatutesa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwa hili uangalie tena hili suala la mifugo na Serikali sasa iangalie suala hili la mifugo kwani tunataka dawa na tunataka hizo kampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, makampuni yote nane waliopewa fedha kwa ajili ya ruzuku ya dawa za mifugo ambazo hatuwajui tunataka tuwajue ni akina nani na tunataka tujue wamenunua dawa kiasi gani na hiyo bei basi kama ni punguzo tujue wamepunguza nini. Huwezi tu kutupa fedha kwamba nenda kahudumie wafugaji lakini sisi wenyewe hatuwajui ni akina nani hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa ninamuita Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi na pengine Mheshimiwa Elisa David Mollel, anaweza kufikiwa.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa kunipa wasaa huu kuweza kuchangia hoja hizi mbili zilizo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuzungumza leo hapa lakini pili napenda kuwashukuru viongozi wote wa ngazi zote wa Chama changu cha Mapinduzi kwa kunisimamisha ili kuweza kupeperusha bendera ya chama katika uchaguzi ule mdogo ambapo Chama cha Mapinduzi kiliibuka kuwa mshindi kupitia mgombea wake ambaye ni Mimi Mtutura Abdallah Mtutura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana wananchi wote wa Jimbo langu la Tunduru kwa kuwa na imani kubwa na kunipa ushindi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutoa pongezi kwa timu yetu ya Taifa ya *JK Boys* kwa kile walichokifanya na kulipatia Taifa letu sifa kubwa katika medani za michezo hususan mpira wa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitakuwa nina uchache wa fadhila bila kuwashukuru *TVT* ambao walijitahidi kutuletea matangazo yale ya moja kwa moja kupitia watangaziji wao Juma Mkamia na mwenzake Luisi Sendeu, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Napenda vile vile kutoa pole kwa wenzetu wa Singida waliopata ajali ya basi la *Mohamed Trans*, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, *Amin*! Lakini pia na kuwawezesha wale wote waliopata majeraha basi awasaidie wapone haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja hizi mbili zilizo mbele yetu lakini kwanza kabisa napenda kuunga mkono asilimia mia moja hoja zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupa rai Serikali juu ya kodi hizi za magari, nadhani tutakuwa hatuwatendei haki hasa wamiliki wa pikipiki kuwatoza shilingi 80,000/= eti tu kwa sababu chombo chao kile cha usafiri kina *cc* kati ya 1 hadi 1500. Nadhani kuna haja ya hawa wamiliki wa pikipiki wapunguziwe kodi ile yaani badala ya kuwa shilingi 80,000/= angalau ifikie shilingi 40,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika kodi hizi za magari, nadhani kuna haja vile vile ya kuyaangalia magari kama *Salon, Pick Ups,* lori pamoja na mabasi nadhani yangekuwa katika *category* moja badala ya kuangalia zaidi ujazo wa *engine* yaani *cc 1500* kwa sababu magari mengi hasa hizi *pick ups* ndiyo tegemezi kubwa la wanyoge katika maeneo mengi ya nchi yetu hasa Jimbo langu la Tunduru, tegemeo kubwa la usafiri ni hizi *pick ups.* Hatuna mabasi kule na hakuna hata Kata moja ambayo inatumia usafiri wa mabasi bali tegemeo letu kubwa ni *Land Rover* ambayo yapo katika *category* ambayo yanatakiwa yatozwe shilingi 230,000/=.

Kwa hiyo, naomba sana kwa kuwahurumia wapiga kura wa Tunduru, naomba ushuru huu upunguzwe ili uweze kutoa nafuu kwa wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani kabisa kwamba kodi hii ya mafuta ambayo imeongezwa itaelekezwa katika ujenzi wa barabara na hasa ukizingatia kwamba Wilaya ya Tunduru kwa kipindi kirefu sana mipango yote ambayo imekuwa ikipangwa juu ya ujenzi wa barabara Wilaya ya Tunduru imekuwa ikiwekwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo hili la Tunduru, Tunduru ipo Kanda ya Kusini na ukifika Kusini basi kuna Kusini ya Kusini. Kusuni ya Kusini ni Tunduru, kwa hiyo, nitashukuru sana kama Bajeti hii itaikumbuka Tunduru hasa katika ujenzi wa barabara ile ya kutoka Masasi – Tunduru hadi Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli adha ambayo wanaipata wananchi wa Tunduru ni kubwa sana kuhusu barabara kiasi kwamba maisha yanakuwa mazito na magumu sana katika maeneo yote kwa mfano bidhaa za madukani, huduma za hospitali na inafikia kipindi tunakosa madawa tu eti kwa sababu barabara haipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa fedha unaoisha ilifikia hatua miezi mitatu hospitali yetu ya Wilaya haipati dawa kwa sababu barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa kipengele hiki kimoja cha mafuta ya taa, mimi naungana na wachangiaji wenzangu nadhani kodi hii ya shilingi nne inaweza ikaleta athari kubwa sana hasa kwa wananchi wa Tunduru kwa sababu hivi tunavyozungumza sasa hivi mafuta ya taa Tunduru ni shilingi 1,000/= kwa lita. Sasa ongezeko hili litapandisha kutoka shilingi 1000/= ambayo sasa hivi wananchi wa Tunduru wananunua mafuta ya taa katika maduka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia upande wa kilimo wananchi wa Jimbo la Tunduru wanazeeka kabla ya muda wao, ukikutana na kijana wa umri wa miaka 40 wewe wa umri wa miaka 50 utamwamkia, wanazeeka kwa sababu wanatumia nguvu nyingi sana kuliko tija wanayoipata kwa sababu wanatumia jembe la mkono. Nadhani sasa hivi umefika wakati ambapo Serikali iangalie upya juu ya sera za kilimo kwani kuna haja ya makusudi kabisa Serikali iwekeze katika suala la uingizaji wa matrekta kwa bei nafuu ambayo yatakopeshwa kwa wakulima bila riba kwa sababu wengi wao hawana uwezo wa kununua matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo bado ni kero kubwa hasa kwa jimbo langu la Tunduru. Juzi wakati tupo Dar es Salaam tunahudhuria vikao vya Kamati za Bunge nililazimika kuomba ruhusa mara kwa mara ili kufuatilia pembejeo. Namshukuru sana Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu alinivumilia na hasa kwa kuelewa jukumu lililopo katika Jimbo langu la Tunduru. *(Makofi)*

Kwa hali hiyo, ni lazima nitoe shukrani za pekee kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Grey Mgonja, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Katibu Ndugu Andrew Nyumayo, pamoja na msaidizi wake Ndugu Madata kwa juhudi ambazo wamezifanya katika kuisaidia Wilaya ya Tunduru hadi leo hii pembejeo zinaelekezwa Tunduru. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la barabara ni lazima nilirejee tena, tunaiunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Tunduru tukiwa na imani kwamba makusanyo ambayo yatapatikana katika kodi hii yataelekezwa katika ujenzi wa barabara kutoka Masasi, Tunduru hadi Songea na *Mbambabay. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme na nashauri kama nilivyoshauri katika vikao vilivyopita kwamba kuna haja kabisa kwa Shirika la Umeme kujipanga upya na kuangalia gharama za uendeshaji kwa sababu kipato kinaongezeka kwa kudhibiti kile ulichonacho, mapato pamoja na usambazaji wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kiwanda cha korosho ambacho mwaka huu kimejipanga na kimerundika korosho tani 1900 zinasubiri kubanguliwa lakini hadi leo kinahangaika kupatiwa umeme na kiwanda kile kina uwezo wa kula kilowati 213, ni mteja mkubwa kabisa ambaye angeweza kutuingizia mapato ya kutosha kabisa *TANESCO.* Kwa hiyo, naomba *TANESCO* wajitahidi na waharakishe katika kuhakikisha kwamba umeme unafika mapema katika kiwanda kile ili kiweze kutoa ajira kwa wananchi wa Tunduru. *(Makofi)*

Mwisho ni kwamba naomba niishauri Wizara ya Mambo ya Nje hasa katika kuhudumia na kutoa huduma kwa wahisani hasa Mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNDP, ILO, UNICEF* na hata *UNIDO.* Hawa watu wamekuwa wakihangaika kwa kipindi kirefu sana kupata huduma kwa haraka pale Wizara ya Mambo ya Nje, inawachukua muda mrefu sana kupata *VAT Exemption* na *DAPR6.* Imefikia muda sasa tuheshimu juhudi zao kwa sababu wamekuwa wakichangia kwa muda mrefu na kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi yetu, haifai wanapofika kutaka kupata huduma katika Wizara zetu za Serikali wanachukua muda mrefu. Hii kwa kweli itakuwa ni kuwakatisha tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kutoa mwaliko kwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, nawaomba watutembelee Tunduru, waje Tunduru wajionee adha ambazo wananchi wa Tunduru wanazipata. Ninaamini kabisa kama watakuja na watajionea wenyewe adha wanayoipata wananchi wa Tunduru basi mipango ijayo wataichagua Tunduru katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawaomba waje mwezi Machi, wasije mwezi mwingine mwingine lakini waje mwezi Machi wajionee wenyewe adha ambayo wananchi wa Tunduru wanaipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado muda upo nadhani kuna haja ya kuongeza kipengele kimoja cha uwezeshaji wa wananchi. Hadi hivi ninavyozungumza hakuna hata mwananchi mmoja wa Tunduru ambaye ameshapata mkopo wa pesa zile za Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi na atamalizia Mheshimiwa Elisa Mollel.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kutamka kwamba naunga mkono hoja zilizopo mbele yetu asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyoelewa kwamba uti wa mgongo wa Taifa letu ni kilimo na Serikali yetu ina mpango wa kutilia msisitizo kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara kwenda Thailand kama sikosei, alivyorudi nchini alisema kwamba kuna mpango mzuri wa utaliwezesha Taifa letu kuutumia yaani mpango wa kutumia mvua ya kutengeneza ambayo kwa hakika nilikuwa naamini kwamba ingetukomboa vizuri sana. Tungeweza kutumia hali yetu ya hewa kama masika, vuli na baadaye huu mpango ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu alirudi nao katika Taifa letu ungetuletea tija katika uzalishaji mali lakini kwa bahati mbaya haujazungumzwa hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lililotiliwa mkazo pia viwanda vya kilimo, yaani vya kusindika baadhi ya bidhaa za kilimo, lakini kwa bahati mbaya sana sijaona mkazo uliotiliwa kwa ajili ya kuanzisha au kutoa msukumo kwa ajili ya viwanda kwa bidhaa za uvuvi, maliasili ya bahari ambayo kwa kweli Taifa letu lingeweza kufaidika kiasi cha kutosha kabisa katika bidhaa za aina hii. Kwa hiyo, naomba kutoa rai kwa Serikali kwamba ufike wakati sasa wa kufikiria kuanzisha na kusajiisha uanzishaji wa viwanda kwa ajili ya kusindika mazao ya bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa pongezi kwa Serikali, kuna mradi wa kuimarisha njia kubwa za umeme na kuboresha usambazaji umeme katika vituo vidogo. Mradi huu kwa bahati njema umeingia kwenye jimbo langu katika Kata za Vijibweni, Kibada, Mbagala Mkuu, Mbagala na Charambe. Kulikuwa na adha kubwa kwa wananchi, maeneo yao yamechukuliwa kwa muda mrefu lakini yalikuwa bado hayajapata fidia kutoka Serikalini, kwa bahati nzuri na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu waliweza kulipwa hivi karibuni karibuni shilingi bilioni 7. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Taifa letu sasa hivi linakumbwa na tatizo la wizi wa nyaya za umeme, ninaomba Serikali iliangalie suala hili kwa umakini kabisa ama sivyo tutarudi nyuma katika uzalishaji mali. Kuna maeneo kila siku matukio haya yanatokea mara kwa mara na maeneo ya viwanda pia kwa hiyo Serikali inapoteza mapato kutokana na kukosekana na uzalishaji mali. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye utaratibu maalumu za kuhakikisha inapiga vita wizi huu wa nyaya za umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa kuona kwamba Serikali hivi sasa inamiliki asilimia 100 katika shirika la *ATCL.* Lakini tunajua *ATCL* yetu ilivyo, baada ya wenzetu wa Afrika Kusini kujitoa tuna matatizo makubwa ya ndege na ndege tulizonazo ni za muda mrefu kwa hiyo, naomba kutoa rai kwa Serikali kuitazama *ATCL* na kuwaongezea nyenzo za utekelezaji ikiwemo kuwapatia ndege mpya za kisasa ili *ATCL* iwe kweli ni *ATCL* na ijulikane kama kweli ni chombo cha Taifa na isionekana kwamba *Precision Air* ni chombo cha Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *TIPER* yaani *Tanzania Italian Petroleum Refinery.* Kwa bahati mbaya kiwanda hiki Serikali tumekitupa muda mrefu sana ambacho kilikuwa kinatusaidia kwa miaka mingi sana, lakini leo *TIPER* ukipita pale kunasikitisha. Naiomba Serikali itoe tamko rasmi kuhusu kiwanda cha *TIPER* inazungumza nini? Je, tutakiendeleza au ndiyo tutakiacha moja kwa moja? Kama tumekiacha je, ni kwa sababu

zipi za msingi zinazopelekea kuiacha *TIPER* ikae kama vile ilivyo hivi sasa. Kama tumeshindwa sisi Watanzania kuiendeleza *TIPER* basi naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuzishawishi nchi jirani kama Kongo, Burundi na kadhalika ili waweze kukitumia hiki kiwanda cha *TIPER* na sisi tuweze kupata mapato kwa kupitia njia za kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la elimu. Hotuba zimezungumza kwamba kipaumbele kikubwa na changamoto ya Serikali, elimu ni mojawapo na imesema kwamba imejiandaa kwa ajili ya ujenzi wa maabara, nyumba za walimu na kadhalika. Lakini naomba kutoa wito kwamba suala la ujenzi wa nyumba za walimu upewe kipaumbele cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu kuna shule zetu sisi za vijiji walimu wanaripoti na baada ya siku mbili wanaondoka, kwa hiyo ujenzi wa shule zetu za Sekondari utakuwa hauna maana kama tukiyatazama mambo haya ikiwa ni pamoja na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuboresha afya limezungumzwa kwamba kufanya ukarabati wa hospitali za Mikoa lakini kwa bahati mbaya sana Mkoa wetu wa Dar es Salaam hauna Hospitali ya Mkoa. Naomba Serikali katika mipango yake ianze na ifikirie kwa kutupatia hospitali ya mkoa ili wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wakitoka Temeke, Kinondoni na Ilala wanakwenda wapi badala ya kwenda Muhimbili moja kwa moja ambayo ni Hospitali ya Rufaa. Tumepata maelezo kupitia swali la Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, katika kipindi hiki lakini bado naendelea kutoa wito kwa Serikali kuliona hili kwamba ni jambo muhimu kwa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, naomba kuipongeza Serikali kwa namna ilivyojiandaa kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu biashara ya bidhaa ambazo zinatoka hapa hapa Tanzania Bara. Suala hili kwa kweli litaiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuisaidia kimapato, naomba azma hii iendelezwe ni nia njema na nia njema kama alivyosema Mheshimiwa mmoja asubuhi hapa hairogwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la leseni za magari, wenzangu baadhi wamesema kwamba ni balaa, lakini mimi naunga mkono kwa sababu tunaweza kumiliki kununua gari la milioni 60 kwa nini tusiweze kulipa kodi ya shilingi 230,000/=? Labda nitoe rai kwamba badala ya kulipa kwa pamoja basi Serikali ingetoa mwanya angalau wananchi waweze kulipa kwa mfano mara mbili au kwa robo. Hiyo naomba kutoa rai kwa Serikali kwamba waweze kupunguza mzigo ambao Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekuwa wakililalamikia suala hilo ifanyike kama vile Bima inavyofanya. *(Makofi)*

Naomba niishukuru Serikali pia kwa maandalizi mazuri ya mikopo ya nyumba ambayo kwa kweli katika kampeni zetu, kwenye majukwaa yetu kila tulipofanya mkutano tumekuwa tukilizungumza hili kifua mbele kwamba Serikali yetu ya Awamu ya

Nne ya Chama cha Mapinduzi ikifanikiwa tutahakikisha kwamba wananchi wanapata mikopo ya nyumba na vifaa vya mikopo ya nyumba. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa mpango wake huu lakini naiomba ijihimize basi sheria husika ziharakishwe na njia mojawapo ya kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la fukwe zetu, fukwe zetu ni nzuri na zinavutia lakini kwa kweli hatujazitumia ipasavyo. Naiomba Serikali iangalie suala hili kwa undani kwani unapotembea katika nchi za wenzetu unakuta jinsi fukwe zinavyotumika vizuri, naomba Serikali sasa iangalie katika eneo hili ili kutafuta wawekezaji ambao wanaweza kuingia ubia na wenye maeneo haya ya fukwe au Serikali kwa mkono wake inaweza kuchukua kwa mujibu wa sheria zilizopo za nchi. Lakini fukwe nina hakika zitatuletea mapato na tija kubwa. Tuanze sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa sana kwa bahati mbaya kwenye mpango wa Serikali haikuzungumzia hata kidogo ujenzi wa daraja la Kigamboni. Ndiyo najiona huyo Mwinchoum naanguka. Lakini naomba Serikali katika majibu inisemee hilo je, daraja lipo au halipo? Tuwe na kauli sahihi kabisa ili mimi ninaporudi kule niweze kuzungumza vipi na wananchi. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake hili alizungumzie kwa kina kuhusu ujenzi wa daraja la Kigamboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafuta naunga mkono asilimia mia lakini suala la mafuta ya taa naomba kwa heshima na taadhima kwamba tuliangalie kwa kuwa linamgusa mwananchi kwa karibu sana, hili litatuletea matatizo. Ninaomba chonde chonde kwa heshima na taadhima tuliangalie kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Elisa David Mollel, msemaji wetu wa mwisho jioni hii. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufunga mjadala leo jioni. Kabla ya kuchangia nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Naibu Mawaziri wao, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa utekelezaji mzuri na wa mafanikio makubwa ya Bajeti ya mwaka uliopita yaani mwaka 2006/2007 ambayo ilikumbwa na matatizo mengi ya upungufu wa chakula, ukame na matatizo ya umeme yote hayo kwa ujumla imekuwa ni mzigo mkubwa sana katika Bajeti iliyopita. Naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti iliyopo mbele yetu ina mwelekeo wa kutoa kipaumbele kwa huduma za jamii ikiwemo elimu, maji, afya, barabara na kilimo pamoja

na kuangali maslahi ya wafanyakazi wameongezewa mshahara na wamepunguziwa kodi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi naona kwamba kwa mtazamo huu na mwelekeo huu Bajeti hii ni ukombozi kwa wananchi walio wengi na inatekeleza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa misingi hiyo naunga mkono Bajeti iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mafuta, tozo ya shilingi 100 kwa lita ya mafuta ambayo iko kwenye Bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge wote tulishirikishwa kwenye maandalizi ya Bajeti hii na sisi Waheshimiwa Wabunge tulipendekeza kwamba tuunde Mfuko wa kutengeneza barabara zetu kutokana na mvua nyingi zilizonyesha nchini kote na hatukuwa na fedha za kutengeneza barabara. Barabara hizo ziliharibika kwa kiasi kikubwa na tuliona kuna haja ya kuwa na Mfuko huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siogopi kabisa kwenda mbele ya wananchi na kueleze hii tozo ya shilingi 100 kwa lita ya mafuta ya petroli au dizeli. Aidha, tunatoza ama hatutozi na hatupati fedha za miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba mimi sina tatizo kabisa na tozo ya shilingi100 ya kuingia kwenye Mfuko wa barabara ili tutengeneze miundombinu ya barabara, isipokuwa tunaiomba Serikali kama Mheshimiwa Aggrey Mwanri, alivyosema ihakikishe kwamba tunasimamia bei ya mafuta ili isipande kiholela kwa kisingizio hiki cha tozo ya shilingi 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye maeneo mengine mawili, matatu kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza, naomba Serikali itazame kwa upya vyanzo vya mapato yetu. Mwaka hadi mwaka tumekuwa na vyanzo vichache na hivyo hivyo tunavyopanga kuongeza maendeleo yetu Serikali urudia vyanzo vilevile kutoza kodi zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba Serikali iangalie udhibiti wa matumizi ya fedha tunazokusanya. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema makusanyo ya fedha za ndani yanakwenda vizuri, lakini matumizi yake yanatupa mashaka kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo ningeomba Serikali itazame ni hili la misamaha ya kodi. Tumekuwa na misamaha ya kodi ambayo labda mara nyingine siyo ya lazima sana. Tumekuwa na misamaha ya kodi kwa viwango vikubwa sana.

Mapato tunayokusanya tunarudisha asilimia 40 kwa misamaha ya kodi. Nafahamu kuna misamaha ya kodi ambayo ipo kisheria kama tulivyoipitisha, lakini hiyo haitunyimi kutazama sheria hizo kwa upya, haitunyimi kuangalia viwango vya misamaha hii ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie miundombinu kwa ujumla. Miundombinu ninayoizungumzia hapa kwa jumla ni pamoja na barabara, reli, bandari

zetu na viwanja vya nje. Miundombinu hii kwa ujumla inahitaji fedha nyingi sana na uwezo wetu ni mdogo.

Mimi nilikuwa nataka kushauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kupata wawekezaji watakaowekeza kwenye miundombinu mbalimbali ama baadhi ya miundombinu ili sisi tupate nafasi ya kushughulikia miundombinu ile ambayo itakuwa kwenye uwezo wa mapato yetu ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake za kutafuta wahisani wa kutusaidia kujenga barabara zetu. Pamoja na jitihada hizo za Mheshimiwa Rais naishauri Serikali ifungue milango kwa wawekezaji ambao wataweza kujenga na kutoza kodi ama ushuru kwa kutumia miundombinu hiyo na baadaye waturudishie ili hali yetu ya kujifunga na kutegemea fedha za ndani tu kwa miundombinu yote iweze kutupa afueni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya *export* na *import* zetu. *Export* zetu sasa hivi ni sawa na asilimia 44 ya mali tunazoagiza nchi za nje na ni kidogo sana na asilimia hii 44 inatokana na samaki na dhahabu. Sekta zingine hazijachangia kwa kiasi kikubwa katika *exportation* ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunajiuliza hapa kuna nini? Sekta nyingine zimechangia kiasi gani katika *export bill* yetu? Tunaiomba Serikali itazame madini mengine ambayo ni *exported,* jamani hata *Tanzanite a*mbayo tuna *so monopoly* hatujui *Tanzanite* inaingiza kiasi gani? Naishauri Serikali ijitihadi ku-*promote* huu uuzaji wa madini nje na tujue kwamba ni kiasi gani tume-*export* nchi za nje hasa *Tanzanite. (Makofi)*

Nizungumzie juu ya jitihada za Serikali za dhati kabisa za kuunda *Export Processing Zones* pamoja na *Special Economic Zones. Export Processing Zones* zimeundwa miaka karibu mitatu iliyopita, lakini hadi leo hakuna chochote ambacho kimefanyika cha msingi kuanzisha hizi *Export Processing Zones.* Kilichofanyika ni kujenga miundombinu. Je, miundombinu hii itajengwa kwa miaka mingapi? Ningeishauri Serikali ijitahidi kumalizia basi ujenzi wa miundombinu hii ili tuweze kuanzisha hizi *Export Processing Zone* zitusaidie katika kupata fedha za kigeni; na *Special Economic Zones* ambazo zimekuwa *identified* kwenye Mikoa tujaribu basi sasa kuzianzisha ili zitusaidie katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya dawa za mifugo ambazo Mheshimiwa Michael Laizer amezitaja na akasema kwamba wenzetu Wasukuma walisahau mambo ya mifugo. Mimi nataka kumjibu Mheshimiwa Michael Laizer kwamba hawajasahau ni kwamba ng'ombe siku hizi wanasikia dua ya Kimasai tu. Kwa hiyo, wamesahaulika na Wakusuma. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wa Mikoa mingine hatujaona kabisa ruzuku ya dawa za mifugo wala hatujui hiyo ruzuku inapatikana wapi. Tunaomba tupate taarifa ya mwaka 2006/2007 kwamba fedha hizo zimekwenda wapi na zimetumika vipi na

tuambiwe pia kwamba katika mwaka huu wa fedha tunapata kiasi gani katika Sekta ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya Halmashauri zetu kwa jumla kuhusu matumizi ya fedha za Serikali. Taarifa ya *Controller and Auditor General* imebainisha mapungufu mengi sana katika utendaji na uwekaji wa hesabu za fedha katika Halmashauri zetu na hali hii ikiendelea namna hiyo na wakati huu sasa ambapo tunazungumzia *Decentralization by Devaluation (D by D)* hali hii inaweza kuwa mbaya na fedha hizi zote ambazo tunajaribu kuzitafuta na kuzi-*allocate* hapa kwenye miradi mbalimbali na kwenye shughuli za huduma za jamii zinaweza zikatumika visivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeiomba Serikali isisimamie kwa ukaribu zaidi Halmashauri zetu na wale ambao watakuwa wamehusika na ubadhirifu wachukuliwe hatua za kisheria. Tusipofanya hivyo hata kazi hiyo yote tunayoifanya ya kukusanya mapato na kuyapanga kwa kadri tunavyoweza itakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie juu ya maboresha ya Sekta ya Fedha kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyotangulia kuzungumzia. Maboresha ya Sekta ya Fedha ni muhimu sana na tunaomba Serikali iharakishe maboresha haya ili wananchi kama Waheshimiwa Wabunge wenzangu walivyosema wawe wamejibiwa kero zao za kujenga nyumba bora za kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba nimalizie hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa siku ya leo huyo ndiye aliyekuwa msemaji wetu wa mwisho na kesho tutaendelea.

Naomba wale watakaopata nafasi wakaangalie kwenye ubao wa matangazo kama majina yao yapo ama hayapo. Kwa sababu wengine mnakuja mnamuulize Spika, nimo au simo. Tunajitahidi kufuata kama tulivyoweka kwenye ubao wa matangazo. Lakini nadhani kesho tutaanza na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha na Mheshimiwa Pindi Chana na wengine watavyoendelea.

Waheshimiwa Wabunge, vinginevyo naomba niwashukuru sana kwa kazi nzuri tuliyofanya kwa siku ya leo. Nawatakia usiku mwema. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,*
*Tarehe 20 Juni, 2007 saa tatu asubuhi)*